# OFISI YA RAISI.

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## NUKUU ZA SOMO LA KISWAHILI.

## DARASA LA SABA.

## MWAKA: 2021.

# KUWASILIANA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

## KUWASILIANA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

**Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika muktadha mbalimbali.**

### MAZUNGUMZO

Mazungumzo ni utaratibu wa kuongea baina ya pande mbili ambapo kwa kawaida wahusika ni watu.

**a) Kubainisha na kueleza sifa za mashairi ya kimapokeo na kisasa na kuyatofautisha**

**MASHAIRI:**

Mashairi ni tungo zenye kutumia mapigo ya silabi kwa utaratibu maalumu wa kimuziki kwa kutumia lugha ya mkato, lugha ya picha na tamathali za semi.

Mashairi hueleza mambo yanayohusu binadamu na maisha yake ya kila siku. Tungo hizi huwa za aina nyingi kutegemeana na dhamira mbalimbali kama vile mashairi yawasifu, uzindushi, waadhi, simango na majigambo.

Shairi huwa na mlingano wa sauti za herufi, lugha tamu na fupi na pia hubeba mawazo, maono na fikra nzito inayofanya moyo uathirike.

Shairi huwa na urari wa mizani wenye lugha isiyo na matusi. Shairi pia huwa na vina vinavyopatana na muwala pamoja na maana iliyo bora yenye mafunzo, furahisho,

maarifa na kasida za kusifika.

Mashairi huweza kuandikwa au kutungwa kulingana na jinsi yanavyoonekana. Hii ina maana kuwa mashairi huweza kutofautishwa kwa idadi ya mishororo, jinsi maneno

yalivyopangwa, urari wa vina n.k.

- Mtu anayetunga shairi huitwa **Malenga** na mtu anayeimba shairi huitwa **Manju.**

**MASHAIRI YA KIMAPOKEO**

**MAANA:**

Haya ni mashaini yanayozingatia kanuni za muwala/urari (ulinganifu) wa mizani, vina, idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi. Vilevile mashairi haya huitwa **mashairi funge.** Mashairi haya ya kimapokeo ni ya jadi. Yaani yalikuwepo katika jamii kwa muda mrefu.

**SIFA ZA MASHAIRI YA KIMAPOKEO**

**1. BETI**

Shairi hugawanyika katika beti, ambapo kila aya moja huitwa ubeti. Kwa kawaida ubeti wa shairi la kimapokeo huwa na mistari minne. Urefu wa kila mstari hulingana na mwingine kwa idadi ya mizani.

**2. VINA**

Vina ni silabi zenye sauti ya namna moja zinazotokea katikati au mwishoni mwa kila mshororo wa kila ubeti wa shairi. Hivyo, kuna vina vya kati na vina vya mwisho. Ili shairi lihesabike kama limetumia vina ni lazima herufi za kati na herufi za mwisho za kila ubeti ziwe zinafanana.

**3. KITUO**

Ni mstari (mshororo) wa mwisho katika kila ubeti wa shairi ambao huonesha msisitizo wa ubeti mzima au shairi zima. Wakati mwingine huitwa **kibwagizo/korasi/mkarara kiitikio.**

**4. MIZANI**

Mizani ni ulinganifu wa idadi za silabi katika kila kipande au mistari ya ubeti wa shairi. Mara nyingi mashairi ya kimapokeo huwa na mizani nane (8) kwa kila kipande, na mizani kumi na sita (16) kwa kila mstari mshororo).

**5. KIPANDE**

Ni mgao au kisehemu kimojawapo katika visehemu viwili vya mshororo wa shairi ambavyo hutenganishwa na alama ya mkato. Mwishoni mwa kila kipande katika

mshororo kuna kina. Mfano:

Mavazi kuangalia, vizuri tuyatunzeni,

Kufua na kupasia, vijidudu tuucni,

Usafi kuzingatia, kwetu ni nguzo

jamani, Tuzingatia usafi, kuzilinda afya

zetu.

Katika ubeti huu kuna vipande viwili katika kila mstari:

Mavazi kuangalia - kipande cha kwanza

Vizuri tuyatunzeni - kipande cha pili

Kina cha kati ni "a" ni kina cha mwisho ni "ni"

**6. MUWALA**

Muwala ni mtiririko wa mawazo na fani ulio na mantiki katika shairi. Muwala unaweza kuwa na namna mbili:

i. Ni lazima mawazo katika kila ubeti yawe yanafuatana kwa ufasaha kutoka mwanzo ili kuyaweka mawazo kikamilifu.
ii. Kila mshororo katika kila ubeti lazima ujitosheleze kimaana. Aidha, inapasa shauri liwe na mtiririko mzuri wa mawazo kutoka ubeti hadi ubeti.

Shairi la kimapokeo ni fani na sanaa inayofungamana na kanuni maalumu zinazotofautisha ushairi na fani nyingine za fasihi. Iwapo kanuni, ada na kiada hizo zitakiukwa itakuwa ni kuvuruga utamaduni wa shairi la kimapokeo.

Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali:

1. Dunia kuna watu wengi walofanikiwa,
   Sio kwamba wana utu, kuzidi niliopewa,
   Ila si waoga katu, ndipo wamefanikiwa,
   Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

2. Mambo yakiwa magumu, kukata tamaa mwiko,
   Shida zikizidi humu waloshinda mbona wako,
   Najipia majukumu, kupambana buko huko
   Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

3. Sipungukiwi chochote, iweje nife maskini.
   Akili na mali yote, nimeshika mkononi,
   Naweza kwenda popote, kwishi humu duniani,
   Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

**MASWALI:**

A. UFAHAMU:

Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi:

1. Shairi hili lina beti ngapi?

**Jibu:**

- Shairi hili lina beti tatu.

2. Katika shairi hili, kila ubeti una mistari mingapi?

**Jibu:**

- Katika shairi hili kila ubeti una mistari minne.

3. Shairi hili lina mizani mingapi kwa kila mshororo?

**Jibu**

- Shairi hili lina mizani kumi na sita kwa kila mshororo,

4. Methali gani unadhani ingefaa kwa shairi hili?

**Jibu:**

- Methali ambayo ingefaa kwa shairi hili ni penye nia pana njia

5. Vina vya kati vya ubeti wa pili wa shairi hili ni vipi?

**Jibu:**

- Vina vya kati vya ubeti wa pili ni "mu".

6. Taja mstari wa kibwagizo katika shairi ulilosoma.

**Jibu;**

- Mstari wa kibwagizo ni Sitakubali kushindwa, lazima nifanikiwe.

B. MSAMIATI:

Toa maana ya msamiati ifuatayo kisha tunga sentensi.

## 1. Dunia

Sayari ambamo tunaishi, ulimwengu.

SENTENSI

Mwalimu alitufundisha kuwa katika mpangilio wa sayari, dunia ni sayari ya tatu.

**2. Akili**

i. Uwezo wa kuelewa na kujifunza mambo.

ii. Uwezo wa kufikiri na kuamua kwa busara.

SENTENSI

Mwanafunzi mwenye akili hupendwa na walimu,

**3. Mwoga**

Mtu au mnyama mwenye tabia ya kuchelea mapambano au hatari.

SENTENSI

Mjomba alituambia mtu mwoga hapati mafanikio katika maisha.

C. MAZOEZI YA LUGHA:

Andika sentensi hizi kwa kutumia kinyume cha neno lililopigiwa mstari.

1. Nani amevuruga kabati?

Jibu:

- Nani amepanga kabati?

2. Mpanda vizuri hula hovyo.

Jibu:

- Mpanda vibaya hula hovyo.

3. Nilisikitika kwa kuwa umeanzisha mradi wa kununua na kuuza mboga.

Jibu:

- Nilifurahi kusikia umeanzisha mradi wa kununua na kuuza mboga.

4. Bandikeni hizi picha ukutani.

Jibu:

- Bandueni hizi picha ukutani.

5. Itakuwa bora ukawie kufika ili ukute ofisi imefunguliwa.

Jibu:

- Itakuwa bora uwahi kufika ili ukute ofisi imefunguliwa.

6. Nikilala kifudifudi ninaota ndoto za kutisha.

Jibu:

- Nikilala chali ninaota ndoto za kutisha.

7. Funua mfuniko ili maziwa yachemke haraka.

Jibu:

- Funika mfuniko ili maziwa yachemke haraka.

8. Serikali inatamka kila raia kufanya kazi haramu.

Jibu:

- Serikali inatamka kila raia kufanya kazi halali.

**Ondoa silabi moja kutoka katika kila neno ili upate neno jipya la Kiswahili:**

i. Dhamira
ii. Kithiri
iii. Tahayari
iv. Filisi
v. Pindukia

Majibu

i. Dhara
ii. Kiri
iii. Tayari
iv. Fisi
v. Pikia

D. METHALI:

Malizia methali zifuatazo:

1. Mgagaa na upwa______________________________
2. Kiburi si__________________________
3. Kuvuja kwa pakacha________________________

4. Akufaaye kwa dhiki_________________________

5. Penye nia______________________
6. Mkaidi hafaidi_________________________
7. Kuuliza_____________________

**Majibu:**

1. hali wali mkavu
2. maugwani
3. nafuu ya mchukuzi
4. ndiye rafiki
5. pana njia
6. hadi siku ya idi
7. si ujinga

**MASHAIRI YA KISASA**

Haya ni mashairi yasiyozingatia kanuni za muwala/urari (ulinganifu) wa mizani, vina, na idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi. Mashairi haya pia huitwa **mashairi ghuni, masivina au mapingiti.**

Mashairi haya hayatumii vina na mizani kujenga mdundo. Mashairi haya huunda midundo kwa kuzingatia viwango mbalimbali vya lugha kama vile mofolojia, sarufi na mantiki. Katika kila kimojawapo cha viwango hivi kuna uwezekano pia wa midundo kadha wa kadha. Viwango hivi vinaweza kuzingatiwa katika utunzi ili kuleta muwala au mtiririko mzuri wa habari.

Ulinganifu mashairi ya kisasa hutegemea sifa za kisimu na kimantiki. Sifa hizo ni:

i. Mnyambuliko wa maneno
ii. Mpangilio wa mshororo
iii. Ruwaza za mishororo na beti

Aidha mashairi ya kisasa hutumia beti kwa ubunifu mkubwa. Kuna uwezekano wa mshororo mmoja mmoja kujenga ubeti. Hii ni njia mojawapo ya kulikuza jambo au wazo linalozungumzwa kwa njia ya uchanganuzi.

Mfano:

1. Busara na maanfa ni sawa na ujinga na upumbavu,
   Furaha na kicheko ni sawa na kilio na huzuni,
   Njia yenye mwanga ni sawa na njia yenye giza,

Ukitenda wema unaweza kulipwa mabaya.

2. Mwenzako akimwaga ugali,
   Wewe mwaga unga,
   Na mwenzako akimwaga mboga,
   Mwaga mafuta.

3. Lakini yote haya yataisha,
   Binadamu wenzangu,
   Tambueni dunia imegeuka,
   Mbele kumekua nyuma,
   Na nyuma kumekuwa mbele,
   Dunia imegeuka kuwa tambara bovu,
   Ukilishika linachanika,
   Dunia sasa mti mkavu,
   Usiofaa kuchimba dawa.

**TOFAUTI KATI YA MASHAIRI YA KIMAPOKEO NA MASHAIRI YA KISASA**

❖ **MASHAIRI YA KISASA**

i. Hayazingatii urari wa vina na mizani wala idadi ya mishororo katika beti.
ii. Hayana idadi maalumu ya mistari katika ubeti mmoja.
iii. Hutumia takriri nyingi ili kusisitiza ujumbe.

❖ **MASHAIRI YA KIMAPOKEO**

i. Huwa na urari wa vina na mizani na idadi ya mishororo.
ii. Yana idadi maalumu ya mistari katika ubeti mmoja.
iii. Hayatumii takriri nyingi katika kusisitiza ujumbe.

**MASWALI:**

A. UFAHAMU:

1. Katika shairi ulilosoma hapo juu ni aina gani ya shairi?

Jibu:

- Shairi hili ni la kisasa.

2. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili.

Jibu:

- Dhamira ya mtunzi wa shairi hili ni kwamba binadamu sasa wamegeuka hawana hekima wala busara. Binadamu hawana upendo, huishi kwa kushindana (mwenzako akimwaga ugali wewe mwaga unga).

3. Bainisha sifa zinazotofautisha shairi la kimapokeo na shairi la kisasa.

Jibu:

**SHAIRI LA KIMAPOKEO:**

i. Lina urari (ulinganifu) wa vina na mizani na idadi ya mishororo katika beti.
ii. Lina idadi maalumu ya mishororo katika ubeti mmoja
iii. Halitumii takriri nyingi katika kusisitiza ujumbe.

**SHAIRI LA KISASA:**

i. Halizingatii urari wa vina na mizani, idadi ya mishororo katika beti.
ii. Halina idadi maalumu katika ubeti mmoja.
iii. Hutumia takriri nyingi ili kusisitiza ujumbe

4. Andika kichwa cha habari cha shairi hili.

Jibu:

Kichwa cha habari cha shairi hili ni **DUNIA TAMBARA BOVU.**

B. MSAMIATI:

Tunga sentensi kwa kila msamiati.

**1. Hekima:**

Kiongozi wetu wa kijiji hutumia <u>hekima</u> anapoongea na wanakijiji.

**2. Furaha:**

Nilipofaulu mitihani yangu nilipata <u>furaha</u> moyoni mwangu.

**3. Dawa:**

Mtoto alipopelekwa hospitali kutibiwa daktari alimpa dawa.

**4. Ugali:**

Kila siku mchana mama hupika ugali na dagaa.

**5. Wema:**

Mjomba alituambia tuwatendee walemavu wema.

C. MIUNDO:

Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.

**1. Sharti**

- Sharti mlipe ada ndiyo mje shuleni.
- Sharti tumngojee mama ndipo tule chakula.

**2. Hata hivyo**

- Hata hivyo tumechoka kulima.
- Hata hivyo tutarudi mapema.

**3. Kwetu**

- Nyumbani kwetu kuna kuku wengi.
- Shambani kwetu kuna mboga nyingi.

D. ANDIKA VISAWE VYA MANENO YAFUATAYO:

i. Ubwabwa
ii. Keti
iii. Treni
iv. Ugali
v. Kauzu
vi. Lumbwi
vii. Mwana
viii. Barua
ix. Mwangaza
x. Macho

**Majibu:**

i. Wali

ii. Kaa
iii. Gari Moshi
iv. Sima
v. Dagaa
vi. Kinyonga
vii. Mtoto
viii. Waraka
ix. Nuru
x. Maninga

E. MAZOEZI YA LUGHA

Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali ya mazoea:

1. Mafundi wanakarabati hospitali ya kijiji.

Jibu:

- ❖ Mafundi hukarabati hospitali ya kijiji.

2. Jogoo anawika alfajiri.

Jibu:

- ❖ Jogoo huwika alfajiri.

3. Wanafunza wanasoma kwa bidii.

Jibu:

- ❖ Wanafunzi husoma kwa bidii.

4. Mtoto amelia kwa sauti kubwa.

Jibu:

- ❖ Mtoto hulia kwa sauti kubwa.

5. Baba alisafiri umbali mrefu kwenda

hospitali Jibu:

- ❖ Baba husafiri umbali mrefu kwenda hospitali.

Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita:

1. Hadija anacheza vizuri nyimbo za kwao.

Jibu:

- ❖ Hadija alicheza vizuri nyimbo za kwao.

2. Wao watakula wali.

Jibu:

- ❖ Wao walikula wali.

3. Samaki wamepungua sokoni.

Jibu:

- ❖ Samaki walipungua sokoni.

4. Mvua za vuli zitaanza kunyesha mapema.

Jibu:

- ❖ Mvua za vuli zilianza kunyesha mapema.

5. Baba ameanguka kwenye korongo.

Jibu

- ❖ Baba alianguka kwenye korongo.

6. Sisi tunasoma darasa la sita.

Jibu:

- ❖ Sisi tulisoma darasa la sita.

7. Mwanariadha ametunukiwa medali ya dhahabu.

Jibu:

- ❖ Mwanariadha alitunukiwa medali ya dhahabu.

**b) Kutunga mashairi va kimapokeo yenye mishororo minne kwa kuzingatia kanuni**

**za utunzi wa mashairi na kuvahusianisha na maisha ya kila siku.**

Katika utungaji wa mashairi ya kimapokeo ni lazima kuzingatia ulinganifu wa mizani, yaani silabi zinazolingana katika kila mishororo minne ya beti. Vilevile mashairi ya kimapokeo huzingatia kanuni za kuwa na vina vya kati na vya mwisho vinavyofanana kwa kila ubeti.

**SHAIRI LA KIMAPOKEO**

1. Nyumbani kwako kuzuri, hata pawe pangoni,
   Nyumba yako ni johari, ya wenzako sitamani,
   Hata pawe kwa tajiri, hapafai maishani,

2. Kwa watu usitamani, jenga yako maskani,
   Utaishi kwa amani, hapa kwetu duniani,
   Usijisikie duni, kujiita masikini,
   Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.

3. Ni bora uwe na kwako, hata pawe msituni,
   Ukila wako ukoko, furahi sana moyoni,
   Fuga na vijibwa koko, viishi kwako uani,
   Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.

4. Ukijenga nyumba yako, utaishi kwa amani,
   Sitamani za wenzako, hizo hazikuauni
   Ulikopanga si kwako, hata pawe ghorofani,
   Nyumbani kwako johari, kwingine usitamani.

**MASWALI**

A. UFAHAMU

Jibu maswali yafuatayo:

**1.** Shairi hili lina beti ngapi?

Jibu:

- Shairi hili lina beti nne.

**2.** Mwandishi anatushauri kila mtu awe na nini?

Jibu:

- ❖ Mwandishi anatushauri kila mtu awe na nyumba yake.

**3.** Mwandishi anawashauri nini watu waliopanga?

Jibu:

- ❖ Mwandishi anawashauri watu waliopanga wajenge nyumba zao hata kama walikopanga ni pazuri na wanalipa kodi lakini bado sio nyumba zao.

**4.** Mwandishi anasema mtu akijenga nyumba yake ataishije?

Jibu:

- ❖ Mwandishi anasema mtu akijenga nyumba yake ataishi kwa amani.

**5.** Kituo katika shairi hili ni kipi?

Jibu:

- ❖ Nyumbani kwako johari kwingine usitamani

**6.** Katika ubeti wa kwanza mwandishi anatufundisha nini?

Jibu:

- ❖ Mwandishi anatufundisha tusitamani vitu vya watu hata viwe vizuri bavitusaidii; tufanye bidii tuwe na vitu vyetu wenyewe

B. MSAMIATI:

Tunga sentensi kwa kila msamiati:

**1. Johari**

Jibu:

- ❖ Mwalimu alitufundisha maana ya johari kwamba ni kitu cha thamani.

**2. Tajiri**

Jibu:

- ❖ Jirani yetu ni tajiri lakini ni mchoyo.

**3. Ukoko**

Jibu:

- ❖ Mdogo wangu anapenda ukoko wa ubwabwa.

Jibu:

**4. Nyumba**

Jibu

- ❖ Tulipokwenda kijijini kumsalimia bibi tuliziona nyumba zilizoezekwa kwa nyasi.

**5. Duni**

Jibu:

- ❖ Mjomba alitumbia tukifanya kazi kwa bidii maisha yetu hayatakuwa duni.

**C. MAZOEZI YA LUGHA:**

Katika kundi la maneno A na B chagua neno sahihi ili kukamilisha sentensi.

Kundi A - **Ndege, nahodha, rubani, dereva**

Kundi B - **Meli, gari, ndege**

i. ______________________ilipoharibika ghafla baharini__________________alitoka na kuogelea hadi nchi kavu.

Jibu:

- ❖ Meli ilipoharibika ghafla baharini nahodha alitoka na kuogelea hadi nchi kavu.

ii. Tulipokuwa tunasafiri______________letu lilitumbukia kwenye mtaro kwa uzembe wa________

Jibu:

- ❖ Tulipokuwa tunasafiri gari letu lilitumbukia kwenye mtaro kwa uzembe wa dereva.

iii. _______________ilitua salama ingawa_________wake alisema kuna hitilafu katika injini moja.

Jibu:

- ❖ Ndege ilitua salama ingawa rubani wake alisema kuna hitilafu katika injini moja.

**Andika vitawe vya maneno haya:**

1. Mlango:

i. Ukoo au watu wenye asili moja.
ii. Sehemu ya kuingia kwenye nyumba.

2. Fua:

i. Unda vyombo/vifaa mbalimbali kwa kupiga chuma.
ii. Osha nguo

3. Vua:

i. Toa nguo kutoka mwilini.
ii. Toa samaki kwenye maji.

4. Kiboko

i. Mnyama mkubwa wa baharini.
ii. Silaha inayotumika kwa kuchapa au kupiga.

5. Kaa:

i. Schemu yenye moto ya kuni.
ii. Keti chini.
iii. Mnyama wa majini.

Chagua herufi ya jibu sahihi:

1. Sisi____________________tulikwenda shambani.

A. Wote
B. Sote
C. Nyote
D. Nae

2. Uniwie_________________nimechelewa kufika nyumbani.

A. Radhi
B. Huruma
C. Msamaha
D. Adhabu

3. Mtu hodari asiyeogopa kwa neno moja huitwa_________________

A. Mkaidi

B. Gaidi

C. Jambazi

D. Jasiri

E. Mtoto

4. Loo! Sukari yote ______________

A. Zimemwagika

B. Imemwagika

C. Umemwagika

5. Meli________________baharini.

A. Imetia nanga

B. Imetua

C. Imefika

D. Imeondoka

6. Neno "mboni" lina silabi ngapi?________________

A. Moja

B. Tatu

C. Tano

D. Mbili

| | |
|---|---|
| 1. | **B** |
| 2. | **A** |
| 3. | **D** |
| 4. | **B** |
| 5. | **A** |

**c) Kutunga mashairi ya kisasa yenye beti sita au zaidi na kuyahusianisha na maisha ya kila siku.**

**MASHAIRI YA KISASA:**

Maana:

Haya ni mashairi yasiyozingatia kanuni za muwata, urari (ulinganifu) wa mizani, vina, na idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi

**SHAIRI LA KISASA:**

1. Nchi yetu Tanzania
   Kwa furaha naisifia
   Rais wetu hakika
   Shukrani nyingi tunampa
   Wajibu wake kautimiza
   Bila ya rushwa kuingiza.

2. Rais wetu
   Elimu bure katupa
   Watu wengi kushangilia
   Na pongezi kumpatia
   Furaha nyingi Watanzania

3. Viwanda vingi vimejengwa
   Miundo - Mbinu zimeboreshwa
   Bila rushwa kufanyika
   Na sheria kutimizwa.

4. Najivunia kuwa Mtanzania
   Vitu vingi kumiliki
   Amani na furaha
   Watu kushirikiana
   Kila sekta kuimarika
   Nchi yetu kuendelea.

MASWALI:

a. UFAHAMU:

1. Mtunzi wa shairi anaizungumzia nchi gani?

Jibu:

- Mtunzi wa shairi anaizungumzia nchi ya Tanzania,

2. Rais wa nchi hiyo katoa nini bure?

- Rais wa nchi hiyo katoa elimu bure.

3. Wananchi wa nchi hiyo wanajivunia nini katika ubeti wa nne wa shairi?

Jibu:

- Wananchi wa nchi hiyo wanajivunia kuwa na amani, furaha na ushirikiano.

4. Katika shairi hili, mtunzi anazungumzia ujenzi wa viwanda na miundombinu. Vitu hivi vina faida gani kwa wananchi?

Jibu:

- **Faida ya viwanda:**

  Ni watu kupata ajira kutokana na kufanya kazi visandani. Pia wananchi kupata bidhaa zinazozalishwa kutoka viwandani na kuacha kutegemea bidhaa kutoka nje ya nchi. Vilevile kuongeza pato la Taifa.

- **Faida ya miundombinu:**

  Mfano; barabara watu wanaweza kusafiri kwa haraka kwa sababu ya uhakika wa barabara na hupelekea kuwepo kwa biashara.

5. Je, shairi hili lina urari wa vina na mizani?

Jibu:

- Shairi hili halina urari wa vina na mizani.

b. MSAMIATI:

Tunga sentensi kwa kila msamiati:

**1. Elimu**

Baba alituambia tusome kwa bidii kwani elimu ni ufunguo wa maisha.

## 2. Amani

Baba wa Taifa Hayati Mwalimu J. K. Nyerere alituambia tulinde amani ya nchi yetu.

**3. Sheria**

Mwalimu alitumbia ni lazima kufuata sheria za shule.

**4. Rushwa:**

Mjomba alituambia kwamba rushwa ni adui wa haki.

**5. Wajibu:**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kusoma kwa bidii.

c. MAZOEZI YA LUGHA:

Chagua maneno kwenye kisanduku kisha jaza nafasi wazi:

- Timilifu
- Huba
- Tumeamua
- Shaibiu
- Maajuza
- Tufadhili
- Gubu
- Bilashi
- Kumhimidi

1. Wakati wa mkutano, waziri alipokea____________za watumishi wa wizara yake.
2. Maneno yake yalijaa_____________
3. Serikali ilitoa msaada wa chakula kwa__________________
4. Wajumbe walikataa taarifa ya mwenyekiti kwa madai kwamba haikuwa na ______________
5. Mwaka huu_____________kushinda mechi zote.
6. Ingawaje mzee Juma alikuwa na mali nyingi, hakuwahi_____________Mungu.
7. Baba yangu amekuwa____________kwani ana miaka mia moja sasa.
8. Ni lazima_________________watu wenye mahitaji maalumu.
9. Baada ya timu mbili za mpira wa miguu kurushiana maneno ikatokea_________________na watu wakaumizana
10. Askari alifyatua risasi__________________baada ya kushikwa na kichaa cha ghafla.

**Majibu:**

1. Hoja
2. Huba
3. Maajuza
4. Bilashi
5. Tumeamua
6. Kumhimidi
7. Shaibu
8. Tufadhili
9. Gubu
10. Timilifu

**Kamilisha methali zifuatazo:**

1. Mkita ago hanyeli - **huenda akauya hapo**
2. Mchovya asali - **huchonga mzinga**
3. Aingiaye msituni - **hasikilizi matawi**
4. Akupendaye - **hukuasa**
5. Kila mlango - **tina ufunguo wake**
6. Kukalia kiti kikubwa - **hakikupi ufalme**
7. Maarifa ni bora - **kushinda utajiri**
8. Maji ya kuomba **- hayakati kiu**
9. msema kweli – **Hana rafiki**
10. Mwanzi mchanga - **si wa kujengea**

**d. Kugbani tenzi na kueleza ujumbe unaopatikana na kuhusianisha na mazingira ya kila siku**

**TENZI**

Tenzi ni tungo ndefu za ushairi zinazoelezea juu ya jambo fulani na huwa na pande moja yaani huwa na vina vya kati tu.

Utenzi huweza kuwa maelezo ya wasifu wa mtu fulani, jambo fulani la kihistoria au jambo lolote zito linaloelezwa kwa maelezo marefu.

Tenzi huwa na beti nyingi kuliko mashairi na pia hutegemea jambo lenyewe na ufundi wa mtunzi.

**SIFA ZA UTENZI:**

Zipo sifa mbalimbali za utenzi za kipekee kabisa katika upande wa fani. Sita bizo ni:

i. Utenzi una beti nyingi kuliko mashairi.
ii. Utenzi una upande inmoja yaani huwa na vina vya kati tu
iii. Utenzi una mistari minne, mistari mitatu ya kwanza huwa na vina vyenye urari sawa. Lakini mstari wa mwisho unakuwa na vina tofauti.

**UTENZI**

1. Sekunde hamza muda
   Kuhesabu siyo shida
   Maneno haya shahada
   Shika yasikuponyoke
2. Dakika huenda mbio,
   Tena bila ya mlio,
   Sitini bila salio,
   Saa moja imetimu

3. Dazani moja ya saa,
   Na nyingi ongezea,
   Siku imeshatimia
   Milango tunafungua.

4. Siku zikifikia'saba,
   Zenye saa si haba,
   Na dakika zenye buba,
   Wiki tumekamilisha.

5. Wiki nne zikifika,
   Mwezi umekamilika,
   Siku zaenda haraka,
   Mwaka tunachungulia.

6. Miezi kumi na mbili,
   Yenye wingi wa shughuli,
   Siku zaenda haraka,
   Mwaka tunachungulia.

7. Miaka kumi nasifu,
   Mwongo ulio timilifu,
   Sibashiri nakwarifu,
   Muda unasonga mbele.

8. Karne miongo kumi,
   Aseme yeye na mimi,
   Tutamke kwa ulimi,
   Karne miaka mia.
9. Miaka kufika elfu,
   Milenia timilifu
   Kare kumi nasifu
   Milenia kufikisha.

10. Tamati nimefikia.
    Mwisho wa kufuatia
    Mwisho wa kufurahia,
    Hakuna wa kufikia,
    Ila dunia yenyewe.

**MASWALI**

a) UFAHAMU:

1. Utenzi huu una beti ngapi?

Jibu:

- ❖ Utenzi huu una beti kumi.

2. Kila ubeti una mishororo mingapi?

Jibu:

- ❖ Kila ubeti una mishororo mine.

3. Utenzi huu unaelezea nini?

Jibu:

- ❖ Utenzi huu unaelezea jinsi muda unavyoanza hadi kufikia milenia.

4. Kati ya sekunde na dakika ipi ni ndogo na kwa nini?

Jibu:

- Iliyo ndogo ni sekunde kwa sababu sekunde sitini (60) ndio tunapata dakika moja.

S. Kutokana na utenzi huu karne kumi zinaitwaje?

Jibu:

- ❖ Karne kumi zinaitwa milenia.

6. Saa ngapi hufanya siku moja?

Jibu:

- ❖ Saa 24 hufanya siku moja.

7. Miezi mingapi hufanya mwongo mmoja?

Jibu:

- ❖ Miezi 120 hufanya mwongo mmoja.

8. Miongo mitatu ni miaka mingapi?

Jibu:

- ❖ Miongo mitatu ni miaka thelathini (30).

9. Unafikiri kichwa cha utenzi kiitwe nini?

Jibu:

- ❖ Kichwa cha utenzi huu kiitwe MUDA

10____________dakika, saa,________________mwezi, mwaka, mwongo,_____________na________

b) MIUNDO:

Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayol

1____________jinsi ya________________

Jibu:

- ❖ Maana alinifundisha jinsi ya kupika maandazi

2._____unde si punde____________________

Jibu:

- ❖ Walipoanzia kuchimba shimo punde si punde walimfukia nyoka,

3. Licha ya _______________

Jibu:

- ❖ Licha ya kuwa karibu na bahari hawawezi kuvua samaki.

4. ____________________kwa niaba _________________

Jibu:

- ❖ Alisoma risala mbele ya mratibu kwa niaba ya wanafunzi wote.

5. _______________sharti__________________

Jibu:

- ❖ Ukitaka kufaulu vizuri sharti usome kwa bidii.

c) MAZOEZI YA LUGHA:

Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari

1. Yule aliyevaa taji ndiye mfalme wao.

Jibu:

- ❖ Yule aliyevaa taji ndiye malkia wao.

BI

2. Alipokuwa akikwea mtini aliteleza akaanguka.

Jibu:

- ❖ Alipokuwa akishuka mtini aliteleza akaanguka.

3. Elimu ya msingi ndiyo mwisho wa upeo wa elimu.

Jibu:

- ❖ Elimu ya msingi ndiyo mwanzo wa upeo wa elimu.

4. Wageni wetu walifika wakati wa

mawio, Jibu:

- Wageni wetu walifika wakati wa machweo.

5. Nani amekudanganya kuwa dawa ni chungu?

Jibu:

- ❖ Nani amekudanganya kuwa dawa ni tamu?

6. Gunia hili ni dogo sana kwangu. Itabidi umpelekee mdogo wangu.

Jibu:

- ❖ Gauni hili ni kubwa sana kwangu. Itabidi umpelekee mkubwa wangu.

7. Hapa Somanga ni mbali sana na

mjini Jibu:

- ❖ Hapa Somanga ni karibu sana na mjini.

8. Nani amekukataza kupita hapa?

Jibu:

- ❖ Nani amekuruhusu kupita hapa?

**Chagua herufi ya jibu sahihi:**

1. Wanafunzi wangalisoma kwa bidi____________________mtihani

A. Wamefaulu
B. Wangefaulu
C. watafaulu

2. Makamu wa Rais alitoa hotuba______________ya Rais wa nchi

A. Kwa niaba
B. Kwa sababu
C. Kwa ajili
D. Kwama

3. Nilipofika shuleni asubuhi_________________kiranja anatekeleza majukumu yake

A. Nitamkuta
B. Sijamkuta
C. Nilimkuta

D. Mnakula

4. Maneno yafuatayo yapo katika kundi gani? Vitungu, iliki, mdalasini, binzari tangawizi.________

A. Viungo
B. Vyakula
C. Nafaka
D. Matunda

5. Nidhamu maana yake ni________________

A. Tabia mbaya
B. Tabia nzuri
C. Safi
D. Jeuri sana

**MAJIBU:**

| | |
|---|---|
| 1. | **B** |
| 2. | **A** |
| 3. | **C** |
| 4. | **A** |
| 5. | **B** |

**e kuchambua maudhui yote yaliyomo katika mashairi ya kimapokeo na kisasa, kuyaclezea na kuyahusianisha na mazingira ya kila siku.**

**KUCHAMBUA** ni kitendo cha kuichunguza kazi ya fasihi kwa makini na kuhakiki, kutathmini na kuainisha ubora na udhaifu wa kazi hiyo kwa kutumia vigezo vya fani na maudhui.

**MAUDHUI**

Maudhui ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo

mbalimbali yanayomsukuma msanii hadi akatunga kazi fulani ya kifasihi.

**VIPENGELE VYA MAUDHUI**

**1. DHAMIRA**

Hili ni wazo kuu au mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Dhamira ni sehemu tu ya maudhui na aghalabu dhamira kuu ndio hujenga kiini cha kazi ya

fasihi

Dhamira imegawanyika katika makundi mawili ambayo ni:

i. Dhamira ndogondogo
ii. Dhamira kuu

**2. MIGOGORO**

Hii ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi ya fasihi. Migogoro yaweza kuwa ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, na migogoro ya nafsi ambayo hujitokeza katika mitazamo tofauti kulingana na mtiririko wa visa na matukio yaliyopangwa na mwandishi.

**3. UJUMBE**

Mwandishi anapoandika kazi yake huwa na ujumbe ambao hutaka uifikie jamii aliyokusudia. Ujumbe katika kazi ya fasihi ni mafunzo mbalimbali ambayo hupatikana baada ya kuisoma kazi ya fasihi.

**4. MSIMAMO**

Msimamo ni ile hali ya mwandishi kuamua kufuata na kushikilia jambo fulani. Jambo hili huweza kukataliwa na wengi lakini yeye akalishikilia tu. Msimamo ndio huweza kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaoandika kazi kuhusu mazingira yanayofanana.

**5. FALSAFA**

Ni msimamo wa msanii katika maisha juu ya utatuzi wa matatizo katika jamii. Falsafa ya mwandishi inaweza kujulikana kwa kusoma kazi zake zaidi ya moja.

**6. MTAZAMO**

Ni hisia na uelewa wa mwandishi juu ya jambo fulani. Mfano anaweza kutazama jambo fulani kwa mtazamo wa kidini, kisayansi nk

**7. MAFUNZO**

Haya ni mawazo ya kuelimisha yanayopatikana katika dhamira mbalimbali za kazi za fasihi.

**SHAIRI LA KIMAPOKEO:**

1. Nisaidieni jamii, enyi majirani zangu,
   Nanyi wapita njiani, mwilone hali yangu,
   Kumezuka manyumbani, meniruka ndugu zangu,
   Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

2. Sina baba wala mama, sina babu sina nyanya,
Sigambi mie yatima, wandugu watanisonya,
Nanyimwa hata kulima, jamani nini tafanya,
Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

3. Marehemu wangu baba, urithi kanitengea,
Urithi mwingi si haba, ndugu wakajigawia,
Na kwa upanga wa shaba, mbio wakanitimua,
Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

4. Mie sio chokoraa, wala si mwendawazimu,
Sikupenda nikavaa, mavazi ya kuazimu,
Au kujiongelea, pekee kama mzimu,
Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

5. Nala nalala njiani, nishazowea baridi,
Mwanipita maskini, kunitema mumezidi,
Mwanitemea usoni, nyinyi ni ndugu zangu shaidi,
Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

6. Nami vile natamani, niwe na wale wenzangu,
Tupingane darasani, kwa swahili na kizungu,
Nikalie mitihani, nishindane na wenzangu,
Nala nanywa mapipani, hali yangu taabani.

**UHAKIKI WA MAUDHUI:**

**1. DHAMIRA**

Shairi hili linaongelea dhamira mbalimbali ambazo ni:-

**i. Ukombozi wa mwanamke:**

Msanii anaongelea suala la ukombozi wa mwanamke katika nyanja za kiutamaduni na kisiasa. Kwamba wanawake waachane na fikra potofu kwamba hawawezi kushikanyadhifa mbalimbali au kumiliki vitu ambavyo fikra hizi hupelekea umaskini. Anawahimiza kwamba wakati umefika sasa wa

kuachana na tamaduni za kizamani ili wajikomboe kiuchumi, kififikra, kimtazamo pia kielimu, kwani ukimsomesba mwanamke umeelimisha jamii nzima.

**ii. Elimu:**

Msanii anabainisha kuwa ili kujikomboa ni lazima upate/uwe na elimu. Hili jambo lipo katika jamii zetu kwani wanawake wanapopata elimu wanafanya mambo makubwa na wanawazidi hata wanaume. Ndio maana hata katika nchi yetu wapo wanawake wengi walioshika nyadhifa mbalimbali za uongozi.

**iii. Ushirikiano:**

Msanii anasisitiza ushirikiano miongoni mwa wanajamii kwani ndiyo nguzo ya kujikomboa na kujitoa katika mateso. Msanii anasisitiza wanawake waache tabia ya kulumbana kwani watapoteza nguvu, badala yake wao washirikiane. Ndio maana upo umoja wa wanawake katika taasisi mbalimbali za kiserikali. Lengo ni kuwapatia nafasi za kuwaongoza na kuwa wawakilishi wengi.

**iv. Ujasiri:**

Msanii anawasisitiza wanawake wasiwe waoga bali wawe majasiri katika kujikomboa kiuchumi, kiutamaduni, na kisiasa. Ujasiri pekee ndio utakaowasaidia kujikomboa dhidi ya ukandamizaji kwani wanawake wengi wanakuwa hawana sauti mbele ya wanaume. Na hii ilipelekea serikali kuanzisha sheria ya haki sawa dhidi ya wanaume na wanawake kwani wanawake wanaweza kumiliki mali, kuongoza n.k.

**2. UJUMBE**

Ujumbe tunaopata ni kwamba mwanamke anapaswa kujikomboa yeye mwenyewe na hakuna mtu mwingine atakayemsaidia kujikomboa. Hivyo mwanamke hana budi kupambana ili kujikomboa.

**3. FALSAFA**

Msanii anaamini ili kujikomboa ni lazima utie bidii na pia ni lazima mshirikiane ili kujikomboa maana ushirikiano ndio nguzo muhimu katika vita.

**4. MSIMAMO**

Mshairi ana msimamo wa kimapinduzi kwani anataka wanawake wajikomboe kutoka katika ukandamizaji. Pia katika jamii bado kuna wanawake wananyanyaswa kama vile

kukeketwa. Ndio maana serikali imepiga marufuku ukeketaji na ikibainika kuna wanaoendelea kufanya hivyo huchukuliwa hatua kali.

**5 MTAZAMO**

Mtazamo wa msanii ni wa kiyakinifu kwani anawataka wanawake kujipigania wenyewe ili wajikomboe watoke kwenye hali duni na pia wawe na ushirikiano watashinda vita hii kirahisi.

**MASWALI:**

1. Tunga shairi la kisasa

2. Chambua shairi hilo katika vipengele vya maudhui.

1. Kutafsiri lugha ya picha katika ngonjera na kutamba kingonjera na kubusianisha na maisha ya kila siku,

**NGONJERA**

Ngonjera ni aina ya mashairi ya majibizano baina ya pande watu wawili au zaidi. Muundo wa ngonjera ni sawa kabisa na mashairi.

Aghalabu mazungumzo hayo huwa na mijadala ya malumbano yenye kusudio la kutoa ujumbe maalumu kwa hadhira au jamii husika. Msemaji mmoja huuliza swali katika ubeti mmoja na mwingine hutoa jibu katika ubeti unaofuata na majibizano ya hoja kuendelca hivyo hadi kukamilisha mada ya mjadala husika.

Ngonjera, tofauti na nyimbo na mashairi, huwa haziimbwi bali husemwa. Katika ngonjera kunakuwa na majibizano kuhusu mada fulani. Mhusika mmoja hutatizwa na mada hiyo wakati mhusika mwingine hujaribu kumpa ufafanuzi

**NGONJERA:**

**KARIMU:**

Nimepita kila kona, watu wengi wasifia,

Wazee pia vijana, wengi nimewasikia,

Wote wahamasishana, vitendawili sifia,

Vitendawili kutega, faida zake sioni.

**RAHIMU:**

Karimu wewe Karimu, unatania hakika,

Wakubwa nao watoto, wote wanajua fika,

Vitendawili ni joto, la akili kutumika,

Hutufanya kufikiri, jibu tunapotafuta

**KARIMU:**

Nijulisheni kwa mifano, jinsi vilivyo muhimu,

Nitakuunga mkono, ukinijaza elimu,

Vitatu au vitano, vyatosha toa hukumu,

Vitendawili kutega, faida yake ni nini?

RAHIMU:

Kwanza ni kufikirisha, tunapodaiwa jibu,

Pili vinatufundisha, kuyakwepa masahibu,

Mazingira vyahusisha, tuyajue kwa karibu,

Ni nyingi faida zake, vitendawili kutega.

KARIMU:

Nimekutaka nifano, wewe wanipa faida,

Wacha nikupe kibano, uache kupindapinda,

"Chauma bila ya meno", tegua toa faida,

Vitendawili kutega, faida yake siioni,

**RAHIMU:**

Jawabu lake ni moto, twatumia kila siku.

Kulifikiria jibu, akili nimetumia,

Moto vitu waharibu, pasipo meno tumia,

Tahadhari tunapewa, tuutumiapo moto.

**KARIMU:**

"Ala lakini hashibi", jibu na funzo nataka,

Leo ninapiga kambi, uniondolee shaka,

Leo ninapiga kambi, uniondolee shaka,

Sitalitimua vumbi, hadi tupate mwafaka,

Vitendawili kutega, sioni faida yake.

**RAHIMU:**

Ala lakini hashibi, jibu lake ni mauti,

Nami ninapiga kambi, hadi tufike tamati,

Hata tumwombe Yarabi, yatatufika mauti,

Twafundishwa tutambue, kifo kwetu hakikomi.

**KARIMU:**

Leo Karimu nakiri. Rahimu wewe Mwalimu,

Tangu nianze fikiri, nilibaki kulaumu,

Sikutaka kuamini, bila kujua umuhimu,

Vitendawili kutega, faida nimezijua.

**RAHIMU:**

Waungwana karibuni, tutegue na kutega,

Nyumbani pia shuleni, vitendawili kutega,

Mafunzo tuyapateni, uwezo tutaujenga Ni

nyingi faida kwetu, vitendawili kutega.

**MASWALI**

**a) UFAHAMU**

1. Katika ngonjera hii wanaolumbaua ni akina nani?

Jibu:

- Katika ngonjera hii wanaolumbana ni Karimu na Rahimu.

2. Karimu anataka kujua nini?

Jibu:

- Karimu anataka kujua umuhimu wa vitendawili.

3. Ngonjera hii ina beti ngapi?

Jibu:

- Ngonjera hii ina beti kumi.

4. Kutokana na ngonjera faida za vitendawili ni zipi?

Jibu:

- Kutokana na ngonjera hii faida za vitendawili
- Kufikirisha
- Kufundisha
- Kuhusianisha mazingira

5. Kutokana na ngonjera hii, kitendawili "chauma bila meno jibu lake lina faida gani katika maisha ya kila siku?

Jibu:

- Faida ya jibu la kitendawili "chauma bila meno" katika maisha ya kila siku linatufundisha kuwa makini na moto kwani waweza kuleta madhara mfano kuunguza misitu na kuleta jangwa.

6. Dhamira ya ngonjera hii ni ipi?

Jibu:

- Dhamira ya ngonjera hii ni kuelimisha kusisitiza umuhimu wa vitendawili. Watu wajue kuwa vitendawili vinapaswa kupewa kipaumbele kwani vinafikirisha kuelimisha na kuhusianisha vitu katika mazingira tunamoishi vile vile huburudisha.

**b)** MAZOEZI YA LUGHA:

Badilisha kauli halisi kuwa kauli taarifa:

1. Rais alisema, “kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii ili tukuze uchumi wa nchi.”

Jibu:

- Rais alisema kwamba kila Mtanzania afanye kazi kwa bidii ili tukuze uchumi wa nchi.

2. Mama alisema, “Kaeni juu ya jiwe."

Jibu:

- ❖ Mama alisema kwamba tukae juu ya jiwe.

3. Mama alisema, "damu nzito kuliko

maji." Jibu:

- ❖ Mama alisema kwamba damu nzito kuliko maji.

4. "Maziwa yamemwagika" Asha alisema.

Jibu:

- ❖ Asha alisema kuwa maziwa yamemwagika

5. "Funga mlango", baba aliamuru.

Jibu:

- ❖ Baba aliamuru mlango ufungwe.

**Badilisha sentensi zifuatazo ziwe katika wingi:**

1. Mimi ninakula chakula.

Jibu:

- ❖ Sisi tunakula vyakula.

2. Yeye anaimba wimbo mzuri.

Jibu:

- ❖ Wao wanaimba nyimbo nzuri

3. Wewe unajua kucheza vizuri.

Jibu:

- ❖ Ninyi mnajua kucheza vizuri.

4. Shamba limelimwa lote.

Jibu:

- ❖ Mashamba yamelimwa yote.

5. Ukuta umebomoka.

Jibu:

- ❖ Kuta zimebomoka.

6. Mkulima amenunua mbegu na mbolea.

Jibu:

- ❖ Wakulima wamenunua mbegu na mbolea.

7. Yeye ni

mkulima Jibu:

- ❖ Wao ni wakulima.

**g. Kutafsiri lugha ya picha katika vitendawili na kueleza maana zake kwa kuhusianisha na maisha ya kila siku.**

**VITENDAWILI:**

**Vitendawili** ni semi zilizofumbwa ambazo hutolewa kwa hadhira ili zifumbuliwe. Vitendawili hufikirisha na kufanya watu wavihusishe na hali halisi ya maisha na vitu au matukio mbalimbali katika mazingira yao na dunia kwa ujumla.

Vitendawili huwa na sifa ya ufupi wa maelezo ambayo wakati mwingine huweza kuwa neno moja tuu. Vitendawili hujengwa na miigo na mifananisho na mlinganisho ya maana, sauti, rangi, ukubwa, na udogo.

Vitendawili vinaweza kugawanyika kati ya:

i. Vinavyoshughulikia uhalisia
ii. Vinavyoshughulikia mimea
iii. Vinavyoshughulikia wanyama
iv. Vinavyoshughulikia maisha ya nyumbani
v. Vinavyoshughulikia sehemu za mwili
vi. Vinavyoshughulikia vyombo vya jikoni

vii. Vinavyohusu utamaduni wa mzungu nk

Mfano:

i. Popoo mbili zavuka mto.

**Jibu: Macho**

ii. Mnazi wangu uko mlimani lakini nayanywa madafu hapa.

**Jibu: Mvua**

iii. Kuku wangu katagia mibani.

**Jibu: Nanasi**

**FAIDA ZA VITENDAWILI:**

i. Hufundisha watu kuhusu mazingira yao
ii. Huburudisha
iii. Hufikirisha - (huchemsha bongo)

**a) Vitendawili vyenye kufundisha mazingira ya kimaumbile na kitamaduni ni kama vile:**

i. Kuku wangu kutagia mibani (nanasi)

- ❖ Kitendawili hiki kinamfundisha mtoto mimea na kilimo.

ii. Wanangu wawili wanashabihiana (tui la nazi na maziwa)

- ❖ Kitendawili hiki kinamzoesha mtoto kutambua vitu vilivyopo katika maumbile na kuweza kuvifananisha na kuvitofautishia.

**b) Vitendawili vyenye kuonesha matumizi ya picha za uiti, viungo vya mwili, wanyama, na vitu mbalimbali.**

i. Niendako nikirudi humwambia mama mbebe (kitanda)

- ❖ Mama ni mfano wa kitanda. Lazima utake kulala juu ya kitanda. Hivyo ni sawa na kumwambia mama nibcbe

ii. Miche ya shamba letu haihesabiki nywele)

- ❖ Shamba hapa ni kichwa na miche ni nywele

iii. Haitwi, hafukuzwi, hatulii daima yu safari (bahari)

iii. Haitwi, hafukuzwi, hatulii daima yu safari (bahari)

- ❖ Maji ya bahari daima hujaa na kupwa. Hujaa bila kuingizwa baharini. Pia hupwa bila kuambiwa yatoke ufukweni. Muda wote huwa yana mawimbi na ndipo tunaposema yapo safarini.

**MASWALI:**

Tegua vitendawili vifuatavyo:

1. Ukoo wetu hauishiwi safari - **Siafu**
2. Hana adabu wala staha kwa watu - **Utelezi**
3. Nikimwita huniita, nikienda simkuti - **Mwangwi**
4. Ajenga ingawa hana mikono - **Ndege**
5. Anajihami bila silaha - **Kinyonga**
6. Hachagui chifu wala mjumbe - **Utelezi**
7. Fuu funua! fuu funika! **- Kutembea**
8. Hausimiki hausimami - **Mkufu**
9. Damu ya simba hatui nzi-**Moto**
10. Bwana afya wa pori – **Fisi**
11. Bibi hatui mzigo wake – **Konokono**
12. Kilemba chake havui wala haizimishi – **Jogoo**
13. Maji ya kisima hiki hayanyweki – machozi
14. Kombe la Mungu li wazi – **Kisima**
15. Kila nikienda nasikia wifi wifi – **Mbaazi**
16. Pita hapa na mimi nipite kule tukutane kwa mjomba – **Mkanda**
17. Ninapompiga mwanangu watu hucheza **Ngoma**
18. Nina watoto wangu watano kofia zinafanana – **Kucha**
19. Nina rafiki yangu lakini namwogopa – **Kifo**
20. Niliona mkufu njiani lakini sikuweza kunyanyua – **Siafu**
21. Ndani kokoto nje simenti (saruji) – **Pera**
22. Namkata mwanangu nalia mwenyewe **Kitunguu**
23. Mjomba hataki tuonane – **Kisogo**
24. Mama nieleke **- Kitanda**
25. Napigwa faini kosa silijui **– Kujikwaa**
26. Mkutanapo marafiki muachanapo maadui - **Kinyesi**
27. Ubwabwa wa mwana mtamu - **Usingizi**
28. Ukimgusa mwanangu hucheka - **Kwapa**

29. Nyumba yangu ina mlango juu - **Chupa**
30. Nina watoto wangu watatu ukimtoa mmoja kazi haifanyiki - **Mafiga**
31. Popoo mbili zavuka mto - **Macho**
32. Zulia la Mungu - **Ardhi**
33. Uwanja mweupe wachezaji wekundu - **Wali Na Maharage**
34. Utupacho wewe kwake ni dhahabu - **Nzi**
35. Ukiona njigi utadhani njege ukiona njege utadhani njigi - **Maziwa Na Tui La Nazi.**

**h. Kueleza mafunzo yaliyopatikana katika methali na kulinganisha na maisha ya kila siku katika miktadha mbalimbali.**

**METHALI**

Ni usemi mfupi wa mapokeo wenye mpangilio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jamii husika.

Ni kauli fupi yenye pande mbili za fikra ambazo upande wa kwanza huanza upande wa pili kumalizia.

**Mfano:**

Mficha ugonjwa **- kifo humuumbua**

Mcheza kwao - **hutunzwa**

Kila methali huwa na maana au ujumbe.

**Tunaweza kutofautisha kati ya aina mbili kuu za maana.**

**i. Maana ya juu/nje**

Hii ni ile inayopatikana kutokana na kufahamu maneno yaliyotumiwa.

**ii. Maana ya ndani**

Hii ni maana iliyofichwa, ili kuipata maana hii, inabidi kuzielewa tamathali za semi zilizotumwa. Huu ndio msingi wa kupita maana ya kitamathali. Siyo methali zote huwa

na aina hii ya maana, kuna methali ambazo ni sahili tu. Zina maana ya nje/juu tu, mfano: "Kawia ufike, "Haraka haraka haina baraka".

MATUMIZI YA METHALI:

1. Methali huonya/hutahadharisha watu katika jamii dhidi ya maovu, mfano: usipoziba uta utajenga ukuta
2. Methali hutumiwa na waandishi, wazungumzaji na katika kazi mbalimbali za sanaa kama mapambo ya lugha.
3. Hutumika kutoa mawaidha katika jamii, mfano: asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
4. Hutumika kuunganisha jamii pamoja, mfano:Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, Kidole kimoja hakivunji chawa

Kwa ujumla methali hutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu kwa jamii kuhusu maadili yao, imani zao, itikadi zao, historia yao, mtazamo wao nk

Methali ni nyenzo kuu na muhimu ya kuhifadhi sifa za kisimu za lugha tofauti ulimwenguni.

**METHALI NA MAFUNZO YAKE:**

Vita vya panzi furaha ya kunguru

Maana:

- ❖ Ndugu au marafiki wakigombana adui zao hufurahia

Lugha:

- ❖ Lugha iliyotumika ni ya taswira kwani anawakilisha ndugu au marafiki na kunguru anawakilisha maadui.

Mafunzo

- ❖ Ni vema kuwa waangalifu na maadui zetu kwani wanaochochea ugomvi ili wanufaike.

**MASWALI:**

Andika maana na mafunzo yanayopatikana katika methali zifuatazo:

1. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Maana: :

- ❖ Mtu asiyefuata ushauri wa wakuu wake mabaya humpata.

Mafunzo:

- ❖ Ni vyema kufuata ushauri wa watu waliotuzidi umri ili yasije yakatupata mabaya kwani ukubwa dawa.

2. Ganda la muwa la jana chungu kaona kivuno.

Maana:

- ❖ Kitu kisichokuwa na faida kwako chaweza kuwafaa wengine.

Mafunzo:

- ❖ Unachoona kwako hakina thamani, kwa mwenzio kina thamani na chaweza kumfaa kwa matumizi yake.

3. Afadhali dooteni, kama ambari ya kitanda.

Maana

- ❖ Afadhali kibaya kidogo ulichonacho kulikokingi kizuri usichonacho wala huna njia ya kukipata.

Mafunzo

- ❖ Jifunze kujipatia sifa mbaya pia usijikweze usije ukaaibika

4. Avumaye baharini papa kumbe wengine wapo.

Maana:

- ❖ Mtu anaweza kuwa mtenda mabaya lakini kumbe wapo watu wengine watenda mabaya zaidi yake.

Mafimzo:

- ❖ Jiepushe na kujipatia sifa mbaya pia usijikweze usije ukaaibika.

**Andika methali inayofaa kutumika katika sentensi zifuatazo:**

1. Kila mtu niliyekutana naye alijua mimi si mkazi wa pale kijijini.

Jibu:

- Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

2. Ushirikiano ni muhimu katika kufanya kazi.

Jibu:

- ❖ Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

3. Huwezi kupata kila kitu kwa urahisi, ni lazima kufanya kazi kwa bidii.

Jibu:

- ❖ Mtaka cha uvunguni sharti ainame.

4. Huwezi kukosa shilingi elfu kumi ya kunikopa kwani watu wazima hamkosi akiba ndani.

Jibu:

- ❖ Jungu kuu halikosi ukoko.

5. Rafiki wa kweli ni yule anayekuwa nae wakati wa shida.

Jibu:

- ❖ Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

6. Kila kitu huwa kina mwisho wake.

Jibu:

- ❖ Hapana marefu yasiyo na ncha.

7. Nilifanya kazi taratibu na kwa uangalifu hatimaye

nikaikamilisha Jibu:

- ❖ Mwenda pole hajikwai, au Polepole ndio mwendo.

8. Lazima ulie kwa kufukuzwa kazi, hata hivyo hakuna jinsi maana limeshatokea.

Jibu:

- ❖ Maji yakimwagika hayazoleki.

9. Ukijinyoa utajiharibu japo wewe ni kinyozi.

Jibu:

- ❖ Mganga hajigangi.

10. Shughuli unazozifanya sio zako kwanini usitafute shughuli zako mwenyewe.

Jibu:

- ❖ Mtegemea cha nduguye hufa maskini.

Utatumia methali gani kwa watu hawa:

1. Mtu anayejitapa ameshafaulu maishani halafu puude

akafeli Jibu:

- ❖ Aliyeko juu mngoje chini.

2. Mtu asiye msikivu kwa wakubwa.

Jibu:

- ❖ Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

3. M

wizi

Jibu:

- ❖ Za mwizi ni arobaini.

4. Mtu mwenye

pupa Jibu:

❖ Haraka haraka haina baraka

5. Mtu aliyekata tamaa kutokana na dhiki ya

maisha Jibu:

- ❖ Baada ya dhiki faraja

6. Mtu asifiaye jambo

fulani Jibu:

❖ Aisifuye mvua imemnyeshea

7. Mtu ambaye hujui shida

yako Jibu:

- Kitanda usichokilalia hujui kunguni wake.

**i. Kueleza maana za nahau na kutumia mahau mbalimbali katika mazungumzo kwa kuzingatia miktadha mbalimbali.**

**NAHAU:**

Nahau ni semi fupifupi ambazo hutumia lugha/maneno ya kawaida lakini maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyoko kwenye maneno ya awali. Japokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida lakini kauli yake ina undani kiasi kwamba kwa wageni wasiofahamu lugha hiyo hawawezi kuelewa maana.

Mfano wa nahau;

Ana mkono mrefu - **mwizi**

Ana inda**- ana wivu**
Ametutupa mkono - **amefariki**

Nahau kama zilivyo methali zina maana zake pamoja na matumizi yake.

Mfano:

1. Tia kitumbua

mchanga Maana:

- ❖ Kumharibia mtu sifa yake au mambo yake mazuri

Matunzi:

- ❖ Hutumika pale mtu anapomchafulia mwenzake jina lake au mambo yake

2. Kata mzizi wa

fitina Maana: :

- ❖ Kutatua chanzo cha mgogoro au ugomvi na kutokomeza kabisa

Matumizi:

- ❖ Hutumika pale mtu anapotaka kukomesha tatizo au ugomvi.

**Kwa kila kifungu cha maneno andika nahau inayofaa kutumwa badala ya maneno**

**yaliyopigiwa mstari:**

1. Ilikuwa ni safari ya hatari lakini tulifika bila matatizo

Jibu:

- ❖ Salama salimini

2. Maendeleo ya mazao yangu sasa yananipa faraja.

Jibu:

- ❖ Tia moyo

3. Boti ilizama taratibu mwishowe ikazama yote.

Jibu:

- ❖ Zama

4. Dereva wa basi alijitahidi kwa kila njia gari lisianguke.

Jibu:

- ❖ Fanya juu chini

5. Baba aliugua sana lakini kwa sasa afya yake ni nzuri sana.

Jibu:

- ❖ Buheri wa afya

6. Hili banda lilikaribia sana kuangushwa na upepo.

Jibu:

- ❖ Nusurika

**Andika maana za nahau zifuatazo:**

1. Ahadi ni deni - **timiza ahadi yako**
2. Amevaa miwani - **amelewa pombe (chakari)**
3. Chemsha bongo - **fikiri kwa makini**
4. Kuchungulia kaburi **- kunusurika kifo**

5. Fyata mkia – **nyamaza kutamani**
6. Hawapikiki chungu kimoja - **hawapatani kamwe**

7. Kumvika kilemba cha ukoka - **kumsifu mtu kwa unafiki**
8. Kula mlungula - **kula rushwa**
9. Mezea mate - **kutamani**
10. Vunjika moyo **- kata tamaa**
11. Meza maneno - **kutunza siri movoni**
12. Kalia kitako **- kumsengenya mtu**
13. Paka mafuta kwa mgongo wa chupa - **kumsengenya mtu**
14. Mangimeza - **kiongozi anayependa kuamrisha watu**
15. Sina hali - **sijiwezi**

.

# KUONESHA UELEWA WA JAMBO ALILOLISIKILIZA AU KULISOMA

## KUONESHA UELEWA WA JAMBO ALILOLISIKILIZA AU KULISOMA

### kusikiliza na kuonesha uelewa wa jambo alilosikiliza

a. Kusoma hotuba na kubaini maudhui yaliyojitokeza na kuyafafanua kwa usahihi.

**HOTUBA:**

Hotuba ni mazungumzo yanayofanywa na mtu kuhusu suala fulani mbele ya kikundi cha watu. Hotuba inaweza kutolewa na mwanasiasa kwa wananchi, walimu kwa wanafunzi, au mhubiri kwa waumini

Hotuba hujikita kwenye suala kuu fulani, na inaweza kutolewa bila kuandaliwa. Hata hivyo mara nyingi hotuba huandikwa ili kumtayarisha msemaji vilivyo kuhusu lugha atakayoitumia, masuala atakayoyaongelea na mtiririko wa mawazo. Hata hivyo, hotuba nzima huwa haiandikwi, kwani kuna haja ya atakayeitoa kutayarisha vidokezo vya kumwelekeza

**MALENGO YA KUTOLEWA KWA HOTUBA:**

1. Kuelimisha watu, mfano jinsi ya kujikinga na Korona (Covid 19).
2. Kutoa habari, mfano Waziri wa Elimu kueleza mabadiliko ya mtaala wa elimu.
3. Hotuba hupata jina lake kutegemeana na mada yake. Inaweza kuwa hotuba za kiafya, kisiasa, kielimu, kunazingira u.k.

**MUUNDO WA HOTUBA:**

**1. KICHWA CHA HOTUBA**

Kichwa, anwani, hurejelea mada ya hotuba. Pia mada inaweza kutaja hadhira.

Mfano: Hotuba ya Waziri wa Afya kuhusu madhara ya madawa ya kulevya kwa wananchi.

**2. UTANGULIZI**

Kipengele hiki ni kwa ajili ya kuwatambua waliohudhuria katika mkutano. Ni vema kuwataja majina kwa kuanzia na yule wa cheo cha juu hadi wa cheo cha chini.

Pia ni vema kujitambulisha kwa hadhira hasa ikiwa unazungumza na hadhira isiyokujua au wageni.

Mfano:

Waziri wa Kilimo, Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Mbunge wanachama wa kikundi hiki cha mazingira, mabibi na mabwana. Ni matumaini yangu kwamba nyote mu buheri wa afya. Mimi ni mwakilishi wa kikundi cha mazingira na mchana wa leo kuna jambo muhimu ambalo ningependa sote tulifahamu ili tuboreshe mazingira yetu.

**3. KIINI**

Sehemu hii ni mubimu kwani ndiyo sehemu yenye boja na mawazo. Hakikisha kila hoja imeandikwa kwenye aya yake yenye sentensi kuu. Hakikisha kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho na ujumbe unapaswa kuwa katika usemi halisia wala si wa taarifa.

**4. TAMATI**

Tamati inaweza kuwa na mitindo mingi. Unaweza kumalizia kwa usemi, ama unaweza kumalizia kwa kusisitiza hoja muhimu katika hotuba. Ni katika sehemu hii hadhira huweza kupewa changamoto kuhusu suala kuu la hotuba. Mfano, kama hotuba ni ya kutunza mazingira unaweza kuuliza hadhira, Je, tukizidi kuharibu vyanzo vya maji tutapata wapi maji ya kutumia pindi vyanzo vitakapokauka? Pia, kumbuka kuwashukuru watu kwa kuhudhuria. Msimamo wa hotuba usisitizwe hapo.

**MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA HOTUBA**

Uandishi wa hotuba unatakiwa kuzingatia mambo kadhaa. Mambo hayo ni:

i. Kuchagua jambo la kuzungumza
ii. Kujua kusudio la kutoa hotuba kama ni kushawishi, kuelimisha au kuonya
iii. Kubaini aina ya hadhira unyohutubia, mfano, watoto, wazee, wanakijiji, wanafunzi, wasomi,
iv. au waumini wa dini.
v. Kujielimisha kuhusu mada inayohusika. Hii inaweza kuwa ni kwa njia ya kusoma vitabu au kuwauliza wataalamu
vi. Kutumia lugha inayoendana na mada pamoja na hadhira inayohusika

**UTOAJI HOTUBA**

Utoaji wa hotuba ni jambo tofauti sana na utayarishaji. Kuna watu walio na uwezo wa kutayarisha hotuba nzuri lakini hawawezi kuitoa kikamilifu kwa hadhira

**Mambo yawezayo kumwongoza mtoaji hotuba:**

i. Ni muhimu kuzingatia muda wa hotuba ili usiwachoshe wasikilizaji wako. Hotuba isiwe fupi wala isiwe ndefu kupindukia ikiwaudhi wanaosikiliza
ii. Hakikisha umezingatia hadhira katika utayarishaji vilevile, katika utoaji hakikisha hadhira imezingatiwa. Teua lugha inayofaa kwa hadhira yako
iii. Hakikisha unafanya mazoezi ya sauti, lugha na kusimama mbele ya hadhira kabla ya kutoa hotuba
iv. Hakikisha umevaa vizuri na kuonekana nadhifu mbele ya watu
v. Kumbuka unazungumza na hadhira hai hivyo maneno ya hotuba yako lazima yasbawishi
vi. Zingatia kasi inayofaa; usizungumze haraka haraka mno wala polepole sana.

**MFANO WA HOTUBA:**

Hotuba ya Diwani wa Kata kwa wananchi wa kijiji cha Kirishia kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji.

**Kirisha hoyeeee!**

Ndugu mwenyekiti wa kijiji ndugu katibu wa kijiji, ndugu wanakijiji wote mabibi na mabwana. Ninayo furaha kusimama mbele yenu na kuzungumza. Nikiwa kama mwanaharakati wa muda mrefu wa utunzaji wa vyanzo vya maji, leo ninasimama tena mbele yenu kuwaeleza na kuuthibitishia umma huu kuwa maji ni uhai.

Asilimia sabini ya miili yetu ni maji. Hivyo bila maji mwanadamu hawezi kuishi. Sisi ni maji, hivyo lazima tuishi kwa tahadhari kubwa kuyanusuru maji haya yasipotee tukaadhirika.

Laiti kama tungepata nafasi ya kutembelea watu waishio jangwani, tukawaona jinsi wanavyopata shida ya maji tungejifunza kitu. Vipo visa kadhaa vimekuwa vikiripotiwa katika vyombo vya habari kuhusu watu na wanyama waliokufa kwa ukosefu wa maji.

Ukiachilia mbali matumizi yetu, hata viumbe wengine kama mamba samaki, viboko, nao wanategemea maji hava hava ili waendelee kuishi. Ndugu zangu lazima sasa tukubaliane kuwa maji ni uhai.

Ni kipi hakihitaji maji? Hata viwanda vyetu hivi tunavyovitegemea kwa uzalishaji wa bidhaa mbalimbali vinahitaji maji ya kupoozea mitambo.

Wanyama na mimea ni vitu ambavyo tunavitegemea kwa chakula pia vinahitaji maji. Kilimo bila maji ni sawa na sifuri. Bila maji wote tutakwisha na kusahaulika mara moja.

Niwaombe ndugu zangu, tuache mara moja hii tabia iliyozuka hivi karibuni. Tabia ya kunywesha mifugo kwenye vyanzo vya maji pamoja na kukata miti hovyo. Hii itatuletea balaa. Hatukatazi

kukata miti, lakini hakikisha unapokata mti uwe na kibali maalumu, kwani unatakiwa kupanda mti ndipo ukate mti.

Ni matumaini yangu makubwa mtayafanyia kazi yote niliyoyasema. Kimsingi zaidi, tuhakikishe tunaepuka tabia zote ambazo zitatuharibia vyanzo vyetu vya maji.

Mwisho niwashukuru wote mliohudhuria na kunisikiliza, nasema asanteni sana.

**MASWALI**

**A. UFAHAMU:**

1. Hotuba hii inahusu nini?

Jibu:

Hotuba hii inahusu utunzaji wa vyanzo vya maji.

2. Ni watu gani wanaohutubiwa katika hotuba hii?

Jibu

- Ni wanakijiji wa kijiji cha Tirisha.

3. Aliyetoa hotuba ni nani?

Jibu:

- Aliyetoa hotuba hii ni diwani wa kata.

4. Mhutubiaji alitaka tabia gani zikomeshwe?

Jibu:

- Mhutubiaji alitaka tabia za kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji na kukata miti ovyo zikomeshwe.

5. Mtoa hotuba alikuwa akiwasisitiza umuhimu wa nini?

Jibu:

- Mtoa hotuba alikuwa akiwasisitiza umuhimu wa maji.

**B. MSAMIATI:**

Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. H

otuba

Jibu:

- Mbunge alipokuja kijijini kwetu alitoa hotuba nzuri sana na kila mwanakijiji alimsifia

2. M

aji

Jibu:

- Mwalimu alituambia asilimia sabini ya miili yetu ni maji.

3. Mt

ambo

Jibu:

- Serikali imewekeza fedha nyingi katika kujenga mtambo wa kufua umeme.

4. Ja

ngwa

Jibu:

- Mwalimu wa Maarifa ya Jamii alituonesha kwenye ramani nchi zinazokabiliwa na jangwa.

5. K

ibali

jibu.

- Mwalimu alituambia hatuwezi kwenda kwenye ziara ya masomo mpaka tuwe na kibali kutoka kwa Afisa Elimu.

**C. JIBU MASWALI YAFUATAYO:**

1. Nini maana ya hotuba?

Jibu:

- Hotuba ni mazungumzo yanayofanywa na mtu kuhusu suala fulani mbele ya kikundi cha watu. Hotuba inaweza kutolewa na mbunge kwa wapiga kura wake, walimu kwa wanafunzi

2. Kwenye kipengele cha utangulizi katika hotuba huzungumza juu ya nini?

Jibu:

- ❖ Kwenye kipengele cha utangulizi ni kwa ajili ya kuwatambua waliohudhuria katika mkutano na pia kujitambulisha kwa hadhira.

3. Taja mambo matatu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba.

Jibu:

i. Kuchagua jambo la kuzungumza.
ii. Kubaini aina ya hadhira unayoizungumzia
iii. Kutumia lugha inayoendana na mada pamoja na hadhira husika.

**D. MAZOEZI YA LUGHA**

**Taja neno lililopigiwa mstari lipo katika kauli gani:**

1. Kila mwalimu atajengewa nyumba ya kuishi.

Jibu:

- ❖ Kauli ya kutendewa

2. Mwizi aliyekamatwa alipelekwa kwenye kituo cha Polisi.

Jibu:

- ❖ Kauli ya kutendewa

3. Watoto hawa wanaimba vizuri.

Jibu:

- ❖ Kauli ya kutenda

4. Asha na Ali wanagombana kila siku.

JIBU

- ❖ Kauli ya kutendana

5. Chakula chetu kililika kwa sababu kilitayarishwa vizuri

Jibu:

- ❖ Kauli ya kutendeka

**b. Kusikiliza hotuba na kubainisha mambo muhimu vanavotokana na hotuba na kuvahusianisha na maisha ya kila siku.**

**HOTUBA YA MHESHIMIWA WAZIRI WA AFYA KWA WANANCHI:**

Ndugu wananchi, ninayo furaha kupata nafasi ya kuzungumza nanyi kupitia vyombo vya habari, juu ya ugonjwa wa Korona.

Ndugu wananchi, mwezi Februari mwaka jana, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza mlipuko wa ugonjwa wa Korona. Pia, lilisema upo uwezekano mkubwa wa ugonjwa huo kuenea duniani kote. Baada ya muda mfupi tu, matukio ya ugonjwa huo yalianza kuripotiwa sehemu mbalimbali duniani.

Baada ya miezi minne, ugonjwa huu ulianza kuripotiwa Afrika Mashariki. Matukio yalianza kuripotiwa nchini Kenya, Burundi, Rwanda, Uganda na Tanzania.

Ndugu wananchi, virusi vya korona ni virusi ambayo hupatikana miongoni mwa baadhi ya wanyama na vinaweza kusababisha ugonjwa kwa wanyama na binadamu. Kwa binadamu, virusi hivi hushambulia mapafu na mgonjwa hushindwa kupumua vizuri.

Ndugu wananchi, dalili za ugonjwa huu wa Korona ni boma kali kichwa kuuma, mafua, kikohozi pamoja na kujisikia uchovu. Dalili hizi huanza polepole. Watu wengine wanaweza kuwa na maambukizi lakini hawaoneshi dalili zozote. Ni kama mtu mmoja kati ya watu kumi wanaopata korona ndio hudhohofika.

Ndugu wananchi, mtu yeyote anayekumbana na virusi vinavyosababisha Korona yuko hatarini. Hata hivyo wazee na wenye matatizo ya kiafya, mfano watu wenye shinikizo la damu, saratani, ndio wapo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya ugonjwa huu.

Ndugu wananchi, ugonjwa huu unaweza kusambaa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine wakati wa kupiga chafya au kukohoa. Pia, wakati mtu anapogusa vitu au sehemu yenye virusi na kujigusa puani, mdomoni na machoni.

Ndugu wananchi, ili kuepuka kuambukizwa virusi hivi, epuka kukaribiana, kupeana mikony, epuka mikusanyiko isiyo ya lazima, na safari zisizo za lazima.

Ndugu wananchi, hatua stahiki za usafi katika kujikinga na ugonjwa huu ni kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kutumia vitakasa mikono mara kwa mara hasa baada ya kuwa mahali pa umma. Epuka kugusa macho, pua na mdomo kwa mikono isiyooshwa.

Ndugu wananchi, ikiwa unahisi una dalili za Korona, jitenge na wenzako, kisha piga simu zetu tulizotoa namba, wahudumu wa afya watakuja kukufuata na kukupeleka karantini.

Ndugu wananchi, tunawashauri kutumia tangawizi na malimao kwa wingi, kwani vitamin nyingi inayohusika na kupambana na virusi vya magonjwa mbalimbali vipo.

kwenye tangawizi na malimao, vilevile vaa barakoa unapokuwa kwenye mikusanyiko ya watu mfano kwenye magari ya umma, kituo cha afya, sokoni n.k.

Ndugu wananchi, ni matarajio yangu kwamba kila mtu atachukua tahadhari ili kujiepusha na maambukizi ya virusi vya Korona. Kila mtu akichukua tahadhari tutaishinda Korona.

Asanteni sana.

**MASWALI**

**A UFAHAMU:**

1. Hotuba hii ameitoa nani na kwenda kwa nani?

Jibu:

- ❖ Hotuba hii ameitoa Mheshimiwa Waziri wa Afya kwenda kwa wananchi.

2. Hotuba inahusu nini?

Jibu:

- ❖ Hotuba inahusu ugonjwa wa korona.

3. Watu gani walitangaza habari za ugonjwa huu kabla ya kusambaa na kufikia Afrika?

Jibu:

- ❖ Waliotangaza ni Shirika la Afya Duniani (WHO).

4. Ni kundi gani la watu walio katika hatari ya kuambukizwa virusi vya korona?

Jibu:

- ❖ Kundi lililopo katika hatari ya kuambukizwa virusi hivi ni wazee pamoja na watu wenye matatizo ya kiafya, mfano shinikizo la damu, saratani n.k.

5. Dalili za maambukizi ya virusi vya korona ni zipi?

Jibu:

❖ Dalili zake ni:

  - Homa kali
  - Kichwa kuuma
  - Kushindwa kupumua
  - Kujisikia uchovu

6. Kanuni za usafi katika kujikinga na ugonjwa huu ni zipi?

Jibu:

❖ Kanuni za usafi za kujikinga na ugonjwa huu ni:

  - Kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.
  - Kutumia vitakasa mikono hasa unapotoka kwenye mkusanyiko wa watu.
  - Kufunika pua unapopiga chafya.

**B. MAZOEZI YA LUGHA**

Andika wingi wa maneno haya:

1. Waziri
2. Kiongozi
3. Mtu
4. Kituo
5. Jicho

**Majibu:**

1. Mawaziri
2. Viongozi
3. Watu
4. Vituo
5. Macho

Badili sentensi kuwa katika umoia:

1. Mbuzi hawana

chakula Jibu:

- Mbuzi hana chakula

2. Nyufa hizi zitadondosha kuta.

Jibu:

❖ Ufa huu utadondosha ukuta

3. Ukiona vyaelea

vimeundwa Jibu:

❖ Ukiona chaelea kimeundwa

4. Madhumuni yenu ya kuja hapa ni nini?

Jibu:

❖ Dhumuni lako la kuja hapa ni nini?

**c. Kufupisha habari/hadithi alivoisoma kwa kutumia maneno yake na kubainisha mawazo yote ya msingi ya mwandishi na kuyaelezea kwa usahihi.**

Habari ni mawasiliano ya maarifa kuhusu matukio ambayo huwasilishwa kwa intu/watu kwa maneno ya kinywa, kwa maandishi kama vile magazeti, kwa matangazo ya masafa marefu kama vile redio au runinga, na kwa intaneti.

Ufupisho wa habari ni kuelezea upya jambo kwa maneno inachache zaidi bila kupoteza maana ya msingi. Kwa kawaida idadi ya maneno inatakiwa kuwa theluthi ya Habari ya awali. Uwezo wa kufupisha unatumika kama kigezo kimojawapo cha kupima uelewa wa mwanafunzi.

**HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUANDIKA UFUPISHO**

Ili ufupisho uwe mzuri hatua zifuatazo hazina budi kufuatwa:

i. Kuisoma na kuisikiliza habari kwa makini ili kueleweka vizuri.
ii. Kutambua na kubaini mawazo makuu yanayojitokeza katika kila aya.
iii. Kuyaunganisha mawazo makuu na kuandika au kuelezea ufupisho wa habari hiyo kwa maneno yako mwenyewe bila kupotosha maana ya habari ya kwanza.
iv. Kuhesabu idadi ya maneno ya ufupisho ili kuyapunguza ikiwa yanazidi idadi inayotakiwa.
v. Pitia tena habari ya mwanzo na pitia tena ufupisho ili kujiridhisha kuwa hujaacha

taarifa yoyote ya muhimu

**UMUHIMU WA UFUPISHO**

i. Ufupisho humzoesha mwanafunzi kufikiria waziwazi, kwani mazoezi hayo humtaka mwanafunzi asome kwa uangalifu ili aone habari muhimu.
ii. Ufupisho humfanya mwanafunzi aeleze kwa ufupi, usahihi na atumie lugha ya mkato.
iii. Ufupisho humpa mwanafunzi mazoezi ya kupanga mawazo yake kwa uangalifu na katika sentensi zilizonyooka. Katika kufupisha buanza na vifungu vya maneno, kisha sentensi moja kabla ya kuelekezwa kuchambua habari ndefu.

**MATLIMIZLYALUE PISHO**

i. Hutumika wakati wa kutayarisha ripoti na kumbukumbu za mikutano
ii. Husaidia wakati wa kuandaa hoja kutokana na mihadhara au hotuba
iii. Hutumika katika kuandaa shajara au kumbukumbu za kila siku
iv. Husaidia katika ubariri wa habari
v. Husaidia kuokoa gharama basa katika uandishi wa simu ya maandishi

**Soma kifungu cha habari kisha andika ufupisho:**

**PANYA MTU**

Palikuwepo na familia moja iitwayo familia ya Bwana Suka, aliyekuwa na mke na binti zake watatu. Mke wa Suka aliitwa Sara. Sara alikuwa hodari kwa kupika kitoweo kilichokuwa maridadi na kitamu sana.

Suka, baba wa watoto alitamani kula kitoweo hicho hata kabla ya chakula cha jioni. Katika harakati za kupakua hata kabla ya wakati kuwasili, mchana alisubiri wanae waende shuleni na mkewe aende shambani.

Alianza kuita, kila jina la mtu aliyeishi pale ili kuhakikisha kwamba wote wametoweka ili aingie ndani aibe kitoweo kilichoachwa kwa ajili ya kutumiwa katika chakula cha jioni.

Mke wa Suka kila wakati anaporudi nyumbani hukuta kitoweo kimeliwa. Na hil humlazimu kuandaa kitoweo kingine japokuwa anakuwa amechoka kwa shughuli za shamba.

Panya aliyekula kitoweo alikuwa ana nguvu za kunyanyua hata mfuniko kutoka kwenye sufuria. Familia ya Mzee Suka ilishangazwa na panya huyu alivyokuwa na nguvu tofauti na panya wengine,

Siku moja binti mkubwa aliwaambia wanafamilia kwamba, "Mimi panya huyu nitamkamata. Lakini sitasema ni lini wala kwa wakati gani nitakapofanya hili jambo, kwani panya huyu ametega masikio yake na amepanua macho yake kusikia na kuona tunayoyapanga."

Suka alimshukuru binti yake kwa hatua hiyo. Suka alifanya hivyo ili asijulikane kwani akijulikana itakuwa ni aibu kubwa mno.

Usiku mmoja binti yake Suka alitega mtego karibu na sufuria iliyokuwa na kitoweo maridadi. Mtego huu ukamsubiri panya mtu anayewakera watu. Manane ya usiku panya mtu aliwasili na alikuwa si mwingine bali ni Mzee Suka. Kwa bahati mbaya Mzee Suka alikuwa uchi wa mnyama Hivyo alipochuchumaa karibu na mtego alibanwa sehemu zake za siri. Mzee Suka alihisi maumivu makali. Mzee mwizi alipiga kelele watu wa nyumbani kwake wakakurupuka kutoka usingizini kuona ni kitu gani kilichompata baba yao. Waliona damu zikitiririka na mtego ukining'inia kwenye sehemu zake za siri.

Familia ya mzee huyu ilishangazwa, wakamuokoa. Lakini kila mtoto aliyetoka usingizini wimbo ulikuwa "panya mtu panya mtu."

**MASWALI**

Fupisha habari uliyoisema:

**PANYA MTU**

Familia ya Bwana Suka ilikuwa ina mama anayejua kupika kitoweo kitamu. Pakawa na panya mwenye nguvu kama za mtu. Huinua mfuniko wa sufuria na kuurudisha

Watu walishangazwa na panya huyo. Mtoto wa Suka aliahidi kumkamata panya huyo na hakuwaambia familia siku wala saa atakapofanya jambo hilo. Baba yake alimshukuru kwani hakutaka kujulikana kama yeye ni mwizi.

Usiku mmoja mtego uliwekwa karibu na sufuria lenye kitoweo. Suka alipocliuchumaa ili aibe kitoweo, mtego ulibana sehemu zake za siri. Alitoa kelele watu wa nyumbani kwake wakaamka na kumnusuru. Lakini walishangaa sana na asubuhi wimbo ulikuwa ni panya mtu! panya mtu!

**MAZOEZI YA LUGHA:**

Jaza nafasi wazi kwa kutumia maneno hata au tangu:

1. Siondoki hapa____________akija polisi

Jibu:

- ❖ Siondoki hapa hata akija polisi.

2. Nimekusubiri________________asubuhi.

Jibu:

- ❖ Nimekusubiri tangu asubuhi.

3. Sijaondoka hapa______________uondoke.

Jibu:

- ❖ Sijaondoka hapa tangu uondoke.

4. Dawa hii______________watoto wadogo wanaweza kuitumia.

Jibu:

- ❖ Dawa hii hata watoto wadogo wanaweza kuitumia.

5. Sijawahi kutoroka shule______________siku moja.

Jibu:

- ❖ Sijawahi kutoroka shule hata siku moja.

**Jaza nafasi wazi kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:**

1. Huwezi kufaulu mtihani huu_________________ hutakuwa mwangalifu.

   A. Japo
   B. Isipokuwa
   C. Kama
   D. Ingawaje
   E. Hata

2. Ipi ni ngeli ya neno chungwa?________________

   A. A-WA
   B. I-ZI
   C. LI-YA
   D. U - YA

E. I - TA

3. Watoto wale wanapendana sana. Sentensi hii ipo katika kauli ipi?

A. Kutenda
B. Kutendana
C. Kutendeana
D. Kutendwa
E. Kutendewa

4. Humo_______________alimopita mwanasiasa maarufu wakati wa kuomba kura.

A. Ndipo
B. Ndio
C. Ndimo
D. Ndiko
E. Ndiko hapa

5. Wewe ni kijana mdogo. Neno wewe lipo katika nafsi gani?

A. Nafsi ya pili
B. Nafsi ya kwanza
C. Nafsi ya wingi

**Majibu:**

| **1.** | **2.** | **3.** | **4.** | **5.** |
|---|---|---|---|---|
| **C** | **C** | **B** | **C** | **A** |

**Kusoma kwa ufasaha na kuonesha uelewa wa matini aliyoisoma.**

**a) Kusoma matini teule kwa kuzingatia alama zote za uandishi na kueleza umuhimu wa matini hizo.**

**Matini** ni andiko au chapisho linalohusu maudhui zaidi kuliko fani. Kutokana na maana hii tunaweza kusema si matini zote huzingatia zaidi kipengele cha fani na kuacha maudhui. Zipo ambazo huweka usawa katika vipengele hivyo. Matini kama zile za kisiasa na zile za kisayansi, zinahusisha kipengele cha maudhui zaidi kuliko fani.

Matini ni wazo au mfululizo wa mawazo ambao unajitosheleza kimaana. Matini yaweza kuwa neno moja, kirai, kishazi, sentensi, aya au kifungu cha habari ambacho kipajitosheleza kimaana chenye ujumbe au wazo linalojitosheleza.

**Soma matini teule ifuatayo kwa kuzingatia alama zote za uandishi kisha jibu maswali yanayofuata:**

Maji ni moja kati ya vitu muhimu sana vinavyotuwezesha kuishi. Vitu vingine ni hewa na chakula. Hewa ndiyo ya kupewa kipaumbele kwani binadamu au mnyama akikosa hewa kwa dakika chache hufa.

Kusingelikua na maji, maisha ya binadamu na viumbe wengine yasingeliwezekana. Maji yanatamalaki maisha ya viumbe hai kwa kinsi kikubwa sana. Baadhi ya viumbe maskani yao ni kwenye maji, mfano samaki, mamba na nyangumi.

Binadamu hutumia maji kwa shughuli mbalimbali. Hutumia maji kwa kunywa, kuogea, kupikia, kuoshea vyombo na shughuli nyingine ndogondogo. Kuna sehemu nyingine watu hutumia maji kumwagilia bustani za mboga.

Kilimo cha umwagiliaji kinafaa kwani mkulima anakuwa na uhakika wa kuvuna wakati wote.

Maji ya mvua yanatuwezesha kulima na kupanda mazao ya chakula na biashara. Ingawaje hapa kwetu Tanzania kuna sehemu ambazo wakulima hutegemea kilimo cha mvua

Bila maji hakuna uhai kwa sababu maji ni uhai. Uharibifu unaofanywa na binadamu unasababisha kuwepo kwa upungufu mkubwa wa maji. Binadamu ameharibu mazingira kwa njia nyingi sana. Baadhi ya njia hizo ni kulima kandokando ya vyanzo vya maji, ufugaji huria, ukataji misitu hovyo, kuchoma misitu ni mambo yanayochangia katika kuharibu mazingira na kupelekea upungufu wa maji.

Maji kwa upande mwingine yana hasara zake. Maji yanapokuwa mengi kupita kiasi, mathalani mvua kubwa sana zinaponyesha mfululizo, mafuriko hutokea. Watu huweza kupoteza maisha kwa kufa maji na mazao huharibika mashambani. Hata hivyo mafuriko hutokea kwa nadra sana.

**A. UFAHAMU**

Jibu maswali yafuatayo:

1. Ni kitu gani muhimu cha kwanza kinachomwezesha binadamu kuishi?

Jibu

- Kitu muhimu cha kwanza kinachomwezesha binadamu kuishi ni hewa.

2. Taja faida za maji.

Jibu:

- Faida za maji hutumika kwenye kilimo (kustawisha mimca), kufulia, kupikia, kuoshea vyombo, kunywa nk

3. Binadamu anawezaje kusababisha upungufu wa maji?

Jibu:

- Binadamu anaweza kusababisha upungufu wa maji kwa kulima kandokando ya vyanzo vya maji, kukata mito hovyo, kuchoma misitu, ufugaji huria n.k.

4. Kwa nini kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika zaidi kuliko kile cha mvua?

Jibu:

- Kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika zaidi kuliko kile cha mvua kwa sababu mvua zinaweza zikakatika au zikachelewa kunyesha na mazao yaknkauka lakini ukimwagilia maji mazao hayakauki.

5. Zipi ni hasara za maji?

Jibu:

- Maji yanapokuwa mengi kupita kiasi huweza kuleta mafuriko na kupelekea watu kufa maji na mazao kuharibika mashambani.

**B. MAZOEZI YA LUGHA**

Andika visawe vya maneno yafuatayo:

1. Chubua **- chuna**
2. Herufi - **hati**

3. Rushwa - **hongo**
4. Shika - **kamata**

5. Mlolongo - **foleni**
6. Kivumbi **- fujo**
7. Moto kaa - **gari**
8. Nakshi - **urembo**
9. Spika - **kipaza sauti**
10. Korongo - **gema**
11. Kileo - **pombe**
12. Kichaa - m**wendawazimu**
13. Ndoa - **chuo**
14. Ukwasi - **utajiri**
15. Vunja - **pasua**
16. Waza - **fikiri**
17. Upara - **kidazi**
18. Ukuta - **kiambaza**
19. Ugonjwa - **maradhi**
20. Wivu - **husuda**
21. Masalia **- mabaki**
22. Kandanda - **soka**
23. Idhini - **ruhusa**
24. Jogoo - **Jimbi**
25. Saka - **winda**
26. Sala - **dua**
27. Lisani - **ulimi**
28. Fukara - **maskini**
29. Azma - **makusudio**

.

**b) Kusoma, kuchanganua na kueleza mawazo yote ya msingi katika matini teule za kisiasa, kiuchumi na kijamii.**

**Soma matini ifuatayo kisha jibu maswali:**

Ulinzi huleta amani, utulivu na usalama wa maisha ya wananchi na rasilimali zao. Msingi wa ulinzi na usalama ni kujikinga na kujilinda. Jukumu la ulinzi na usalama wa nchi yetu ni la kila mwanajamii.

Jamii isipoimarisha ulinzi wa nchi yao, hali ya amani na usalama inaweza kutoweka. Kutoweka kwa hali ya usalama na amani husababishwa na kuwepo kwa matukio ya kiuhalifu au vita katika maeneo tunayoishi. Vita inaweza kuwa kati ya wakulima na wafugaji.

Kila mwananchi hana budi kushiriki katika suala la ulinzi na usalama wa rasilimali za nchi kama vile misitu, wanyama pori, nk. Pia mali zao wenyewe. Wananchi wanatakiwa kushiriki katika suala la ulinzi na usalama wa nchi yao kwa njia mbalimbali. Miongoni mwa njia hizo ni kuwafichua wahalifu waliopo katika maeneo wanayoishi. Hapa hutakiwa kutoa taarifa kwa viongozi pamoja na vituo vya polisi wanapowaona watu wanaowatilia mashaka katika maeneo yao wanakoishi. Vilevile kuhudhuria mikutano inayohusu namna ya maisha ya watu kwa ujumla.

Kushiriki katika ujenzi wa vituo vya polisi pamoja na kuchangia vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi. Vifaa hivyo ni kama pikipiki baiskeli na simu kwa ajili ya mawasiliano. Wananchi wenye uwezo au makampuni mbalimbali wanaweza kutoa misaada hiyo ili kuimarisha ulinzi na usalama.

**A. UFAHAMU:**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Unafikiri kichwa cha habari hii kinaweza kuwa kipi?

Jibu:

- Kichwa cha habari hii kinaweza kuwa Ulinzi Na Usalama wa Watu Na Rasilimali zao.

2. Mwandishi anasema ulinzi huleta nini?

Jibu:

- Mwandishi anasema ulinzi huleta amani, utulivu na usalama wa wananchi na rasilimali zao.

3. Jukumu la ulinzi na usalama ni la nani?

Jibu:

- Jukumu la ulinzi na usalama ni jukumu la kila mwanajamii.

4. Kutoweka kwa hali ya amani na usalama husababishwa na nini?

Jibu:

- Kutoweka kwa hali ya amani na usalama husababishwa na matukio ya kiuhalifu au vita katika maeneo tunayoishi.

5. Ni jukumu la nani kufichua wahalifu waliomo katika maeneo tunamoishi?

Jibu

- Ni jukumu la kila mwanajamii kufichua wahalifu waliomo katika maeneo tunamoishi.

**B. MSAMIATI**

**1. Ulinzi**

i. Kazi ya kulinda kama vile benki au nchi
ii. Namna ya kulinda (ulindaji)

Sentensi:

- Kazi mojawapo ya jeshi la polisi ni kulinda watu na mali zao.

**2. Amani:**

- Hali salama isiyokuwa na ghasia au fujo

au vita. Sentensi:

- Rais wetu alituambia; kila mtu ailinde Amani ya nchi hii.

**3. Rasilimali**

- Jumla ya mali alizonazo mtu, shirika au nchi.

Sentensi:

Nchi yetu ina rasilimali nyingi sana ikiwemo misitu, bahari, milima, mbuga za wanyama, na madini.

**4. Halifu**

- tenda knyume cha sheria
- vunja sheria
- kataa kutii

Sentensi:

- Serikali imewataka wananchi kutoa taarifa kituo cha polisi pale wanapobaini muhalifu

katika eneo lao.

**C. MAZOEZI YA LUGHA:**

Badili sentensi zifuatazo kuwa amri:

1. Tafadhali, naomba kitabu chako.

Jibu:

- ❖ Nipe kitabu chako

2. Unaweza kupiga

mpira Jibu:

- ❖ Piga mpira

3. Mnaombwa mfagie haraka.

Jibu:

- ❖ Fagieni haraka

4. Naomba ukae

kimya Jibu:

- ❖ Kaa kimya

5. Unashauriwa uondoke

haraka Jibu:

- ❖ Ondoka haraka

**Toa maana ya nahau zifuatazo:**

1. Andika meza
2. Chungulia kaburi
3. Kata maini
4. Kula fadhili
5. Kuwa kibunye
6. Kwepa mishale
7. Piga chenga
8. Vuta Kamba
9. Shika mkia

10. Pokewa kwa mikono miwili

**Majibu:**

1. Weka chakula mezani
2. Ugua sana hata kukaribia kufa
3. Umiza
4. Tendewa hisani
5. Kosa meno
6. Epuka balaa
7. Kwepa jambo au mtu
8. Kufa/fariki
9. Kuwa wa mwisho
10. Karibishwa kwa wema

**c) Kusoma matini teule za kisiasa, kiuchumi na kijamii kubaini maneno mapya na kuyatumia katika miktadha mbalimbali.**

**MANENO MAPYA:**

Mabadiliko mengi yanatokea kila siku katika nyanja mbalimbali za kimaisha kama kiuchumi, kisiasa, sayansi na teknolojia. Watu buhitaji kuwasiliana.

Lugha huhitaji kuunda maneno mapya ili kuwasilisha dhana mpya zilizoibuka mtapo maneno kama kompyuta, tarakilishi, udukuzi yameundwa ili kuwasilisha dhana za kiteknolojia kwa Kiswahili.

Mabadiliko ya kimaendeleo yanafanya lugha ihitaji maneno ya kuyafikisha na kutumiwa na jamii ili kukidhi mahitaji hayo.

Maneno hayo yanaweza kuwa katika fani mbalimbali kama vile sayansi na teknolojia, siasa, utamaduni na uchumi kulingana na mkondo wa maendeleo

**Soma hii habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata:**

Tangu nchi yetu ipate uhuru tumeanzisha viwanda vingi. Kuanzishwa kwa viwanda hivyo kulikuwa na lengo la kuimarisha uchumi na kuwapa wananchi ajira. Baada ya uhuru viwanda vidogo na vikubwa vimekuwa vikijengwa katika mikoa mbalimbali nchini. Viwanda hivyo vilimilikiwa na serikali na vilijulikana kuwa ni mali ya umma.

Miaka ya liivi karibuni viwanda ambavyo vimeshindwa kujiendesha kwa ufanisi vimebinafsishwa. Serikali inaruhusu makampuni ya ndani na nje ya nchi kuanzisha viwanda hapa nchini. Watu binafsi pia wenye uwezo wanaruhusiwa kuanzisha viwanda hapa nchini.

Humu nchini vipo viwanda vinavyozalishia mafuta ya kupikia yanayotokana na mbegu, mfano, mafuta ya alizeti. Mafuta haya yanazalishwa kwa wingi katika mikoa ya Dodoma na Singida, kwani mikoa hiyo hulima alizeti kwa wingi.

Pia vipo viwanda vinavyotengeneza vinywaji baridi kama vile soda, juisi (shurubati) na maji Na viwanda vingine hutengeneza vinywaji vikali kama bia na konyagi. Vipo viwanda vya pembejeo za kilimo, vifaa vya majumbani na viwanda vingine vingi.

Kabla kiwanda hakijaanzishwa, ni lazima wataalamu wa mambo ya viwanda wafanye utafiti wa kutosha kuhusu kuanzishwa kwa kiwanda hicho. Ni lazima wajue kama kiwanda kitakapojengwa patakidhi masharti muhimu ya kuanzishwa kwa kiwanda hicho. Mfano, hakitawabugudhi wakazi waliopo jirani na kiwanda au kama hakitaharibu mazingira. Wataalamu hao ni lazima wajue pia malighafi zitatoka wapi na zitafikaje kiwandani na ni wapi bidhaa zitakapotengenezwa zitauzwa. Kiwanda kikianzishwa bila kufanyiwa utafiti wowote kinaweza kufilisika haraka na kufungwa au kuendeshwa kwa gharama kubwa

Viwanda vinapaswa kuinua uchumi wa nchi kwa kutoa ajira kwa wananchi na pia kulipa kodi kwa serikali. Kodi hiyo huiwezesha serikali kuhudumia hospitali, shule, miundombinu, na huduma nyingine za jamii.

Viwanda vingi vilivyomo nchini vimejengwa kwa kuzingatia masharti muhimu ya ujenzi wa viwanda. Mfano, viwanda vya kusindika minofu ya samaki vipo Mwanza kwa sababu kuna ziwa Victoria lenye samaki wakubwa na wenye minofu. Na pia kuna barabara, uwanja wa ndege, na reli kwa ajili ya kusafirishia bidhaa ndani na nje ya nchi.

**A. MSAMIATI:**

Toa maana ya misamiati ifuatayo na kisha tunga sentensi:

**1. Kiwanda:**

- ❖ Mahali panapotengenezwa bidhaa au vifaa
- ❖ Mahali mafundi wanapofanyia kazi zao

Sentensi:

- Baba yangu anafanya kazi kwenye kiwanda cha kutengeneza saruji.

**2. Utafiti:**

- Uchunguzi wa kisayansi au kitaaluma ambao unalenga kugundua, kuvumbua, kufasiri, kuchanganua au utumiaji wa maarifa mapya, nadharia au kanuni fulani

Sentensi:

- Mwalimu alitupa kazi mradi ya kufanya utafiti juu ya wadudu wanaoshambulia migomba.

**3. Uchumi**

- Mali iliyopatikana kutokana na mali za nchi au watu
- Taaluma ya mapato na matumizi ya watu
- Mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi

Sentensi:

- Dada yangu alipomaliza elimu ya sekondari alichaguliwa kujiunga na chuo cha uchumi.

**B. UFAHAMU**

1. Kiwanda ni nini?

Jibu:

- Kiwanda ni mahali panapotengenezwa bidhaa au vifaa.

2. Kwa nini kiwanda cha mvinyo kimejengwa Dodoma na sio Arusha?

Jibu:

- Kiwanda cha mvinyo kimejengwa Dodoma kwa sababu ndipo kwenye bidhaa ya kuzalisha bidhaa hiyo. Dodoma huzalisha zabibu kwa wingi.

3. Taja mambo muhimu ya kufanya kabla ya kuanzishwa kwa kiwanda.

Jibu:

- Mambo muhimu ya kufanya kabla ya kuanzishwa kwa kiwanda ni kuangalia:-

i. Upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya kutengenezea bidhaa
ii. Usafirishaji wa malighafi pamoja na bidhaa zitakazotengenezwa
iii. Kutokuwabugudhi wakati wa maeneo jirani na kiwanda
iv. Kama hakitaharibu mazingira

4. Kodi inayotokana na viwanda ina faida gani kwa wananchi?

Jibu:

- ❖ Kodi inayotokana na viwanda huwanufaisha wananchi kwa kupata huduma kama hospitali ya matibabu, miundombinu bora na shule

**C MAZOEZI YA LUGHA**

**Kamilisha methali zifuatazo**

1 mjukuu

Jibu:

- ❖ Majuto ni mjukuu

2. Maji

yakimwagika Jibu:

- ❖ Maji yakimwagika hayazoleki

3. Hakuna

masika Jibu:

- ❖ Hakuna masika yasiyokuwa na mbu.

4. Mali bila

daftari Jibu:

- ❖ Mali bila daftari hupotea bila habari.

6.____________________hakuna wajenzi

Jibu:

- ❖ Penye miti hakuna wajenzi.

6. Heri kenda

shika Jibu:

- Heri kenda shika kuliko kumi nenda rudi.

7. Vita ya

panga Jibu:

- ❖ Vita wa panga bawiamuliwi kwa fimbo

8. Zimwi likujualo____________________

Jibu:

- ❖ Zimwi likujualo halikuli likakwisha.

9______________agana na nyonga.

Jibu:

- ❖ Ukitaka kuruka agana na nyonga.

10. Udongo

upate Jibu:

- ❖ Udongo upate ungali maji.

11. ______________njaa mwana malegeza

Jibu:

- ❖ Shibe mwana malevya njaa mwana malegeza.

**D. Kubaini maudhui yaliyomo katika hadithi na kuelezea tabia zote za kila mhusika na kuhusianisha na mazingira ya kila siku.**

Hadithi ni masimulizi ambayo yanatumia lugha ya nathari na mtiririko wake huwa ni mwepesi au sahili. Urefu wa hadithi hutofautiana kutoka tanzu au kipera kimoja hadi

kingine. Kuna baadhi za kubuni na hadithi za kihistoria.

**MAUDHUI:**

Haya ni yaliyomo au ni jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi. Maudhui huibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira au wazo kuu la kazi ya fasihi. Kwa ufupi

dhamira hujitokeza kama sehemu ya maudhui. Katika kusoma na kuchambua maudhui katika hadithi fupi,

msomaji achunguze lengo kuu na ujumbe wa mwandishi. Msomaji anaweza kuelekezwa kwenye lengo kuu au dhamira ya hadithi na kichwa cha hadithi yenyewe kisha msomaji atafute na kubainisha msimamo wa mwandishi pamoja na mwelekeo wake wa kimawazo na kifalsafa.

**WAHUSIKA**

Wahusika katika kazi yoyote ya sanaa itumiayo lugha ni watu, wanyama ama vitu. Wahusika husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Wahusika katika hadithi huwa ni binadamu na mazimwi ama binadamu hata miti. Huwezekana pia wahusika wakawa binadamu na viumbe visivyokuwa hai kama vile mawe.

**Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali:**

Hapo zamani za kale alikuwepo mzee mmoja aliyeitwa Mtinga. Mzee huyo alikuwa maarufu sana pale kijijini kwao. Jina lake lilikuwa akilini mwa kila mtu awe mdogo au mkubwa. Alikuwa na kipaji cha kusema na kuvutia watu. Mzee Mtinga hakuwa na choyo na aliwapenda watu wanaofanya juhudi katika kutafuta maendeleo. Hakupenda ugomvi wala kulipiza kisasi kwa watu japokuwa watu walimkosea kwa kuwa yeye alikuwa na moyo mweupe. Kila wakati alikuwa yupo tayari kumsaidia mtu yeyote hata kama alikuwa hamfahamu. Kamuwe hakuwa mtu wa kujigamba "Yeye alielewa vizuri methali isemayo, "Tenda wema nenda zako usingoje shukrani".

Siku moja Mzee Mtinga alikuwa akikagua shamba lake la miwa. Alipokuwa anaendelea na ukaguzi huo, walipita wanafunzi ambao walikuwa wanatoka shule Wanafunzi hao walikuwa wanaongea. Mzee Mtinga alitega sikio ili asikie yale waliyokuwa wanayaongea.

Wale wanafunzi walikuwa wanajadiliana kuhusu faida za maji. Majadiliano ya wanafunzi wale yalimvuta sana nzee Mtinga. Akaamua kuwasalimia na kusema: "wajukua zangu, nimefurahi sana kusikia mkizungumza vizuri sana kuhusu faida za maji. Lakini kujua faida tu haitoshi. Ni lazima mjue na hasara zake pia kwani hakuna masika yasiyo na mbu."

Wale wanafunzi walipigwa na butwaa waliposikia Mzee Mtinga akisema kuwa maji yana hasara. Ana, mmoja kati ya wale wanafunzi akauliza, "Hivi babu maji yanaweza kuwa na hasara?

Mzee Mtinga alicheka kidogo kisha akajibu, "Oh! Maji yana hasara nyingi. Maji husababisha mafuriko yanapozidi kwa ajili ya mvua kuwa nyingi kupita kiasi. Mafuriko yanapotokea mimea yote humezwa na maji, barabara, zahanati na shule pia. Kadhalika, maji ya mvua husababisha makorongo ambayo huleta uharibifu mkubwa wa mazingira yetu."

Mwanafunzi mwingine aitwaye Nyamchele naye akauliza, "Babu tunajua kuwa hewa ina faida kubwa kwa viumbe. Je? Hewa nayo ina hasara?" Mtinga akacheka kidogo kisha akamwambia hewa chafu kama ile yenye moshi au vumbi ina hasara kwani huathiri mapafu. Pia hewa inayotoka viwandani huathiri mazingira yetu

Baada ya wanafunzi kujibiwa maswali yao, walimshukuru Mzee Mtinga. Kabla hawajaondoka, Mzee Mtinga aliwaambia, "wajukuu zangu, hakuna kitu kizuri duniani kama kuwa tajiri wa akili."

Wale wanafunzi walifurahi sana. Nyamchele alimpongeza Mzee Mtinga kwa kumshika mkono kisha akamuaga kwa niaba ya wenzake.

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja wahusika wa hadithi hii:

Jibu:

- ❖ Wahusika wa hadithi hii ni Mzee Mtinga na Wanafunzi.

2. Eleza wasifu wa Mzee Mtinga katika hadithi hii.

Jibu:

- ❖ Mzee Mtinga ni mtu mwenye moyo mweupe asiye na makuu. Hupenda kusaidia watu hata kama hakuwa akiwafahamu. Ni mzee asiyelipiza kisasi hata kama aliudhiwa na mtu na pia hakuwa mtu wa majigambo.

3. Eleza wasifu wa wanafunzi.

Jibu:

- ❖ Wanafunzi hao ni wadadisi wanaopenda kujifunza hata wanapokuwa nje ya shule. Hii inajidhihirisha pale walipokuwa wanaelezana juu ya umuhimu wa maji wakiwa njiani wanarudi shuleni

4. Ujumbe wa mwandishi katika hadithi hii ni upi?

Jibu:

- ❖ Ujumbe wa mwandishi katika hadithi hii ni kutaka kueleza jamii kuwa na moyo mweupe, tusiwe watu wa kujigamba wala kulipiza visasi hata watu wanapotuudhi. Pia kuwasaidia watu au kusaidiana wakati wowote hata kama mtu humfahamu unaweza kumsaidia. Tuwe

mfano wa kuigwa kama Mzee Mtinga. Na pia wanafunzi wawe na tabia ya kuendelea

kujifunza hata wanapokuwa nje ya mazingira ya shule. Hii inajionesha pale wanafunzi walipokuwa wanajadili umuhimu wa maji walipokuwa wanarudi shuleni.

5. Taja methali zilizotumika katika hadithi hii.

Jibu:

Methali zilizotumika katika hadithi hii ni:

- Tenda wema nenda zako usingoje shukrani
- Hakuna masika yasiyokuwa na mbu

6. Taja nahau zilizotumika katika hadithi hii.

Jibu:

Nahau zilizotumika katika hadithi hii ni:-

- Tega sikio
- Pigwa na butwaa

7. Unafikiri kichwa cha hadithi hii kinaweza kuitwaje?

Jibu:

- Kichwa cha habari hii kinaweza kuitwa Faida Na Hasara,

Andika methali inayoendana na maelezo yanayohusika:

1. Tunabishana kuhusu jambo hili wakati mwalimu yupo. Kwa nini tusimuulize ili tupate jibu sahihi.

- Methali: Kuuliza si ujinga.

2. Tukishirikiana tutapambana na kuwashinda majambazi, tusiposhirikiana watatuandama na kupora mali zetu.

- Methali: Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

3. Wazazi walimwonya kuhusu tabia yake ya kufuatana na vijana wa kijiweni na kuvuta bangi lakini hakuacha. Sasa hivi amekamatwa na polisi.

- Methali: Asiyesikia la mkuu huvunjika guu au asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

4. John hujiwekea akiba ya fedha benki kidogokidogo, sasa hivi ana fedha nyingi

- ❖ Methali: Haba na haba hujaza kibaba.

5. Wakulima walilima na kupalilia kwa shida sana, mazao yalipokomaa, walipata mavuno mengi.

- ❖ Methali: Mchumia juani hulia kivulini.

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kujaza vielezi sahihi:**

1. Dira hiyo ilimwongoza kwenda - (popote, yeyote) Jibu:

- ❖ Dira hiyo ilimwongoza kwenda popote.

2. Rehema aliyauza maembe hayo - (kabla ya, kwa mafungu) Jibu:

- ❖ Rehema aliyauza maembe hayo kwa mafungu.

3. Mtuhumiwa aliapa kutorudia jambo hilo - (kamwe, vibaya) Jibu:

- ❖ Mtuhumiwa aliapa kutorudia jambo hilo kamwe.

4. Kazi yake ni nzuri - ilipendeza (hivi, sana) Jibu:

- ❖ Kazi yake ni nzuri sana ilipendeza.

**Andika jibu sahihi:**

1. Mtu asiye na pua huitwa______________________
2. Mtu aliyefiwa na mume wake huitwa_____________________
3. Dada wa baba yako huitwa__________________
4. Mtu aliyezaliwa na meno tayari huitwa_______________
5. Chombo kinachozuia vitu visioze huitwaje kwa Kiswahili sanifu_________________
6. Mtu anayeongoza meli huitwa__________________
7. Mtu anayeipenda nchi yake na yuko tayari kuitetea huitwa____________________

8. Mtu anayemfuata imamu anayeongoza swala, au mfuasi katika sala____________

9. Mtu mwenye tabia ya kuzua na kutia fitina huitwa_________________

**Majibu:**

1. Toinyo
2. Mjane
3. Shangazi
4. Kigego
5. Jokofu
6. Nahodha
7. Mzalendo
8. Maamuma
9. Mzabizabina

**E. Kueleza maana za maneno mapya katika matini mbalimbali, kuyatumia katika sentensi na kuhusianisha na mazingira ya kila siku.**

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali:

Mawasiliano ni tendo la kupashana habari kwa watu, wanyama, ndege na viumbe vinginevyo. Binadamu wanapokuwa na dhamira ya kupashana habari hutumia lugha ya ishara na sauti. Wanyama, ndege na wadudu hutumia sauti zao kuwasiliana kuhusu furaha, huzuni, hadhari, maumivu, njaa au hatari. Binadamu kwa kutumia lugha anaweza kuwasiliana na wenzake na kutoa taarifa nyingi zaidi.

Kuna aina mbalimbali za habari kama vile; habari za kielimu, kiuchumi, kiutamaduni, kisayansi na kiteknolojia, kijamii na kadhalika. Ili habari hizi zicnee, lazima kuwe na mawasiliano baina ya watu.

Zipo njia mbalimbali za kufanya mawasiliano. Kuna mawasiliano ya mdomo. Katika njia hii watu

wawili au zaidi hutumia lugha ya mazungumzo kupashana habari.

Kinyume chake ni kuandikiana barua, rísala au notisi. Jambo la msingi hapa ni lugha. Watu wanaotaka kuwasiliana lazima watumie lugha wanayoielewa wote.

Njia nyingine ya mawasiliano ni kwa kutumia vyombo vya habari kama vile redio, luninga (televisheni) na magazeti. Kwa kutega sikio kwenye redio au kuangalia televisheni na kusoma magazeti na majarida tunapata habari za kielimu, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

Mawasiliano pia yanaweza kufanyika kwa njia ya simu ya mdomo, kuandika barua pepe na nukushi. Siku hizi kuna simu za mkononi. Haya ni maendeleo makubwa sana.

Badala ya taarifa kuchukua takribani wiki au miezi kadhaa, hutumia sekunde chache tu, kwa kutumia njia ya barua pepe, simu na nukushi.

Njia ni kwa kutumia kompyuta iliyounganishwa na mtandao wa intaneti. Kwa njia hii, watu wanaweza kupelekeana ujumbe, barua na makala mbalimbali. Siku hizi unaweza hata kusoma vitabu kupitia kompyuta. Pia unaweza kusomea shahada au kozi mbalimbali zilizopo ughaibuni kwa kutumia kompyuta na kupata cheti.

Japokuwa mtandao wa intaneti una faida kubwa kimawasiliano yapo mambo mabaya pia. Hivyo, sheria kali za kudhibiti usambazaji wa taarifa na picha zinazokiuka maadili zimewekwa.

**A. MSAMIATI:**

Toa maana ya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi:

**1. Habari:**

- ❖ Maelezo ya jambo fulani lililotokea
- ❖ Hutumika katika kuamkiana na kuuliziana

hali Sentensi:

- ❖ Kila siku jioni mama husikiliza taarifa ya habari kupitia kituo cha T.B.C Taifa

**2. Barua pepe**

Ujumbe unaotumwa kwa njia ya elektroniki kupitia kompyuta au simu iliyounganishwa kwenye mfumo wa mtandao wa intaneti

Sentensi:

- ❖ Dada yangu hutumiana ujumbe na rafiki yake aishie Marekani kwa njia ya barua pepe.

**3. Kompyuta**

- ❖ Mashine ya elektroniki ya kuhifadhi na kuchagua taarifa zilizoingizwa kukokotoa na kuongoza mitambo.

Seniensi:

- Mwalimu wetu alitufundisha jinsi ya kutengeneza kanzi data kwenye kompyuta

**4. Ughaibuni**

- Nchi za mbali

Sentensi

- Mwalimu alituambia tukisoma kwa bidii tunaweza kupata kazi ughaibuni

**5. Takribani**

- Neno linaloonesha ukaribiano wa vitu kwa hali au idadi karibia karibu,

Sentens

- Kutoka hapa hadi kijiji cha pili tunaweza kutumia takribani dakika ishirini.

**6. Shahada**

- Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo ili kuthibitisha kwamba amekamilisha masomo na kufaulu mitihani yake

Sentensi:

- Kaka yangu alipomaliza chuo alitunukiwa shahada ya usanifu majengo.

**B. UFAHAMU:**

1. Nini maana ya mawasiliano?

Jibu:

- Mawasiliano ni kitendo cha kupashana habari kwa watu, wanyama, ndege na viumbe vinginevyo.

2. Eleza tofauti baina ya mawasiliano ya wanyama na yale ya

binadamu, Jibu:

- Wanyama hutumia sauti zao kuwasiliana kuhusu furaha au huzuni wakati binadamu

hutumia lugha.

3. Toa mifano ya vyombo vya habari.

Jibu:

❖ Vyombo vya habari ni:

- Televisheni
- Redio
- Magazeti na majarida

4. Taja aina tatu za habari.

Jibu:

- Habari za kielimu
- Habari za kiuchumi
- Habari za kisiasa

**C. MAZOEZI YA LUGHA**

Kanusha sentensi zifuatazo:

1. Nitarudi

kesho Jibu:

❖ Sitarudi kesho

2 Sitaki kukaa hana

Jibu:

❖ Nataka kukaa hapa

3. Watoto walipatiwa chanjo ya kifua kikuu.

Jibu:

❖ Watoto hawakupatiwa chanjo ya kifua kikuu

4. Huyu ni

mwalimu Jibu:

❖ Huyu si mwalimu

5. Nyumba hiyo haitakuwa na vyumba

vingi Jibu:

- Nyumba hiyo itakuwa na vyumba vingi.

# KUTUMIA MSAMIATI KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

## 3.0. KUTUMIA MSAMLATI KATIKA MIKTADIA MBALIMBALI

### MAZUNGUMZO

Mazungumzo ni utaratibu wa kuongea baina ya pande mbili, ambapo kwa kawaida wahusika ni watu. Lugha ya mazungumzo huwa na mtindo na rejista zake.

**a) Kuwasilisha hoja na kuzielezea kwa kufuata mpangilio sahihi wa mawazo katika miktadba mbalimbali.**

### HOJA:

**Hoja** ni maelezo bayana yanayotolewa na mwandishi kutetea msimamo wake. Ili hoja zote zipate kueleweka ni sharti zipangwe kwa mtiririko wa mawazo ulio sahihi ili mtu asomapo aweze kuelewa ni jambo gani analizungumzia na msimamo kuhusu jambo hilo.

Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali:

Yapata miaka mitatu sasa tangu wazazi wa Nyambuli waage dunia. Miaka yote hiyo Nyambuli amekuwa akiishi maisha ya shida sana. Hakuwa na mbele wala nyuma.

Hakika mtoto huyu alipata bahati mbaya isiyoelezeka.

Miaka mitatu iliyopita, Nyambuli alikuwa anasoma darasa la saba katika shule ya msingi Lawate. Shule hiyo ipo Wilaya ya Siha katika mkoa wa Kilimanjaro. Nyambuli aliishi na wazazi wake waliokuwa wafanyabiashara wakubwa mjini Moshi.

Wazazi wake walipata ajali mbaya ya gari na kupoteza maisha papo hapo. Huu ndio ukawa mwanzo wa Nyambuli kuanza maisha mapya bila ya wazazi wake. Nyambuli alikuwa mtoto wa pekee kwani dada yake alifariki kwa kugongwa na pikipiki akiwa na miaka tisa. Ooh! maskini Nyambuli aliachwa yatima.

Kwa kuwa wazazi wake walikuwa na ukwasi, kila ndugu alijifanya kuwa mlezi wa Nyambuli. Wakati wote wa msiba hali ilikuwa shwari. Baba yake mkubwa alijigamba kwamba yeye ndiye mwenye mamlaka ya kumtunza Nyambuli. Baada ya kuanua matanga ilikubaliwa baba mkubwa amlee

Nyambuli kwani binti huyo ni yatima. Kwa kuwa mali zote za marehemu ziliandikwa jina la marehemu, baba yake mkubwa Nyambuli alifanya juu chini kubadili umiliki wa mali zile uwe kwa jina lake. Baada ya mwaka, mali za marehemu zilisajiliwa kwa jina la Sadoki Mariale.

Kwa upande wa Nyambuli maisha yalikuwa magumu kupindukia. Shule aliacha kwani baba yake mkubwa aliacha kumlipia ada. Mahitaji yote muhimu yalikuwa nadra kupatikana. Bwana Sadoki alitumia mali ile ovyo na kwa anasa. Baada ya muda mfupi mali zote za marchemu mdogo wake zikawa zimeyoyoma. Maisha yalizidi kuwa duni zaidi.

Nyambuli aliamua kutoroka na kwenda mjini kutafuta kibarua ili aweze kukidhi mahitaji yake. Huko nako hali haikuwa shwari. Hakupata kibarua katu. Hivyo ilimlazimu

kuzunira mjini akiomba wasamaria wema wampe chochote. Maskini ya Mungu! Nyambuli mtoto wa aliyekuwa tajiri maarufu bwana Samweli Mariale sasa ni mtoto anayeishi katika mazingira magumu. Ama kweli hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe.

**A. UFAHAMU**

Jibu maswali yafuatayo:

1. Nyambuli aliishi maisha gani baada ya kufiwa na wazazi wake?

Jibu:

- Nyambuli aliishi maisha ya shida sana baada ya kutiwa na wazazi wake.

2. Shule aliyosoma Nyambuli iliitwaje na ipo mkoa gani?

Jibu:

- Shule aliyosoma Nyambuli iliitwa Lawate ipo mkoa wa Kilimanjaro.

3. Kwa nini ndugu walitaka kuwa walezi wa Nyambuli?

Jibu:

- Ndugu walitaka kuwa walezi wa Nyambuli kwa sababu wazazi wake walikuwa na ukwasi.

4. Mtoto aliyefiwa na wazazi wake huitwaje?

Jibu:

- Mtoto aliyefiwa na wazazi wake huitwa yatima.

5. Baba yake Nyambuli aliitwa nani?

Jibu:

- ❖ Baba yake Nyambuli aliitwa Samweli Nyambuli.

6. Nani alimlea Nyambuli baada ya kifo cha wazazi wake?

Jibu:

- ❖ Aliyemlea Nyambuli baada ya kifo cha wazazi wake ni baba yake mkubwa, bwana Sadoki Mariale,

7. Nini maana ya neno yoyoma kama lilivyotumika katika habari hii?

Jibu:

- ❖ Maana ya neno yoyoma ni kuishi bila mpangilio.

8. Taja methali iliyotumika katika habari hii.

Jibu:

- ❖ Methali iliyotumika katika methali hii ni "Ama kweli hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe."

9. Andika kichwa cha habari hii uliyoisoma.

Jibu:

- ❖ Kichwa cha habari ni NYAMBULI AWA YATIMA,

**B. MSAMIATI**

Tunga sentensi kutokana na msamiati:

**1. Ukwasi**

- ❖ Baba yake ana ukwasi anaweza kununua bata ndege,

**2. Ajali**

- ❖ Wazazi wa Nyambuli walifariki kwa ajali ya gari.

**3. Bahati**

- Kaka yangu alipata bahati ya kujiunga na shirika la ndege.

**4. Zurura**

- ❖ Mtaani kwetu mbuzi huzurura hovyo.

**5. Shwari**

- ❖ Baada ya Waziri Mkuu kuhutubia hali ilikuwa shwari.

**6. Wafanyabiashara**

- ❖ Wazazi wangu ni wafanyabiashara wanaomiliki makampuni makubwa,

**7. Kibarua**

- ❖ Juma alipata kibarua baada ya kuhangaika kwa muda mrefu

**C. MALEZI YA LUGHA:**

Andika neno lisiloendana na mengine katika kila kundi:

1. Bunduki, bastola, mshale, sahani, gobore_________________
2. Babu, bibi, mama, shangazi, dada________________
3. Mwanaume, beberu, fahali, jogoo, mwanamke________________
4. Kati, baibui, buibui, kanga, kitenge________________
5. Bahari, ziwa, korongo, mto, bwawa________________
6. Matawi, shina, matunda, mlango________________
7. Mwavuli, shati, seksi, kanga, shuka________________
8. Meli, jahazi, gari, ngalawa, mtumbwi________________
9. Baiskeli, gari moshi, ndege, bajaji________________
10. Ugali, wali, kande, soda, samaki________________

**Majibu:**

1. Sahani
2. Babu
3. Mwanamke
4. Buibui
5. Korongo
6. Mlango

7. Mwavuli

8. Gari
9. Ndege
10. Soda

b) **Kubainisha aina saba za maneno na dhima zake katika sentensi na kutambua kifupisho cha kila aina ya neno**.

**NENO:**

**Neno** ni sehemu fupi ya lugha yenye maana. Ni sauti inayotamkwa au kuandikwa pamoja na kutaja jambo fulani. Neno linaweza kuwa fupi lenye mofimu (yaani sauti

inayowakilisha maana fulani) moja tu au kuwe refu lenye mofimu mbalimbali. Kwa kawaida ni muunganiko wa silabi kadhaa. Mfano **ba + ba= baba. Irabu u + 2 = ua**

**AINA ZA MANENO**

Aina za maneno uhusisha mgawanyo wa maneno hayo kulingana na matumizi yake. Zipo aina saba za maneno ambazo ni:

**1. NOMINO (N)**

Nomino hufanya kazi ya kutaja jina la mtu, kitu hali au mahali.

Mfano: baba, Tanzania, ugonjwa nk.

Baba analima, chakula kimemwagika

N N

Zipo aina mbalimbali za nomino ambazo ni:

**i. Nomino za kawaida**

Nomino hizi hazibainishi waziwazi vitu vinavyotajwa. Ikiwa ni mtu hatambuliwi kama ni Juma au Asha, ikiwa ni mlima hautambuliwi kama ni Kilimanjaro, Meru, hutaja kwa jumla. Mfano: baba, mvulana, mji, nchi. Nomino hizi kwa jina jingine huitwa nomino za jumla.

Mfano:

Rafiki yangu amekufa

N

Baba analima

N

ii. **Nomino za kipekee**

Nomino hizi hutaja na kutambulisha nomino mahsusi na kipekee. Yaani kitu ni hicho hicho wala si kitu kingine. Mfano: Juma, Arusha, Mlima Kilimanjaro nk Herali za

kwanza za nomino za kipekee huwa ni kubwa hata kama nomino hizo zinapatikana katikati ya sentensi

Mfano:

Mpelwa anafua nguo

N

iii. **Nomino za jamii**

Hizi ni Domino zinazowakilisha vitu vingine katika jina moja. Yaani hutaja ujumla wa vitu vingi. Mfano: Jeshi timu, mkutano, kamati.

Timu yetu ilishinda kwa kishindo.

N

iv. **Nomino dhahania**

Hizi ni nomino zinazofikiriwa pasipo kuonekana

Mfano: Malaika. Zimwi. Jini.

v. **Nomino za wingi**

Nomino hizi hudokeza dhana ya wingi japokuwa zenyewe hazina wingi wala umoja. Umbo la nomino hizi linafanana na nomino zilizo katika wingi japokuwa mfano huo ni wa bahati tu.

Mfano: maziwa, maji, manukato, majadiliano.

Maziwa yamemwagika.

N

vi. **Nomino za matendo**

Nomino hizi huonesha matendo.
Mfano: ukulima, ufugaji, mapigano.
Mapigano yalizuka mjini.

N

**MASWALI:**

Onesha nomino katika sentensi zifuatazo:

1. Asha anafua zile nguo chafu N N
2. Halima anakula chakula kibaya. N N
3. Mlima Kilimanjaro ni mrefu.

   N
4. Watoto wote wameondoka. N
5. Shule yetu ni nzuri. N

Soma maneno yafuatayo kisha bainisha ambayo ni nomino:

- Imba
- Chama
- Ali
- Malaika
- Fagia
- Shambani
- Gari
- Mto Ruvu
- Wanajeshi
- Vizuri sana

- Yote
- Majadiliano
- Maziwa

Majina ambayo ni nomino:

- Malaika
- Ali
- Gari
- Mto Ruvu
- Chama
- Wanajeshi
- Maziwa
- Majadiliano

**2. VIVUMISHI (V)**

Haya ni maneno yanayotoa taarifa ya ziada katika Domino. Hufanya kazi ya kufafamua kuelezea zaidi kuhusu nomino ili kupambanua kutofautisha nomino husika miongoni mwa nomino nyingine.

Mfano:

Mtoto wangu amefaulu, yule mpole amesafiri.
V V

**AINA ZA VIVUMISHI**

i. **Vivumishi vya idadi**

Vivumishi hivi hutumika kueleza kuhusu idadi ya nomino. Yaweza kuwa idadi isiyodhihirika. Mfano: wengi, wastani, nyingi nk au idadi halisi. Hapa nambari hutumika kueleza idadi ya nomino, mfano: kumi, elfu.

Mfano:

Watu wengi waliabudu sanamu lakini watatu walikataa.
V

ii. **Vivumishi vya sifa**

Hivi hutumika kutoa sifa za nomino mbalimbali, mfano: kali, safi, mfupi mnene n.k

Mfano:

Yule kijana mrefu ana pua kubwa

V V

**iii. Vivumishi viulizi**

Hutumika kuuliza swali, mfano: gani? yupi?
Mtoto yupi amevunjika?

V

**iv. Vivumisha vya a-unganifu**

Vivumishi hivi huundwa kwa mzizi wa kihusishi a - unganifu. Kihisishi hiki huandamana na nomino kuunda kirai husishi ambacho huvumisha nomino iliyotajwa awali.

Vivumishi hivi huleta dhana za umilikaji wa nomino na nafasi katika orodha.

Mfano: ya, cha, za.

Nguo za juma zilianguka alipocheza.

**v. Vivumishi vya kumiliki**

Vivumishi hivi hutoa taarifa ya kujulisha umiliki wa nomino. Maneno yake hujulisha kuwa nomino hiyo iliyotajwa ni mali ya nani.

Mfano: yangu, wao, wenu.

Nyumba yangu imebomoka

V

**vi. Vivumishi vya kuonesha**

Vivumishi hivi hutoa taarifa ihusuyo nomino au kiwakilishi cha nomino kwa kudokeza umbali au ukaribu wa nomino iliyotajwa. Umbali huo unaweza kuwa karibu, mbali kidogo au mbali sana. Pia tunaweza kuvitupia katika wingi au umoja tukizingatia ngeli za nomino na upatanisho wa kisarufi.

Mfano: kile, ile, hii.

Kidumu kile ni changu.

V

Jembe hili limevunjika.

V

**MASWALI:**

Tambulisha vivumishi katika sentensi zifuatazo:

1. Watoto wazuri wanacheza muziki.

V

2. Kwetu kuna mama mmoja anapika maandazi.

V

3. Wanafunzi wangapi wamefaulu mtihani?

V

4. Gari lile ni langu.

V

5. Mwanafunzi hodari husoma kwa bidii

V

6. Viatu hivi vimechakaa.

V

7. Nguo za Juma zilianguka.

V

**3. VIWAKILISHI (W)**

Haya ni maneno yanayosimama badala ya nomino. Maneno hayo hutumika pale tu ambapo nomino haipo au haikutajwa, huenda kwa kuwa imeshatajwa hapo awali au inafahamika katika mazingira husika.

Mimi ni mwalimu.

W

Wote wamepotea.

W

**AINA ZA VIWAKILISHI:**

Zipo aina mbalimbali za viwakilishi ambazo ni:

a) **Viwakilishi vya kuuliza/viulizo**

Viwakilishi hivi husimama badala ya nomino iliyoulizwa.

Mfano:

- Nani anagonga ?
- Lipi ni zima?
- Mangapi ni mabovu?

b) **Viwakilishi vya sifa**

Viwakilishi hivi huonesha sifa za nomino zinazowakilisha.

Mfano:

- Mfupi amelala
- Mjinga kaondoka
- Mchangamfu anakuja kesho

c) **Viwakilishi vya idadi**

Viwakilishi hivi hujulisha idadi ya watu au vitu. Idadi inaweza kuwa ya jumla au kamili.

Mfano:

- Wanne wamekamatwa idadi kamili)
- Wengi hawakufika (idadi ya jumla)

d) **Viwakilishi vya kuonesha/vioneshi/mahali**

Haya ni maneno yanayosimama badala ya nomino ili kujulisha/kudokeza ukaribu au umbali wa nomino hiyo ambayo hutoka kwa mzungumzaji.

Mfano:

- Yule ni mvivu
- Wale wameondoka
- Hili limeiva

e) **Viwakilishi vya nafsi**

Haya ni maneno yanayosimama badala ya majina yanayotaja nafsi za watu. Viwakilishi vya nafsi vimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni:

- Viwakilishi vya nafsi huru
- Viwakilishi vya nafsi kiambata

**a. Viwakilishi vya nafsi huru**

Haya ni maneno yanayoweza kusimama peke yake bila kuambatanishwa katika neno au mzizi wa

| NAFSI | UMOJA | UWNGI |
|---|---|---|
| I | Mimi | Sisi |
| II | Wewe | Ninyi / Nyinyi |
| III | Yeye | Wao |

neno jingine.

Mfano:

- ❖ Mimi ni mkulima
- ❖ Ninyi ni wakulima
- ❖ Sisi ni walimu
- ❖ Yeye ni mwalimu
- ❖ Wao ni walimu

**b. Viwakilishi vya nafsi kiambata**

Hizi ni mofimu tegemezi /vipande vya maneno vinavyoambikwa au vinavyoambatanishwa katika neno au mzizi wa neno jingine ili kudokeza nafsi inayohusika.

Mfano:

| NAFSI | UMOJA | WINGI | MZIZI |
|---|---|---|---|
| I | NI | TU | Ni kija – Tu kija |
| II | U | M | U kija – M kija |
| III | A | WA | A kija – Wa kija |

**vii. Viwakilishi vya kumiliki/ vimilikishi**

Hivi huonesha umiliki na umiliki huo huhusishwa moja twa moja na nomino inayohusika.

Mfano:

- ❖ Kwetu ni karibu

- Kwao ni walevi

### viii. Viwakilishi vya -a-unganifu

Haya ni maneno ya sifa yanayosimama badala ya pomino inayosifiwa kwa kutumia a-unganifu.

Mfano:

- ❖ La saba wamemaliza
- ❖ Vya China ni feki

### ix. Viwakilishi vya urejeshi /virejeshi

Haya ni maneno yanayorejelea nomino an sayo haikutajwa. Maneno hayo huwa na kirejeshi kinachorejelea na nomino yenyewe haitajwi.

Mfano:

- ❖ Aliyemaliza aondoke
- ❖ Lililoiva litaliwa leo
- ❖ Alimoingia mna vumbi sana

### x. Viwakilishi vya pekee

Hivi hubainisha nomino ambayo hutajwa kwa kutumia viambishi vya:

-ote, -o-ote, -enye-, -enyewe, na -ingine.

Viwakilishi hivi huitwa vya pekee kwa sababu kila mmoja hutoa taarifa fotauti (ya peke yake) na chenzake. Kimsingi mizizi yake ipo mitano.

**MCHANGANUO:**

**a. a ote-**

Maana hasa ya hali ya "kutokubaki na kitu" ukiwa mazungumzoni

Mfano:

- ❖ Yote yamemwagika
- ❖ Zote zimeharibika

- ❖ Chote kimeliwa

**b. 0-ote-**

Maana hasa ni hali ya kutokuchagua "pasipo uchaguzi"

Mfano:

- Yeyote aje
- Lolote liwe
- Zozote zitapendezwa

**c. -enye-**

Maana hasa ni hali ya "umiliki"

Mfano:

- Mwenye nyumba amefariki
- Vyenye sukari vimeharibika

**d. enyewe-**

Maana hasa ni hali ya msisitizo"

Mfano:

- Yenyewe imepasuka
- Chenyewe kimetoboka
- Kwenyewe kumenuka

**e. -ingine-**

Maana hasa ni hali ya "nyongeza"

Mfano:

- Mwingine amefariki
- Kingine kimepotea
- Nyingine imepauliwa
- Vingine vimeletwa

### xi. Viwakilishi vya amba

Haya ni maneno yanayosimama badala ya nomino kwa kutumia mzizi wa amba

Mfano:

- Ambaye amemaliza aje

- ❖ Ambazo zimeoza zitatupwa
- ❖ Ambacho kina sumu kimechomwa

**MASWALI:**

Onesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo:

1) Sisi tunakabiliwa na changamoto nyingi.

   W

2) Yenu na yetu yameharibika.

   W W

3) Mwenyewe kafika.

   W

4) Yenu ni ya zamani, yetu ni

   mpya W W

5) Watatu wanatakiwa kwenda sokoni.

   W

6) Lipi limeharibika?

W

7) Mfupi kuliko wote

   amefika W

**4. VIELEZI (E)**

Haya ni maneno yanayotoa taarifa ihusuyo kitenzi. Maneno hayo huelezea /hufafanua na kupambanua au kuongeza maana zaidi ya namna jinsi tendo linavyotendeka, Idadi au kiasi cha kutendeka kwa tendo hilo, mahali ambapo tendo linatendeka. Hivyo vielezi ni maneno yanayotoa taarifa ili kukijulisha kitenzi hicho kimetendeka kwa namna gani, au jinsi gani, mara ngapi au kwa kiasi gani, wapi, lini na kwa sababu gani. Wakati mwingine vielezi hutoa taarifa inayohusu nomino, viwakilishi, vivumishi na hata vielezi vyenzake.

AINA ZA VIEL EZIE)

Zipo aina mbalimbali za vielezi nazo ni:

## I. Vielezi vya namna

Haya ni maneno yanayotoa taarifa au ufafanuzi ambao unaelezea namna au jinsi kitenzi (tendo) linavyofanyika na maneno haya hujulisha kuwa kitenzi hicho kita namna gani au jinsi gani.

Vieleza hivi vya namna vimegawanyika katika makundi madogomadogo sita, ambayo ni:

### a. Velezi halisi

Vielezi hivi kazi yake ni kutoa taarifa ihusuyo kitenzi

Mfano:

- ❖ Nyoka anakimbia sana
- ❖ Hadija anaandika vizuri
- ❖ Asha amejikwatua mno

### b. Vielezi vinavyoofafanua vivumishi

Mfano:

- ❖ Baba amenunua nyumba nzuri sana
- ❖ Ndondi si mchezo nzuri kabisa

### c. Vielezi vya ki-ya mfanano

Mfano:

- ❖ Halima anaimba kitoto
- ❖ Rahimu amevaa kiuni

### d. Vielezı vya hali

Vielezi hivi vina uhusiano na tabia kitu. Nomino za dhahania zinapotumika kufafanua kitenzi huwa kielezi.

Mfano:

- ❖ Barabara zetu zimejengwa upya

- ❖ Gari hili hukimbia kwa kasi

**e. Vielezi viigizi**

Hivi hufuatisha/huiga mlio unaotokea baada ya tendo kutendeka.

Mfano:

- ❖ Maji yamemwagika mwaa
- ❖ Ali ameanguka puu

**f. Vielezi vikariri /vibariki /viradidi**

Haya ni maneno yanayofafanua kielezi kuwa kitenzi hicho kimetendeka mara ngapi au kwa kiasi gani. Idadi hiyo inaweza kuwa idadi ya jumla au idadi kamili

Mfano:

- ❖ Mtoto anatembea polepole
- ❖ Ali analima kinyumenyume

**II. Vielezi vya idadi**

Haya ni maneno yanayofafanua kielezi kuwa kitenzi hicho kimetendeka mara ngapi au kwa kiasi gani. Idadi hiyo inaweza kuwa idadi ya jumla zu idadi kamili.

Mfano:

- ❖ Jamali ameanguka mara nyingi
- ❖ Makande hupikwa mara mbili
- ❖ Gari lilipinduka mara tatu.

**III. Vielezi vya mahali**

Ni maneno yanayofafanua kwa kujulisha mahali ambapo kitenzi hicho kinatendeka/kimetendeka.

Mfano:

- ❖ Mtoto amelala chumbani

- Mama amekwenda shambani
- Panya amejificha shimoni

- Vielezi vya mahali hujengwa kwa kuambikwa/kuambatanishwa na "ni" mwishoni mwa nomino inayokubali upatanisho wa kisarufi baada ya kuongezewa hiyo ni mwishoni mwake.

Mfano:

| NOMINO | KITENZI |
|---|---|
| Duka | Dukani |
| Shamba | Shambani |
| Chumba | Chumbani |
| Shule | Shuleni |

**IV. Vielezi vya wakati**

Ni maneno yanayofafanua kielezi kwa kujulisha wakati ambao kitenzi hicho kinatendeka /kimetendeka.

Vielezi vya wakati vinaweza kuwa vya majina ya siku, wiki, mwezi, majira ya mwaka, nyakati za siku, matukio ya kihistoria n.k

Mfano:

- ❖ Wakulima hupanda wakati wa masika
- ❖ Jambazi sugu limeuawa jana usiku
- ❖ Nitasafiri wiki ijayo
- ❖ Mimi nilizaliwa wakati wa vita vya majimaji

**V. Vielezi viulizi**

Hivi huuliza juu ya tendo linavyofanyika, lilipofanyika, lililotendwa, lilipofanywa.

Mfano:

- ❖ Baba amenunua nini?
- ❖ Asha anasoma wapi?

**5. VITENZI (T)**

Haya ni maneno yanayoeleza jambo lililotendwa. Vitenzi huarifu tendo lililofanyika au litakalofanywa na mnyama, mtu au kiumbe chochote kinachoweza kutenda jambo.

Mfano: cheza, lima, panda, imba.

Mara nyingi vitenzi huwa havisimami peke yake vinatumika katika tungo, bali huambatana na viambishi vingine vyenye kuwakilisha mtenda au mtendwa wa jambo.

Vilevile huambatana na viambishi vyenye kuonesha wakati wa tendo lilipofanyika.

Mfano:

- ❖ Baba analima - a-na-lima
- ❖ Watoto wanacheza wa-na-cheza

Wazungumzaji wa Kiswahili hutumia vitenzi pamoja na viambishi ili kuonesha nafsi ya mtenda na pia wakati tendo lilipofanyika. Ni mara chache sana ambapo wazungumzaji hutumia vitenzi visivyochukua viambishi. Hali hii hutokea wakati mzungumzaji anapotoa amri. Mfano: imba, tembea, simama.

**AINA ZA VITENZI:**

**i. Kitenzi kikuu (T)**

Ni kitenzi ambacho hutoa wazo kwa tendo ambalo linatendwa na nomino au kiwakilishi cha nomino. Mara nyingi kitenzi kikuu hukaa peke yake katika sentensi na hutoa taarifa kamili bila ya kuhitaji msaada wa kitenzi kingine.

Mfano:

- ❖ Baba yangu anacheza vizuri
- ❖ Shamba langu limepandwa mahindi
- ❖ Sisi tunasoma Kiswahili

**SIFA ZA KITENZI KIKUU (T)**

a. Huweza kusimama peke yake katika tungo au sentensi na kukamilisha taarifa bila ya kuwepo kitenzi kingine.

Mfano:

- ❖ Mama anakula

b. Huweza kuonesha ukanushi au

uyakinishi Mfano:

- ❖ Ali anakimbia (uyakinishi)

- ❖ Wewe hutacheza kwaito (ukanushi)

**ii. Kitenzi kisaidizi (Ts)**

Kitenzi hiki hukaa sambamba na kitenzi kikuu ili kusaidia kukamilisha taarifa, Kitenzi kisaidizi kikiwa peke yake hakiwezi kutoa taarifa kamili, hivyo basi kinahitaji kitenzi kingine ndipo taarifa yake ikamilike.

Mfano:

- ❖ Mtoto aliyekuja ameondoka
- ❖ Bibi yangu alikuwa anaumwa

**iii. Kitenzi kishirikishi (t)**

Hiki ni kitenzi ambacho hujulisha hali ya kuwepo au kutokuwepo kwa uhusiano /ushirikiano baina ya vipashio vya lugha. Uhusiano huo unaweza kuwa katika tabia, hali au mazingira fulani.

Mfano:

- ❖ Juma ni mwizi
- ❖ Kikombe ki kabatini

**AINA ZA VITENZI VISHIRIKISHI (t)**

**1) Vitenzi vishirikishi vikamilifu**

Haya ni maneno ambayo yamekamilika yaani hayahitaji mofimu/kiambishi/silabi/neno au kitenzi kingine.

**MIZIZI YA VITENZI VISHIRIKISHI:**

**i. Kuwa:**

Endapo utakuwa na kitenzi cha mzizi wa kuwa kimekaa peke yake katika sentensi na kimetoa taarifa kamili basi hicho ni kitenzi kishirikishi.

- ❖ Ali alikuwa mtulivu darasani
- ❖ Fatuma hakuwa mtoro

**ii. Ni:**

Hiki ni kitenzi kishirikishi kinachojulisha uyakinishi wa tendo. Kitenzi hiki hujulisha kuwepo kwa uhusiano baina ya vipashio vya lugha.

Mfano:

- ❖ Juma ni mcheshi
- ❖ Simba ni mnyama mkali

**iii. Si**

Hiki ni kitenzi kishirikishi kinachojulisha ukanushi wa tendo. Kitenzi hiki hujulisha kuwepo kwa uhusiano baina ya vipashio vya lugha.

Mfano: :

- ❖ Halima si mchokozi
- ❖ Asha si mtiifu
- ❖ Abi si mwimbaji

**iv. Vitenzi vishirikishi vinavyojulisha umiliki**

Hivi ni vitenzi vinavyotoa taarifa ya umiliki kwa nomino au kiwakilishi.

Mfano

- ❖ Juma ana gari zuri
- ❖ Chakula kina mafuta mengi
- ❖ Juma ana mke mzuri
- ❖ Chatu hana miguu

**v. Vitenzi vishirikishi vya viambishi ngeli**

Hivi ni vitenzi vinavyobainisha maana ya ngeli ikisimama peke yake.

Mfano:

- ❖ Ndoo i bwawani
- ❖ Kikombe ki kabatini
- ❖ Jembe li shambani

**vi. Vitenzi vishirikishi vipungufu**

Hivi ni vitenzi vyenye mzizi wa "ndi". Vitenzi hivi hujulisha msisitizo wa jambo. Vitenzi vishirikishi vipungufu huchukua viambishi vya nafsi na viambishi vya ngeli ya urejeshi.

Kuna mizizi miwili ya vitenzi vishirikishi vipungufu navyo ni nafsi na ngeli za urejeshi.

**i. Nafsi**

Mfano:

- ❖ Mimi ndimi mjukuu wao
- ❖ Wewe ndiwe mwalimu wao
- ❖ Ninyi ndinyi walimu wao
- ❖ **Wao ndio walimu**

**ii. Vya ngeli ya urejeshi**

Mfano:

- ❖ Humu ndimo alimoingia
- ❖ Hiki ndicho kitabu chake
- ❖ Hizi ndizo ndizi zake

Bainisha vitenzi katika sentensi zifuatazo:

1) Baba na mama wanalima.

T

2) Mtoto aliyeondoka amegongwa na gari.

Ts T

3) Ali si
mvivu t

4) Chakula kina
chumvi nyingi. t

5) Darasa la saba wanasoma kwa bidii.

T

6) Mwalimu alijeruhiwa amefariki.

T's T

7) Jembe li

shambani.

t

## 6. VIUNGANISHI (U)

Viunganishi ni neno au kikundi cha maneno chenye kuunganisha vipashio vya lugha ili kuuada kipashio kikubwa zaidi. Pia ni maneno yanayounganisha maneno mengine.

Kiunganishi kinaweza kuunganisha neno na neno, kirai na kirai, kishazi na kishazi, senteusi na sentensi au vinginevyo.

Mfano:

- Baba na mama
- Mama anafua na baba anasoma gazeti
- Shoka limeshindwa sembuse kwanja

Maumbo ya viunganishi ni:

Na, lakini, ingawa, bila, sembuse, ila, kwa sababu, kwa kuwa, pamoja na, iwapo, labdа nk

**AINA ZA VIUNGANISHI:**

Zipo aina mbili za viunganishi navyo ni:

**i. Viunganishi huru**

Hivi ni viunganishi vinavyosimama peke yake katika tungo katikati ya vipashio vinavyoungwa.

Mfano:

- Sisi tunaimba na kucheza
- Baba anafua lakini mama amelala

**ii. Viunganishi tegemezi**

Hivi ni vile ambavyo huundwa kwa viambishi o - rejeshi vinavyowekwa katika kislazi huu kwa pamoja kuunda sentensi changamano. Viambishi hivyo ni kama vile: po, ye, lo, cho

Mfano:

- Mama anayepika ni mchaga
- Aliowaona aliwataja.

Bainisha viunganishi katika sentensi hizi:

1) Karanga na mtama hupandwa shambani.

U

2) Anasoma ingawa anaumwa.

U

3) Ashura aliondoka kisha Juma akamfuata.

U

4) Hakuja shule kwa kuwa alikuwa anaumwa,

U

5) Mimi nimeshindwa kukwea mti sembuse wewe,

U

**7. VIHISISHI:**

Vihisishi ni maneno yanayodokeza vionjo na miguso ya moyo au ya akili.

Vionjo vya moyo huweza kuwa vya furaha au huzuni. Maneno hayo kwa kawaida huwepa alama ya mshangao (!) au hutengwa kwa mkato yatokeapo katika maandishi

Mfano wa maneno hayo ni Loo! Ebo! La hasha! nk

Kila kihisishi huweza kuibua hisia mahsusi, kwa hiyo ni vyema kutumia kihisishi kinachofaa.

Mfano:

❖ Lo! Maajabu ya Musa bayo!

❖ Salale! Angalia alivyochafuka!

**c) Kutunga sentensi kwa kutumia aina saba za maneno kwa usahihi kwa kuzingatia miktadha mbalimbali.**

**SENTENSI**

Sentensi ni kipashio cha juu kabisa katika tungo chenye muundo wa kiima na kiarifu ambacho hutoa taarifa kamili.

Mfano:

❖ Baba /analima

- **Kiima/kiarifu**

**AINA ZA SENTENSI:**

Kuna aina kuu nne za sentensi nazo ni:

1) **SENTENSI SAHILI**

Hii ni aina ya sentensi iliyoundwa kwa kishazi huru kimoja tu.

Mfano: Watoto wanacheza.

2) **SENTENSI CHANGAMANO**

Hii ni aina ya sentensi iliyoundwa kwa kishazi tegemezi na kishazi huru. Mfano: Mtoto aliyeondoka kwa shangwe na vigelegele amepotea

3) **SENTENSI AMBATANO**

Hii ni aina ya sentensi iliyoundwa kwa sentensi mbili zilizounganishwa na kiunganishi.

Mfano: Baba analima ingawa mama anacheza

Sentensi ambatano huweza kuundwa kwa sentensi sahili na sentensi sahili, sentensi sabili na sentensi changamano, sentensi changamano na sentensi changamano.

4) **SENTENSI SHURUTIA**

Hii ni aina ya sentensi iliyoundwa kwa mofimu za masharti. Mfano: ki, ngeli, ngali

Mfano:

- Akija anione.
- Angelisoma kwa bidii angelifaulu mtihani

Kutunga sentensi kwa kutumia aina saba za maneno:

1) Mama yangu anafua.

   N V T

2) Mtoto amekula chakula kibaya.

   N T N V

3) Mwalimu aliyepotea ameonekana jana.

N TS T E

4) Mama amekwenda sokoni.

N T E

5) Mtoto huyu anaimba vizuri

N V T E

**MAZOEZI YA LUGHA:**

Kanusha sentensi zifuatazo:

1. Juma alikwenda

shuleni Jibu:

- Juma hakwenda shuleni

2. Asha ni msichana

mvivu Jibu:

- Asha si msichana mvivu

3. Jembe humtupa

mkulima Jibu:

- Jembe halimtupi mkulima

4. Chakula hiki kina mafuta

mengi Jibu:

- Chakula hiki hakina mafuta mengi

**d) Kutunga hadithi fupi na kuelezea mafunzo yanayopatikana katika hadithi hiyo na kuhusianisha na maisha ya kila siku.**

**Hadithi** ni tungo za fasihi za masimulizi zitumiazo lugha ya nathari (lugha ya ujazo, ya maongezi

ya kila siku). Masimulizi hayo hupangwa katika mtiririko wa vitukio

unaokamilisha kisa. Ili kisa hiki kikamilike hadithi lazima iwe na wahusika ambao ndio nyenzo ya kukiendesha kwa chenyewe. Vivyo hivyo hadithi huwa na maudhui.

okamilika

**FAIDA ZA HADITHI:**

i. Kuburudisha:

Hadithi huburudisha watu walichoka baada ya kufanya kazi mchana kutwa.

ii. Hukuza ushirikiano:

Hadithi husimulia mambo yanayohusu ushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii mfano kilimo, misiba, ufugaji, uwindaji, harusi nk

iii. Kurithisha amali za jamii kutoka kizazi kimoja kingine

Hadithi hurithisha mila na desturi za jamii fulani kutoka kizazi kimoja hadi nyingine.

iv. Huliwaza jamii

Hadithi pia huweza kutumika kwa kuliwaza watu waliopatwa na majonzi au wale ambao wapo katika hali ya kuchanganyikiwa kwa kuwasimulia hadithi au kusikiliza.

v. Kujenga jamii na kuipa mwelekeo

Lengo la kusimulia hadithi ni kuifanya jamii iwe na mwelekeo mzuri unaozingatia maadili katika jamii

vi. Kuelimisha:

Katika hadithi kuna maadili na ujumbe unaotolewa kwa jamii. Hivyo kwa njia hii hadithi hutumika kama chombo cha kuelimisha jamii. Mfano hadithi husimulia tabia za uchoyo, uzembe, wizi, wivu, na matatizo yaliyowapata huwa funzo kwa jamii.

Soma hadithi ifuatayo kisha jibu maswali:

**MTOTO UMLEAVYO NDIVYO AKUAVYO**

Kuzoea ni Jambo la heri. Japo baadhi ya watu wengine husema kuzaa ni kuondoa maradhi maradhi tumboni. Mimi sikubaliani na usemi huo kwani ninaamini mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Sitofautiani sana na wanaotumia methali nyingine isemayo "mchelea mwana kulia hulia yeye"

Methali zote hizi mbili zisingeweza kutumika ndani ya familia yam zee Masenza na mkewe kama wangekubali kufuata methali isemayo "samaki mkunje angali mbichi" au wengine wasemavyo "uwahi ungali maji.

Udokozi wa mtoto wao Nyakisageni ungeweza kukomesha mapema kabla ya kuota mizizi lakini haikua hivyo. Kwani udokozi uliendelea kwa kasi hadi ukashika hatamu. Nyakisageni amekua na mkono mrefu, wizi wake sasa umekubuhu.

Inasikitisha kuona kijana mdogo ambaye alipaswa kuwa chuo kikuu lakini amekua mwizi. Haifai kuoka wala kurumangia. Kinywa chake hutoa maneno machafu kama jaa. Amekua jambazi sugu, mcheche wa huruma, katili kupindukia.

Laiti kama wazazi wake wangaemkanya mapema tangu Nyakisagani alivyoanza tabia ya kukwapuakwapua mtaani, hivi leo mzee Masenza asingalikuwapo kizimbani, akisubiri hukumu ya kulipa faini au kwenda jela. Ama kweli ama kweli uchungu wa mwana aujuae mzazi. Hivi hivi mtu asingelichukua dhamana ya kumdhamini. Nyakisagani kutokana na jinsi alivyo mkatili. Kweli mchuma janga hula na wa kwao.

Kutoroka kwa Nyakisagani kumeleta taharuki ndani ya familia. Watu hawali chakula kutokana na visa alivyofanya Nyakisagani. Nyakisagani kurudi tena nyumbani ni ndogo, japokua waswahili busema mwenda kwao si mtoro ila si kwa Nyakisagani. Hakuna la kufanya ni kushukuru tuu, kwani maji yakisbamwagika hayazoleki.

A UFAHAMU:

Jibu maswali yafuatayo:

1. Bainisha mafunzo yanayopatikana katika hadithi hii ukihusisha na maisha ya kila siku.

Jibu:

- Maisha yanayopatikana katika hadithi hii ni:

i. Wazazi wawakunje watoto wao pale wanapoona wameanza tabia ambazo si salama mfano wizi, wawakemee mapema kabisa.

ii. Pia wazazi wawalee watoto tangu wadogo kwa kuwaelekeza maadili mema ili wasije wakaingia katika tabia za wizi.

2. Orodhesha methali zinazopatikana katika

hadithi hii: Jibu:

i. Uchungu wa mwana aujuaye mzazi

ii. Mchelea mwana kulia hulia yeye

iii. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
iv. Samaki mkunje angali mbichi
v. Maji yakishamwagika hayazoleki
vi. Mchuma janga hula na wakwao.

3. Mwandishi anasema mchelea mwana kulia hulia yeye. Kwa nini mzee Masenza Analia?

Jibu:

❖ Mzee Masenza Analia kwa sababu mwanae ametoroka na anapaswa kulipa faini au kwenda jela.

**B. MAZOEZI YA LUGHA**

Toa maana ya nahau zifuatazo:

1) Mbiu ya mgambo
2) Mkono mrefu
3) Kula njama
4) Kutia utambi
5) Kutia kiraka
6) Vunjika moyo
7) Kumchimba mtu
8) Mezea mate
9) Ulimi wa panga
10) Chungulia kaburi.

Majibu:

1) Tangazo
2) Mwizi
3) Kufanya mkutano wa siri
4) Kuchochea ugomvi
5) Fichia siri
6) Kata tamaa
7) Kumpeleleza mtu siri yake
8) Kutamani
9) Maneno makali
10) Kunusurika kifo

Malizia methali zifuatazo:

1) Pema usiyapo pema ukipema
2) Mwenda omo na tezi
3) Macho
4) Mwapazia la nje
5) Kozi mwana Mandanda

.

Majibu:

1. si pema tena
2. marejeo ni ngamani
3. hayana pazia
4. hupata la ndani
5. kulala njaa kupenda

Badili sentensi zifuatazo kuwa katika kauli ya kutendwa:

1) Mama ameleta

zawadi Jibu:

❖ Zawadi imeletwa na mama

2) Vijana wanacheza

mpira Jibu

❖ Mpira unachezwa na vijana

3) Halima amempa Juma mpira

Jību:

❖ Juma amepewa mpira na Halima.

4) Asha amechota maji.

Jibu:

❖ Maji yamechotwa na Asha

5) Mbuzi amekula majani

Jibu:

- Majani yameliwa na mbuzi.

**a) Kubainisha na kuelezea mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa risala na kuelezea matumizi yake kwa usahihi kwa kuzingatia miktadha mbalimbali.**

**RISALA:**

**Risala** ni taarifa fupi inayosomwa mbele ya kiongozi au mgeni rasmi kwa niaba ya kundi fulani la watu ili kutoa maelekezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi

Dhima kuu ya risala ni kuwezesha kundi fulani la watu kuwasilisha hoja zao kwa kiongozi anayehusika. Risala ni njia mojawapo inayounganisha wananchi na viongozi wao.

Kupitia risala viongozi hupata mawazo ya wananchi na kuweza kuyafanyia kazi.

**MUUNDO WA RISALA:**

**Risala imegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni:**

**i. UTANGULIZI**

Hapa hukaa maneno ya utangalizi, maneno hayo huwa ni salamu, ukaribisho na maneno ya hamasa. Lengo la maneno haya ni kuwavuta wasikilizaji ili waweze kusikiliza

risala kwa makini na kwa hamasa. Pia hukaa kichwa cha risala.

**ii. MWANZO WA RISALA:**

Katika sehemu hii hukaa maelezo yanayofafanua lengo la risala kwa ufupi.

**iii. KIINI CHA RISALA:**

Sehemu hii huwa ndiyo risala yenyewe. Huonesha lengo la risala ni ya kikundi basi sehemu hii itaonesha jina la kikundi, historia ya kikundi, malengo yake, shughuli zake, mafanikio, changamoto, mapendekezo na maombi yao kwa mgeni rasmi.

**iv. MWISHO WA RISALA:**

Hapa huhusisha msimamo na maoni ya watayarishaji wa risala yanayotokana na mtazamo waliyonayo juu ya yale waliyoyaelezea katika risala. Pia sehemu hii huhusisha shukrani pamoja na hitinisho. Shukrani hutolewa kwa kutumia maneno machache sana.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA RISALA:**

i. Matumizi mazuri ya alama za uandishi mfano koma (,) nukta (.) ulizo (?) mshangao (!) "funga na fimgua semi" n.k

shukrani pamoja na niumisno. Snukran hutiwa kwa kutumia maneno machache sana.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA RISALA**

i. Matumizi mazuri ya alama za uandishi mfano koma (,) nukta (.) ulizo (2) mshangao (!) "funga na fungua semi" n.k
ii. Matumizi ya nyakati mfanowakati uliopo, wakati uliopita ujao.
iii. Matumizi mazuri ya lugha (lugha fasaha inayoeleweka)
iv. Mpango mzuri wa mawazo kimantiki. Epuka kurudiarudia mawazo. Kuchanganya mawazo nk
v. Matumizi bora ya sarufi ya lugha inayohusika.

- Hii ni kufuata kanuni za sarufi za lugha moja husika.

**RISALA:**

**RISALA YA WAFANYAKAZI WA KIWANDA CHA SHURUBATI BOMBA KWENDA KWA MGENI RASMI SIKU YA UZINDUZI WA KINYWAJI CHA SHUBATI BOMBA TAREHE 13/01/2021**

Ndugu mgeni rasmi, wageni waalikwa ndugu wafanyakazi wa kiwanda cha shurubati bomba, mabibi na mabwana.

Ndugu mgeni rasmi, kwa niaba ya uongozi wa kiwanda cha shurubati bomba ninayo furaha kuwa nanyi leo katika sherehe za uzinduzi wa kinywaji baridi kinachoitwa shurubati bomba. Uzinduzi wa kinywaji hiki utawezesha wakazi wa mkoa huu na mikoa jirani kupata kinywaji ambacho kinatengenezwa kwa matunda yanayolimwa hapa hapa mkoani kwetu. Kwa kuwa malighafi ya kutengenezea kinywaji hiki inatoka hapahapa ni Dhahiri kuwa kitauzwa kwa bei nafuu kabisa ukilinganisha na vinywaji vingine vinavyoingizwa mkoani kwetu kutoka mikoa mingine au hata nje

ya nchi.

Ndugu mgeni rasmi, kuzinduliwa kwa kinywaji cha shurubati bomba kitawapatia ajira vijana mia moja na ishirini na sita wa mkoa huu ambao watapatiwa mafunzo ya kutosha hapa hapa kiwandani ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Tayari vijana mia moja na kumi wameshaajiriwa katika idara mbalimbali za kiwanda.

Uchunguzi wa awali uliofanywa na wataalamu wetu unaonyesha kuwa, watu wengi wanapenda kinywaji cha shurubati bomba kuliko vinywaji vingine walivyovizoea. Sote tunajua kuwa shurubati bomba ni maji ya matunda na matunda yaani faida kubwa katika miili yetu.

Kwa heshima na taadhima ndugu mgeni rasmi tunakuomba utuzindulie kinywaji chetu.

Ndugu mgeni tunakushuru kwa kufika katika uzinduzi huu, kwani tunatambua kuwa una majukumu mengi ambayo umeyaacha kwa ajili yetu. Asante sana,

**A. UFAHAMU**

Jibu maswali yafuatayo:

1. Risala hii imetolewa na nani?

Jibu:

- Risala hii imetolewa na wafanyakazi wa kiwanda cha shurubati bomba,

2. Risala hii imetolewa kwenye sherehe ya nini?

Jibu:

- Risala hii imetolewa kwenye sherehe ya uzinduzi wa kinywaji cha shurubatia bomba

3. Vijana wangapi wameshaajiriwa katika idara mbalimbali za kiwanda cha shurubatia bomba?

Jibu:

- Vijana mia moja na kumi wameshaajiriwa katika kiwanda hiki cha shurubatia bomba.

**B. MAZOEZI YA LUGHA:**

Tunga sentensi kutokana na nahau zifuatazo.

1. Ona cha mtemakuni.

Jibu:

- Mwizi alipokamatwa alikiona cha mtemakuni

2. Kwa moyo mweupe

Jibu:

- ❖ Alipika ugali kwa moyo mweupe

3. Pigwa na

butwaa Jibu:

- ❖ Baba alipopata habari ile alipigwa na butwaa.

4. Buheri wa afya:

Jibu:

- ❖ Mama yangu ameugua kwa muda mrefu lakini kwa sasa ni buheri wa afya.

5. Ponea

chupuchupu Jibu:

- ❖ Juma alipokuwa anavuka barabara aliponea chupuchupu kugongwa na pikipiki.

Jaza nafasi wazi kwa kutega kitendawili chenye majibu hayo:

1. Kuna nywele nyota na mchanga hayo ni majibu ya kitendawili kipi?

Jibu

- ❖ Hesabu yake haina faida.

2. kinyonga amesimama juu ya tawi la mgomba. Kinyonga au mgomba ni majibu yay a kitendawili kipi?

- ❖ Huuawa na wazazi wake.

3. Konokono na kobe ni viumbe ambazo hutembea huku wamebeba nyumba zao. Kitendawili kipi ni majibu yake?

Jibu:

- ❖ Bibi hatui mzigo wake.

**(f) Kuandika risala kwa kuzingatia alama za uandishi na kuelezea matumizi yake katika miktadha mbalimbali.**

**ALAMA ZA UANDISHI**

Hizi ni alama zinazotumwa wakati wa kuandika pamoja na herufi. Kazi za alama hizi ni kutoa msaada wa kuelewa matini vema na kudokeza maana maalumu ya maneno au sehemu za sentensi na kuonesha muundo wa sentensi. Zipo alama mbalimbali za uandishi, nazo ni:-

- Nukta (.)
- Mkato (,)
- Ulizo (?)
- Apostroli au ritifaa (‛)
- Alama za dondoo (‟)
- Nukta mbili (:)
- Nukta Mkato (;)
- Kistari (-)

**i. Nukta**

Alama hii hutumika:-

a. Kuonesha mwisho wa

sentensi Mfano: Kioo

kimevunjika.

b. Hutumika kufupisha

maneno Mfano: C.C.M

c. Kuonesha hesabu isiyo

nzima Mfano: Kilo 8.2

d. Kuonesh

a saa Mfano:

Saa 2:30

**ii. Mkato**

Hutumika:-

a. Kuorodhesha vitu zaidi ya viwili

Mfano: Nimenunua kalamu, daftari na penseli.

b. Kugawanya mawazo katika sentensi

Mfano:

Nilipomuliza kama anamjua jirani yake, aliniangalia tu na kucheka.

c. Katika tarakimu

kugawa elfu Mfano:

200,000/=

**iii. Ulizo**

Hutumika kuuliza swali

Mfano:

Je, utamtembelea lini?

Unaitwa nani?

**iv. Mshangao hisi**

a. Hutumika kuonesha hisia kama vile hasira, mshangao,

furaha nk Mfano: :

Lo! Maji yote yamemwagika

Pepo nyeusi shindwa! Chomoka! Nenda kuzimu!

b. Pia hutumika kuigiza tanakali

sauti Mfano:

Moyo ulidunda ndu! Ndu!

**v. Nukta mbili**

Hutumika:

a. Kutanguliza

orodha Mfano:

Sherehe hiyo ilihudhuriwa na watu wengi: wake kwa waume, wazee kwa vijana

b. Kuonesh

a saa Mfano:

Aliingia saa 5:30

c. Kuonesha maneno ya msemaji katika tamthilia au mchezo wa kuigiza.

Mfano:

Mzee Masenza: unafikiri mimi ni nyanyako?

Kadogoo: Tafadhali nisamahee

d. Hutumika katika kumbukumbu za

mkutano Mfano:

Ajenda namba 2: Kusoma kumbukumbu za mkutano uliopita.

**vi. Nukta mkato (;)**

Hutumika kuunganisha vishazi huru viwili au kuonesha mawazo mawili.

Mfano:

Tuliwasili darasani tukiwa tumechelewa: mwalimu alitukaribisha kwa viboko.

Usiwe na wasiwasi; nitakuwa pamoja nawe siku zote.

**vii. Kistari (-)**

a. Hutumika kuunganisha maneno

mawili Mfano:

Mbwa-koko alimuuma mwana

haramu

b. Kuonesha hadi au

mpaka Mfano:

Bei imepandia kutoka shilingi 20 - 30

c. Kuonesha neno ambalo halijakamilika litaendelezwa katika mstari mwingine.

Mfano:

Ukitaka twende nyum-

bani nitakupeleka

**RISALA**

**RISALA YA WAHITIMU WA DARASA LA SABA KWA MKUU WA WILAYA**

Ndugu mgeni rasmi, mratibu wa Elimu kata, mwalimu mkuu, mwalimu mkuu msaidizi, mwalimu wa taaluma, mwalimu wa nidhamu, walimu wote, wazazi, wanafunzi, mabibi na mabwana, shikamooni. Napenda kuwakaribisha sana kwenye mahafali haya ya tano katika shule yetu msingi Sinza.

Ndugu Mgeni rasmi, shule yetu ilianza inwaka 2001 ukiwa na wanafunzi 50 tuu. Mpaka sasa shule hii ina jumla ya wanafunzi 450. Wasichana 250 na wavulana 200

Ndugu mgeni rasmi, katika kipindi chote hiki wanafunzi, wazazi na walimu wamekuwa wakishirikiana bega kwa bega kwa lengo la kunyanyua kiwango cha taaluma. Ushirikiano huo umezaa matunda mazuri sana kwani kuanzia shule hii ianzishwe hakuna mwanafunzi aliyehitimu shule hii na kushindwa kuendelea na masomo ya sekondari yaani kujiunga na kidato cha kwanza.

Ndugu mgeni rasmi, shule yetu inatambua umuhimu wa michezo. Hivyo basi, wanafunzi pamoja na walimu wanashiriki michezo kwa ukamilifu. Kwa kuwa tunatambua michezo hujenga akili na fikra kwa wanafunzi, shule yetu imeanzisha mashindano mbalimbali ndani ya shule na wanafunzi waweze kujifunza mambo mengi kutoka kwa wanafunzi wa shule zingine. Pia, imetia hamasa kwa wanafunzi kujifunza zaidi.

Ndugu mgeni rasmi, pamoja na mambo yote hayo hayo, shule hii baijabaki nyuma katika kuwapeleka wanafunzi katika safari za mafunzo Safari hizi huwasaidia wanafunzi kujifunza mambo mbalimbali nje ya darasa. Mafunzo hayo ni kama ya kihistoria, kijiografia na kisanaa. Safari hizi hufanyika katika makumbusho ya Taifa, Mbuga za wanyama na sehemu zingine kama hizo.

Ndugu mgeni rasmi, pamoja na mafanikio yote hayo bado shule yetu inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa vitabu vya kiada na ziada, uhaba wa maktaba, uhaba wa vifaa vya michezo, na uchakavu wa baadhi ya miundo mbinu. Pamoja na juhudi za

uongozi wa shule bado mambo hayo yamekuwa changamoto. Hivyo basi tunaomba wadau mbalimbali waweze kutusaidia katika kukabiliana na changamoto hizi.

Ndugu mgeni rasmi, matarajio yetu ni kufaulu katika viwango vya juu. Pia tunatamani shule hii iwe kituo bora chah kitaaluma ili tuweze kujenga Taifa bora lenye wananchi wenye elimu bora na wazalendo

Ndugu mgeni rasmi, wazazi, walimu na waalikwa wote, tunashukuru sana kwa kutusikiliza.

Tunategemea mtakua nasi katika kuboresha shule yetu. Asanteni sana.

**g) Kusoma magazeti mbalimbali yanayoelezea shughuli za kiclimu, kiuchumi na kisiasa na kubaini maneno mapya, kuelezea maana zake na kuyatungia sentensi kwa usahihi.**

**MAGAZETI:**

Magazeti ni karatasi zilizochapwa habari na kutolewa mara kwa mara au kila siku kila wiki. Pia, kuna magazeti yanayotolewa mara moja au mbili kwa mwezi mara nyingi gazeti huwa na habari za kisiasa, kiuchumi, kiutamnduni, michezo pamoja na hali ya hewa na ratiba za vipindi vya televisheni pamoja na burudani mbalimbali kama vibonzo, hadithi na vitendawili.

Sehemu nyingine muhimu ni matangazo ni matangazo ya biashara ambapo kampuni au watu hununua nafasi gazetini na kutangaza biashara, mkutano na mengineyo.

Soma habari hi kisha jibu maswali:

**TAIFA:**

Taifa ili liendelee linahitaji kuwa na uongozi bora na madhubuti pia, siasa safi. Lengo ni kujenga Taifa linalothamini uhuni, usawa, demokrasia, Amani na utulivu.

Ili uchumi wa Taifa uimarike na lazima wananchi wake wapate elimu na kufanya kazi kwa bidii. Ndio maana nchi yetu Tanzania inatoa elimu bure kuanzia darasa la kwanza (shule ya msingi) hadi sekondari

Elimu hii husaidia wananchi waweze kupambana na adui ujinga, maradhi na umaskini.

Tanzania ina rasilimali nyingi ikiwemo ardhi, mito bahari, ibuga za wanyama pamoja na madini. Hizo ni baadhi tuu ya rasilimali zetu. Vyote hivi husaidia katika kukuza uchumi wa nchi, hadi kwa sasa nchi yetu ipo katika uchumi wa kati.

Yote haya yamewekana kwa sababu ya kuwa na viongozi makini. Kiongozi ni mtu aliye mstari wa mbele kimawazo na kiutendaji. Kwa kuwa ni mtu aliyechaguliwa nawatu, wajibu wake ni kuhudumia watu watu. Ni msimamizi, lakini si mnyanyapara. Ni kiongozi mwadilifu sim la rushwa, si mbadilifu, si mwizi, si mzururaji, si mpika majungu bali kioo cha jamii.

**A. UFAHAMU**

1. Kutokana na habari uliyosoma Taifa ili iendelee linahitaji nini?

Jibu:

- ❖ Ili liendelee linahitaji kuwa na uongozi bora na siasa safi.

2. Ili uchumi uimarike ni lazima wananchi wake wapate nini?

Jibu: :

- ❖ Ili uchumi uimarike ni lazima wananchi wapate elim.

3. Taja rasilimali zilizopo Tanzania.

Jibu:

- ❖ Rasilimali zilizopo Tanzania ni mito, bahari, misitu, mbuga za wanyama pamoja na madini.

4. Taja sifa za kiongozi

mwadilifu Jibu:

- ❖ Sio mla rushwa
- ❖ Si mla rushwa
- ❖ Sio mwizi
- ❖ Si mwadilifu

**B. MSAMIATI**

Toa maana ya msamiati na kuitungia sentensi.

**1. Uchumi**

Maana:

- ❖ Mali iliyopatikana kutokana na amali za nchi za watu.

Sentensi:

- ❖ Raisi wetu alituambia kuwa na uchumi wa nchi yetu kwa sasa umepanda hadi kufikia uchumi wa kati.

**2. Rushwa**

Maana:

- Fedha au kitu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani ili mtoaji apewe upendeleo.

Sentensi:

Hayati baba wa taifa alitumbia rushwa ni adui wa haki.

**3. Mwadilifu**

Maana:

- Mtu mwenye kufuata maadili ya jamii yake kwa kiwango kikubwa
- Mpenda haki bila kupendelea.

Sentensi:

- Mbunge wetu ni mwadilifu sana.

**4. Badhirifu**

Maana:

- Kufuja mali

Sentensi:

- Mwalimu alituambia kwamba kiongozi mbadhirifu hata kuongoza

**C. MAZOEZI YA LUGHA:**

Andika wingi wa sentensi zifuatazo:

1. Mtoto wangu ametoroka nyumbani

- Watoto wangu wametoroka nyumbani

2. Mkulima amepalilia shamba lake

- Wakulima wamepalilia mashamba yao.

3. Mwanafunzi amempigia simu mzazi wake

- Wanafunzi wamempigia sim mzazi wake.

4. Kalamu ya Asha haiandiki kabisa

- Kalamu za Asha haziandiki kabisa.

5. Mzazi amemlipia mzazi wake wake karo ya shule

- Wazazi wamewalipia watoto wao karo za shule.

6. Mtoto wa Ana alichelewa shuleni

- ❖ Watoto wa Ana walichelewa sana.

7. Mwandishi anaandika kitabu.

- ❖ Waandishi wanaandika vitabu

8. Chakula hiki kina chumvi nyingi sana.

- ❖ Vyakula hivi vina chumvi nyingi sana.

9. Mwanajeshi amekwenda vitani

- ❖ Wanajeshi wamekwenda vitani

10. Kuku wangu ameangua kifaranga

- ❖ Kuku zangu zimeangua vifaranga.

Andika wingi wa maneno yafuatayo:

1. Joho
2. Mkanda
3. Nanasi
4. Sukari
5. Jiko
6. Chandarua
7. Ukuta
8. J

iwe

Majibu:

1. Majoho
2. Mikanda
3. Mananasi
4. Sukari
5. Meko
6. Vyandarua

7. Kuta
8. Mawe

## KUTUMIA MAANDISHI KATIKA MAWASILIANO KULINGANA NA MIKTADHA MBALIMBALI

### (a) Kubaini miundo ya barua za kirafiki na rasmi na kuiandika kwa kuitofautisha katika miktadha mbalimbali

**MAANDISHI:**

Maandishi (pia mwandiko) ni tendo la kushuka sauti za lugha kwa njia ya alama zinazoandikwa.

**MAWASILIANO**

Mawasiliano kwa kawaida hufafanuliwa kama kupashana au kubainishana mawazo, maoni, au habari kwa maneno maandishi au ishara.

Mawasiliano yanaweza kuelekea vyema kama mchakato kati ya wahusika wawili ambapo kuna mabadiliko na kukuza fikra, hisia au mawazo kufikia lengo lililokubaliwa au mwelekeo ulilokubaliwa.

Mawasiliano ni mchakato ambapo habari hupakiwa na kutumwa na kupashwa na mtu kwa anayepokea kupatia njia maalumu. Kisha anavepokea ujumbe hupakua ule ujumbe na kumpatia aliyetuma majibu. Aina zote za mawasiliano huhitaji mtumaji, ujumbe na mpokeaji.

Mawasiliano huhitaji kwamba wanaohusika wawe na jambo linalowaunganisha kimawasilano. Kuna njia zinazohusika kusikia kama vile uneneaji, wimbo, na toni ya sauti. Kuna zile zisizohusika kusikia kama vile macho na kuandika.

### a) Kubaini miundo ya barua za kirafiki na rasmi na kuandika kwa kutofautisha katika miktadha mbalimbali.

Barua ni ujumbe wa kimaandishi unaotumwa kwa mtu mwingine au watu wengine. Inawezekana kumwachia mtu ujumbe wa kimaandisi yaani barua mahali fulani lakini mara nyingi barua hutumwa kwa njia ya shirika jingine linalofanya kazi hii kibiasbara.

Kwa kawaida siku hizi barua huandikwa kwenye karatasi kwa kutumia kalamu au taipureta ama kwa kutumia kompuyuta na printa. Karatasi ya barua hukunjwa na kuwekwa ndani ya bahasha yenye jina na anuani ya mpokeaji juu yake. Siku hizi idadi kubwa ya ujumbe unaandikwa kwa njia ya barua pepe.

**BARUA RASMI:**

Barua rasmi ni barua ambazo zinahusu mambo ya kiofisi kama vile taarifa za mikutano, kuomba kazi kuagiza vifaa na shughuli zingine rasmi.

Barua rasmi zimegawanyika katika makundi matatu ambayo ni bania za taarifa, barua za maombi mbalimbali na barua za upokeaji vifaa.

Barua rasmi huandikwa kuelezea ujumbe maalumu. Kwa hiyo huhitaji kuandikwa kwa uangalifu na kwa umakini wa kutosha. Ni muhimu kuandika jambo husika waziwazi na kuepuka maelezo yasiyo muhimu kama vile salamu na kadhalika. Mwandishi analazimika kuandika kwa ufupi na lugha nyepesi. Barua rasmi huwa na sentensi chache tena fupi na ni lazima kufuata taratibu za uandishi.

**MUUNDO WA BARUA RASMI**

**1. ANWANI YA MWANDISHI**

Anuani ya mwandishi huandikwa katika barua yake juu, kwenye pembe ya upande wa kulia mwa karatasi.

**2. TAREHE**

Hii huandikwa upande wa kulia wa karatasi kashika karatasi chini ya anwani.

**3. KUMBUKUMBU NAMBA**

Hii ni namba ambayo huwa kama kitambulisho cha barua, bara nyingi huwa na taratibu pamoja na herufi mfano, MSS FV/03

**4. ANWANI YA MWANDIKIWA**

Hii hutanguliwa na cheo cha mwandikwa upande wa kushoto mwa karatasi chini ya namba ya kumbukumbu.

**5. MWANZO WA BARUA:**

Huandikwa chini ya anwani ya mwandikiwa, mara nyingi neno ndugu hutumika kamasalamu au mwanzo wa barua

**6. BARUA YENYEWE**

Hapa huandikwa mambo yote muhimu kuhusu barua yenyewe. Barua iwe fupi na taarifa muhimu tu.

**7. MWISHO WA BARUA**

Hapa huwa ni kimalizio cha barua: ni tamko la heshima la kumalizia barua mara nyingi miisho ambayo hutamkwa ni kama vile, “wako mtiifu", "wako katika ujenzi wa Taifa", "wako mwanachama" nk

**8. CHEO CHA MWANDISHI**

Mwisho wa barua, chini ya jina la mwandishi huandikwa cheo cheo aliyeandikwa barua cheo chaweza kuwa ni mwomboji, mwalimu wa darasa, mwanafunzi, waziri mjumbe wa tawi nk

**BARUA ZA KIRAFIKI:**

Barua za kirafiki na barua hundikwa kwa marafiki. Barua hizi zinaweza kuwa na dhamira mbalimbali kama vile taarifa za huzuni au furaha nk. barua hizi pia huitwa barua za kindugu kwa sababu ni barua ambazo huandikwa miongoni mwa watu wanaohusiana kama baba, mama, kaka, dada marafiki au ndugu wengine. Maksudi ya barua hizi ni kama vile

1. Kusalimiana baina ya ndugu.
2. Kuwajulisha ndugu na marafiki maisha yetu ya kila siku.
3. Kuomba msaada au kutoa shukrani kwa kutimiziwa maombi yetu.
4. Kutoa hongera, rambirambi nk

**MUUNDO WA BARUA ZA KIRAFIKI**

Barua ya kirafiki huwa na muundo ufuatao.

i. Tarehe, chini ya anwani
ii. Mtajo wa heshima kwa anayeandikwa kama vile mpendwa mpendi nk hivi huandikwa upande wa kushoto mwa karatasi baadaya tarehe
iii. Utangulizi wa barua ambao kwa desturi huwa ni salamu.
iv. Barua yenyewe ambayo ndiyo kiini cha waraka wenyewe
v. Salamu za kumalizia
vi. Hitimisho katika aya maalumu mfano, mi mimi mama yako nilikupandayo n.k
vii. Jina la mwandishi mwishoni

| BARUA ZA KIRAFIKI | BARUA RASMI |
|---|---|
| Huwa na anwani ya Mwandishi | Huwa na anwani mbili ya mwandishi tu mwandisbi na mwandikiwa. |

| | |
|---|---|
| Anuani ya mwandikiwa huwa nje ya bahasha | Barua ya mwandikiwa huwa kwenye barua na nje bahasha. |
| Haina kichwa cha barua inaanza na salamu | Haina salamau bali huanza kwa mwanzo maalumu, ina kichwa cha habari |
| Mwisho mwandishi huandika jina lake | Mwisho mwandishi huweka jina Pamoja na saini |
| Mwanzo wake hauhitaji wadhifa wa mwandikiwa | Huonesha cheo cha mwandikiwa |

**b) Kuelezea kanuni za uandishi wa barua va kirafiki na rasmi kutaja faida zake na kuelezea namna ya kuzitumia barua hizo katika mazingira ya kila siku.**

Kanuni za uandishi wa barua ya kindugu Barua ya kindugu hufuata taratibu za uandishi. Hutumia alama kama vile vituo, mkato, matumizi ya aya na mstari wa pambizo huzingatiwa

Kanuni muhimu za kuzingatia katika uandishi wa barua za kirafiki ni:

**1. Anwani ya mwandishi**

Hu huandikwa juu kwenye pembe ya kulia ya karatasi. Anwani huu ni muhimu iandikwe kwa usahihi kwani mwandikiwa ataitumia wakati wa kurudisha majibu ya barua iliyoandikwa

**2. Tarehe**

Hii buandikwa chini ya anwani ya mwandishi. Lengo ni kujumlisha mwandikiwa barua imeandikwa lini

**3. Mwanzo wa barua**

Sehemu hu huandikwa baada ya kuachwa mstari mmoja baada ya kuandikwa tarehe. Mwanzo wa barua huwa upande wa kushoto mwa karatasi. Maneno ambayo huweza kutumiwa ni kama mama mpendwa mpendwa kaka, nk

**4. Salamu**

Sehemu hii huandikwa chini ya mwanzo wa barua, ni sehemu ambayo huwa na salamu za mwandikiwa.

**5. Barua yenvewe /kiini cha barua**


Sehemu hii ndiyo huelezea kusudi la mwandishi. Mwandishi huelezea lengo mfano kuwajulisha wazazi maendeleo yake shuleni, afya yake, kuomba nauli ya kurudi nyumbani kipindi cha likizo, nk

**6. Mwisho wa barua**

Hapa hwa na salamu za kuagana, salamu hizi hutegemea pia uhusiano wa mwandishi na mwandikiwa. Mfano wako akupendaye, salaamu, rafiki yako.

**7. Jina la mwandishi**

Sehemu hii muhimu sana kwani husaidia kufahamu aliyeandika barua ni nani au barua imetoka kwa nani.



## MUUNDO WA BARUA YA KIRAFIKI

SHULE YA MSINGI MWABALOGI,
BARIADI – SIMIYU,
15/01/2021

Mpendwa rafiki

Habari yako, natumaini unaendelea vyema na shughuli zako za kila siku. Mimi pia ni mzima wa afya Dhumuni la barua hii ni kutaka kukujulisha kuwa kutufanya mtihani wa Taifa wa darasa la saba, mwezi wa nane mwishoni. Ni matarajio yangu kuwa, nitafaulu kujiunga na elimu ya sekondari.

Basi rafiki naomba nikutakie kila la heri katika maisha yako. Nisalimie wote wananifahamu

Rafiki yako mpendwa

**Mlelema Mgiwa.**

KANUNI ZA UANDISHI WA BARUA RASMI

**1. ANWANI YA MWANDISHI**

Mwandishi huandika anwani yake juu kwenye pembe ya upande wa kulia mwa karatasi.

**2 TAREHE**

Hii huandikwa upande wa kulia wa karatasi katika mstari uleule wa kumbukumbu ya barua kama ipi. Huwekwa chini ya anwani ya mwandishi

**3 NAMBA YA KUMBUKUMBU**

Hii ni namba ambayo huwa kama kitambulisho cha barua, Mara nyingi namba ya kumbukumbu huwa tarakimu, herufi au vyote kwa pamoja mfano KNO/NL/WAZ/004

**4. ANWANI YA MWANDIKIWA**

Anwani hii hutanguliwa na cheo cha mwandikiwa na huandikwa chini ya nambari ya kumbukumbu Nafasi ya mstari mmoja huachwa baina ya kumbukumbu na anwani mwandikiwa

**5. MWANZO WA BARUA**

Huandikwa chini ya anuani ya mwandikiwa Ni heshima kutaja cheo cha mwandikiwa mwanzoni wa barua rasmni. Mfano: ndugu Afisa taaluma, ndugu mwalimu mkuu.

**6. KICHWA CHA BARUA**

Kichwa cha barua hutaja kwa ufupi madhumuni ya barua Kichwa hiki huandikwa katikati mara baada ya mwanzo wa barua. Mfano YAH: RUHUSA YA LIKIZO YA UZAZI

Kichwa hiki huandikwa kwa herufi kubwa na kupigwa mstari

**7. BARUA YENYEWE**

Sehemu hu huandikwa mambo yote muhimu kuhusu barua yenyewe. Barua sharti iwe fupi na yenye taarifa za lazima tuu. Uanzaji wa barua umrejeshi msomaji kwenye mada ili kufupisha

maelezo mengi

Mfano: Mada hapo juu yahusika----------

**8. MWISHO WA BARUA**

Huwa Ni Kimalizio Cha Barua.

Ni tamko la heshima la kumalizia barua. Mara nyingi miisho ambayo hutumika katika barua za kikazi ni pamoja na wako mtiifu, wako katika ujenzi wa Taifa, wako katika kazi nk

**9. SAINI NA JINA**

Baada ya kimalizio cha barua, mwandishi alie saini na jina lake. Kwa barua zilizopigwa taipu, mwandishi lazima aweke au atie saini yake kwa mkono

**10 CHEO CHA MWANDISHI WA BARUA**

Mwisho wa barua chini ya jina la mwandishi huandikwa cheo. Cheo kinaweza kuwa mwanakijiji, katibu kata, mjumbe wa kamati ya kijiji, Wizara ya Elimu nk

Baada ya sehemu hii barua huwa imekamilika.

PARISHI YA AMANI
SLP 15
DAR ES SALAAM
17.01.2021

KUMB NA UBM 25/03

SHULE WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI AMANI

SLP 325,

DAR ES SALAAM

Ndugu,

**YAH: OMBI LA KAZI YA UALIMU WA SOMO LA KISWAHILI**

Rejea kichwa cha habari hapo juu. Mimi ni kijana mwenye umri wa miaka 20, ninaomba kazi ya ualimu katika shule yako kama ilivyotangazwa katika gazeti la majira siku ya jumatano tarehe 15/12/2020.

Ni mchitimu shahada yangu ya ualimu kwa somo la Kiswahili mwaka 2019 katika chuo kikuu cha Dar es salaam. Pia nimefanya kazi ya kufundisha kwa miezi sita katika shule ya wavulana Feza

iliyoko Mikocheni. Sambamba na hilo ninao uwezo mkubwa wa kutumia kompyuta Ninaambatanisha vivuli vya vyeti vyangu vya kidato cha nne, kidato cha sita na chuo kikuu

Ni matumaini yangu kuwa ombi langu litakubaliwa

Wako mtiifu,

A Sambusa

**Mwombaji**

Jibu Maswali:

1. Taja vipengele vya barua ya kirafiki:

Jibu:

- ❖ Vipengele vya barua ya kirafiki ni anwani ya mwandishi tarehe mwanzo wa barua, salamu, barua yenyewe, mwisho wa barua na jina la mwandishi

2. Taja vipengele muhimu katika barua rasmi Jibu:

- ❖ Vipengele muhimu katika barua rasmi ni anwani ya mwandishi, tarehe, namba ya kumbukumbu (kama ipo) anwani ya mwandishi, mwanzo wa barua kichwa cha barua, barua yenyewe mwisho wa barua, saini ya jina na cheo cha mwandishi wa barua

Hizi ni sehemu gani katika barua?

i. Wasaalamu, ni mimi mwanao Ana
ii. Nia hasa la barua hii ni kutaka kukuambia tutafanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi mwezi wa nane
iii. S.L.P 12 Bukoba
iv. YAH: MAOMBI YA RUHUSA SIKU SABA
v. Rejea kichwa cha habari hapo juu

Jibu:

i. Mwisho wa barua

ii. Barua yenyewe
iii. Anwani
iv. Kichwa cha barua
v. Barua yenyewe

3. Anwani ya mwandishi hukaa upande gani wa barua?

Jibu:

- ❖ Anwani ya mwandishi hukaa pembe ya upande wa kulia.

4. Anwani ya mwandikiwa hutangulia na nini?

Jibu:

- ❖ Anwani ya mwandikiwa hutanguliwa na cheo cha mwandikiwa

5. Tarehe ina umuhimu gani kwenye barua?

Jibu:

- ❖ Umuhimu wa tarehe ni kujumlisha mwandikiwa kuwa barua imeandikwa lini

**(c) Kubaini muundo wa kadi za mialiko kuandika na kuelezea matumizi yake.**

**KADI ZA MIALIKO**

Kadi za mialiko ni aina ya karatasi gumu lenye taarifa fupi ya kumwomba mtu /kumwalika itu ahudhurie kwenye sherehe au kikao fulani

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA KADI ZA MIALIKO**

i. Jina la mwandishi na anwani yake
ii. Jina la mwandikiwa
iii. Lengo la mwalikaji kwa ufupi
iv. Tarehe ya mwaliko
v. Mahali pa kukutana
vi. Wakati wa kukulana
vii. Jibu lipelekwe kwa nani

**AINA ZA KADI ZA MWALIKO**

### 1. Kadi za mwaliko usio rasmi

Hizi ni kadi zinazohusu moloko ya kindupi Kadi za namna hii zinapoandikwa, huwa hazitaji vyeo vya waalikwa, bali buanza na maneno kama vile Bwana bibi/Ndugu, n.k

**MFANO WA KADI YA MWALIKO USIO RASMI**

**MWALIKO WA KIKAO**

Familia ya Bibi Mwanaheri Mchele wa Kinondoni B Dar es salaam mayo furaha kukualika kuwaalika mamA/dada/bibi

__________________________________________________

Kwenye kikao cha Kitchen Party ya binti yao mpendwa Nyanichele kitakachofanyika siku ya Jumamosi ya tarehe 25.02.2021, saa 10.00 jioni nyumbani kwake Kinondoni B.

Kufika kwako ndiyo mafanikio yetu.

Mawasiliano.

Mwanaheri Kidawa: 0713 000000

Husna Rajabu: 0714 222 222

**2. Kadi za mwaliko rasmi**

Hizi ni kadi zinazohusu mialiko ya kiofisi mialiko ya sherehe mbalimbali mfano harusi, lakini katika uandishi wake majina huambatana na vyeo.

Mfano:

Profesa, Mchungaji, Daktari, Askofu, Sheikh, Mwalimu, n.k, hutumika pamoja na Ndugu/Bwana /Bibi

| |
|---|
| MWALIKO WA HARUSI<br>Familia ya Bwana & Bibi Uledi Shumbe wa Kinondoni DSM,<br>Wanayo furaha kukualika /kuwaalika<br>Mh/Askf/Dr/Mch/Sheikh/Pro/mwl/Bw & Bi<br>-------------------------------------------------<br>Kwenye sherehe ya harusi ya watoto wao wapendwa<br>Bakari Uledi<br>Na<br>Husna Yunisi<br>Itakayofanyika siku ya ijumaa ya tarehe 22/2/2021 kwenye ukumbi wa Kiramuu ulipo Mbezi juu, Dar es Salaam kuanzia 12:30 jioni.<br><br>Tafadhali njoo na kadi hii. Watoto tunawapenda lakini tuwaache nyumbani<br>Majibu (Kwa wasiofika tu)<br>Uledi Shumbe: 0755111111<br>Halidi Rajabu: 0766222222 |

Jibu maswali yafuatayo:

1. Nini maana ya kadi ya mwaliko?

Jibu:

- Kadi ya mwaliko ni aina ya karatasi gumu lenye taarifa fupi ya kumwomba mtu/kumwalika mtu ahudhurie kwenye sherehe au kikao fulani

2. Taja aina za kadi za mialiko.

Jibu:

- Kadi za mwaliko usio rasmi
- Kadi za mwaliko rasmi

3. Ni mambo gani muhimu mwandishi wa kadi za mwaliko anatakiwa kuzingatia katika

uandishi wake?

Jibu

- Mambo muhimu mwandishi wa kadi za mwaliko anapaswa kuzingatia ni:
- Jina la mwandishi na anwani yake
- Jina la mwandikiwa au mwalikwa
- Lengo la mwalikaji kwa ufupi
- Tarehe ya mwaliko
- Mahali na kukutania
- Wakati wa kukutana
- Jibu lipelekwe kwa nani.

Chagua neno sahihi kutoka kwenye kisanduku ili kujaza nafasi wazi.

| Familia, Ukumbi, Alasiri, Tarehe, Kuzaliwa, Musa Ali. |
|---|

__________________ya Bwana na Bibi Saidi Juma wa Ilala Dar es salaam wanayo furaha kukualika /kuwaalika Pro/Mch/Dr/Bwana Bibi

_____________________________________

Kwenye tafrija ya _________________mtoto wao Ali Saidi itakayofanyika jumamosi ya_______________22/3/2021 katika_______________________wa Isere DSM kuanzia saa 10 00

Tafadhala fika bila lakosa

**Majibu:**

- Familia
- Musa Ali
- Kuzaliwa
- Tarehe
- Ukumbi

- Alasiri

## KUTUMIA MSAMIATI KATIKA KUANDAA MATINI MBALIMBALI

**MSAMIATI:**

**Msamiati** ni maneno magumu ambayo yanatumika katika ufahamu au kifungu cha habari fulani. Kwa kawaida msamiati hufafanuliwa kabla ya kusoma habari

Vilevile tunaweza sema ni maneno magumu ambayo mtu hayaelewi katika habari fulani.

a) **Kutunga hadithi fupi na kuelezea maana za maneno yote mapya na kueleza jinsi yanavyotumika katika maisha ya siku.**

Hadithi ni masimulizi yenye kusimulia habari fulani ambayo hutumia lugha ya mjazo au nathari na mtiririko wake huwa ni mwepesi au sahili kwa ujumla zipo hadithi za kubuni na zingine za kihistoria

Hadithi huwasilishwa kwa hadhura kwa utendaji ambao unaweza kuhusishwa kwa utendaji ambao ambao unaweza kuhusishwa na sifa kadhaa Sifa hizo huitwa mbinu au mikakati ya usimulizi au utarnbaji katika jamii nyingi hadithi za mapokeo huwa na vitangulizi au mianzo maalumu. Mfano Paukwalpakawal hadithi hadithi, Hadithi njoo utamu koleal Atokeani! ------ Noam --- Twaibu nk

Mianzo maalumu ya hadithi huwa na majukumu kadhaa Huwa ni njia ya kuwavutia wasikilizaji pamoja na kuvuta umakmu wa hadhira Pia hutumwa kumtambulisha mtambaji wa hadithi, huashiria na kuonesha mwanzo wa hadithi

Katika jamii, kuna mtindo maalumu wa kumalizia hadithi Jamii nyingi huwa na kimalizio hadithi yangu imeishia hapo kimalizio huashiria mwisho au kumalizika kwa hadithi.

**HADITHI:**

Hapo zamani za kale, palitokea Mzee mmoja na mkewe Wolinmua kusafiri kuelekea nchi ya mbali. Siku ya kuondoka ilipofika wazee hawa waliwaita watu wa kijiji chao ili waweze kuagana nao. Watu walipofika wote na kuketi, mzee alisimama na kusema, "wanakijiji wenzangu, tangu zama za zama, tumekuwa tukiishi pamoja kama dada, kaka na ndugu na tumbo moja.

Mali ya kijiji hiki imekuwa mali yetu sote Ng'ombe na mbuzi wa kijiji hiki wamekuwa wetu pamoja. Mashamba ya kijiji hiki tumeyatunza pamoja. Najisikia huzuni kuagana nanyi."

**A. MSAMIATI**

Andika maana ya msamiati na kisha tunga sentensi

**1. Zama**

Maana:

- ❖ Ingia ndani ya maji na kwenda chini
- ❖ Toweka machoni
- ❖ Hutumika kuelezea nyakati mbalimbali (awamu, miaka hii, miaka

ile) Sentensi:

- ❖ Mwalimu wa historia alitufundisha kuwa zama za mawe za kale zimegawanyika katika makundi matatu.

**2. Ndugu**

Maana:

- ❖ Mtu aliyezaliwa nawe kwa baba, kwa mama au wazazi wote wawili
- ❖ Mtu wa ukoo mmoja
- ❖ Rafiki mkubwa
- ❖ Mtu unayeshirikiana naye katika shughuli za dini au siasa

Sentensi:

- ❖ Mwalimu wetu alifufundisha methali isemayo ndugu wakigombana chukua jembe ukalime, wakipatana chukua kapu ukavune"

**3. Mke**

Maana:

- ❖ Mwanamke aliyeolewa

Sentensi:

- ❖ Dini yetu ya kiislamu tunashauriwa kuoa mke zaidi ya mmoja

**4. Nchi**

Maana:

- Sehemu ya nchi isiyofunikwa na maji
- Sehemu ya ardhi katika ulimwengu iliyogawanyika kisiasa kwa mipaka na kutambulika kwa taifa lake

Sentensi:

- Nchi yetu Tanzania ni kisiwa cha Amani.

**B. UFAHAMU**

1. Akina nani walitaka kusafiri kwenda nchi ya mbali?

Jibu:

- Mzee mmoja na mkewe walitaka kusafiri kwenda nchi ya mbali.

2. Siku ya kuondoka ilipofika walifanya nini?

Jibu:

- Siku ya kuondoka ilipofika waliwaita watu wa kijiji chao ili waweze kuagana.

3. Mzee alisema mali ya kijiji imekuwa ya nani?

Jibu:

- Mzee alisema mali ya kijiji imekuwa yetu sote.

4. Mzee alijisikia uchungu kufanya nini?

Jibu:

- Mzee alijisikia uchungu kuagana na wanakijiji wenzake.

**C. MAZOEZI YA LUGHA**

Chagua neno katika kisanduku litakalokamilisha sentensi kwa usahihi.

| |
|---|
| Mhanga, Kinaganaga, Mahabusu, Gobole, Kuzirai, Aligwaya, Pomoni, Hadhara, Ahueni, Thabiti, Alilalama, Shahada |

1. Alisimama mbele ya_____________akahutubia mkutano
2. Ingawaje mwizi__________________watu wenye hasira waliendelea kumpiga
3. Asingekua na moyo__________________wezi wasingekamatwa
4. Mtoto aliyeiba nyama________________________alipokutana na baba yake mlango
5. Majambazi walivunja mlango wa ___________________
6. Yahaya alisomea________________ya uandishi wa Habari.
7. Yule kijana alijitoa____________________akamwokoa mwenzake

8. ________________ni silaha aina ya bunduki

9. Aliposikia habari ya kifo cha baba yake akaanguka na ________________________
10. Asha amepata________________baada ya kuugua kwa muda mrefu
11. Chupa hii imejaa maji ____________________
12. Wezi walipokamatwa wakaeleza________________jinsi walivyoiba.

**Majibu:**

1. Hadhara
2. Alilalama
3. Thabiti
4. Aligwaya
5. Mahabusu
6. Shahada
7. Mhanga
8. Gobole
9. Kuzirai
10. Ahueni
11. Pomoni
12. Kinagaubaga

Soma methali zifuatazo kisha jibu maswali:

i. Dunia tambara bovu
ii. Mganga hajinagi
iii. Lila na fila havitangamani
iv. Akiba halozi

Andika methali inayofaa katika maeleezo yafuatayo

1. Tujiwekee vitu vya kutusaidia wakati wa shida kwa sababu havitaharibika

- ❖ Methali: Akiba haioni

2. Tuwe waangalifu katika maisha yetu kwa sababu tukichezea maisha tutaharibikiwa

- ❖ Methali: Dunia tambara bovu

3. Mtu akifanya kazi yake bila umakini mambo hayatakuwa mazuri Ukijifanyia mambo yako bila kufuata utaratibu itabidi uyapokee na ukubali matokeo mabaya ya mambo hayo

- Methali: Mpanda ovyo hula ovyo

4. Umenielezea mambo mengi sana na mimi nimeyachambua na kuona yanayofaa na yasiyonifaa Ni lazima ujue mambo mazuri yana sehemu yake na mabaya kadhalika Ingawaje watu wema na waovu huishi pamoja lakini kila kundi linajibainisha

- Methali Lina na fila havichangamani
- Methali: Lina na fila havichangamani

5. Wewe unajifanya mwerevu sana lakini ukumbuke kuwa pamoja na werevu wako huwezi kuwa mwerevu kwa kila jambo.

- Methali: Mganga hajigangi

**Andika jina moja kwa kundi la maneno haya:**

1. Kasuku, kuku, mwewe, tai, kanga,
2. Buibui inzi, mbu, papasi, mbungo
3. Kanga, kizıbao, koti, gauni,
1. 4 Hiliki, vitunguu swaumu, mdalasini,
4. Zaituni zabibu embe, papai, matunda

**Majibu**:

1. Ndege
2. Wadudu
3. Mavazi
4. Viungo vya chakula
5. Matunda

**b) Kuandika insha inavoeleweka kuhusu uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia alama zote za uandishi.**

**INSHA**

**Insha** ni kifungu cha maneno kilichopangwa kwa mpangilio maalumu wenye kueleza kuhusu jambo fulani lililopangwa katika aya.

Insha huweza kueleza jambo fulani, mfano ugonjwa fulani, mauaji nk

**SEHEMU ZA INSHA**

Kwa kawaida insha imegawanyika katika sehemu kuna nne

**i. KICHWA CHA HABARI**

Hu ni sehemu ya kwanza ya insha ambayo huandikwa kitu kinachotakiwa kuzungumzwa Sehemu hii huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari, mfano **MATUMIZI YA DHARURA**

**ii. UTANGULIZI WA INSHA**

Hu ni sehemu ya pili ya insha ambapo mwandishi huelezea kwa undani zaidi kile kitu ambacho angependa kwenda kukiongelea kwenye insha insha yake katika sehemu hu mwandishi

huandika kwa ufupi tu kile anachotaka kukielezea.

**iii. KIINI CHA INSHA**

Hii ni sehemu ya tatu katika insha Sehemu hii mwandishi huelezea kwa undani zaidi kile kitu ambacho alipanga kukiongelea kwenye utangalizi na kichwa cha habari yake katika sehemu

hi mwandishi hupanga mawazo yake katika aya Kila wazo huwa na aya yake,

**iv. MWISHO WA INSHA**

Sehemu hu mwandishi huandikwa hitimisho la insha yake kwa kawaida sehemu hii huwa ni fupi na hupangwa katika aya nyingine,

**AINA ZA INSHA**

Zipo aina mbili za maisha. Aina hizo ni:

- Insha za kisanaa
- Insha zisizokuwa za kisanaa

Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa Insha

- Kuzingatia kichwa cha habari na kukitolea maelezo
- Kuandika kwa kutumia taratibu za uandishi na lugha fasaha
- Kutumia lugha ya mkato kama vile kuandikwa katika badala ya katika
- Kuandika utangulizi unaovuta umakini wa wasomaji au wasıkılızaji
- Kuandika kiini cha isha kwa mpangilio unaofaa kila wazo kuu lipewe aya yake. Mawazo ya aya yasihusiane

**INSHA**

## UHARIBIFU WA MAZINGIRA

Mazingira ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka binadamu au kiumbe katika maisha yake. Kwa hiyo kila unachokiona ni mazingira yako Mazingira huweza kuundwa na vitu mbalimbali; yanaweza kuwa ya asili kama misitu, milima, muziwa, mabonde, mito baliani na kadhalika Au ya kutengenezwa na binadamu kama majengo viwanda na kadhalika.

Uharibifu wa mazingira ni kitendo chochote kinachofanywa na binadamu ambacho kinapelekea mazingira kupotezea thamani yake ya asili. Shughuli zote za binadamu hutegemea uwepo mzuri wa mazingira

Kuna uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji taka ovyo, uchomaji wa mkaa, moshi wa viwandani, kwani mambo haya hupelekea kusambaa kwa hewa chafu au uchafuzi wa hewa. Uchafuzi wa hewa unaweza kusababisha maradhi kama vile saratani, kifua kikuu na kukohoa.

Vilevile shughuli za uchimbaji wa madini huweza kusababisha mmomonyoko wa udongo kwa kuacha ardhi kuwa wazi kutokana na Mashimo makubwa

Ukataji miti ovyo hupelekea kuwa na jangwa hivyo mito, chemchem hukauka. Hupelekea pia uhaba wa mvua Hapa binadamu au viumbe hukosa chakula kwani mazao hayastawi kutokana na uhaba wa mvua.

Hivyo mazingira hutunzwa kwa njia mbalimbali kama vile kupanda miti kwa wingi kutunza vyanzo vya maji, kuchoma misitu ovyo, kutokulima au kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji

**A UFAHAMU:**

**Jibu maswali yafuatayo**.

1 Nini maana ya mazingira?

- ❖ Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu, kama vile milima, misitu, majengo nk

2. Taja mambo yanayochangia kuharibika kwa mazingira

- ❖ Mambo yanayochangia kuharibika kwa mazingira ni
    i. Ukataji miti ovyo
    ii. Uchomaji wa misitu
    iii. Shughuli za uchimbaji madini
    iv. Moshi wa viwandani

3. Ni maana ya uharibifu wa mazingira

- Uharibifu wa mazingira ni kitendo chochote kinachofanywa na binadamu kinachopelekea mazingira kupoteza thamani yake ya asili

4. Madhara gani yanayoweza kutokea kutokana na uharibifu wa mazingira?

- Jangwa - kutokana na kukata miti ovyo pamoja na kuchoma misitu.
- Magonjwa kama kansa - kutokana na moshi wa viwandani.
- Mmomonyoko wa udongo - kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini

**B. MSAMIATI:**

Tunga sentensi kutokana na maneno haya.

**1. Mazingira:**

- Mma alituambia lazima mazingira ya nyumbani yawe safi kila wakati

**2. Misitu**

- Mwalimu wa Jiografia alitueleza kuwa mojawapo ya uoto wa asili ni misitu.

**3. Uharibifu**

Mama alituambia mtu yeyote atakayefanya uharibifu kwenye miundombinu, sheria itachukua mkondo wake.

**4. Moshi**

- Mama alituambia kuni mbichi hutoa moshi mwingi sana

**5. Mifugo**

- Nyumbani kwa babu yangu kuna mifugo mingi sana.

**6. Uchafuzi**

- Mwenyekiti wa kijiji cha Songambele aliwafundisha wanakijiji juu ya madhara ya uchafuzi wa mazingira

## C. MAZOEZI YA LUGHA:

Soma methali hizi kisha ziandike katika jozi ambazo zina maana sawa:

1. Baada ya dhiki faraja
2. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
3. Aibu ya maiti aijua mwosha
4. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
5. Mpenda chongo huona kengeza
6. Siri ya mtungi ajuaye kata
7. Kipenda roho hula nyama mbichi
8. Mchumia juani hulia kivulini
9. Koti la babu halikosi chawa
10. Jungu kuu halikosi ukoko

**Majibu:**

1. Baada ya dhiki faraja - Mchumia juani hulia kivulini
2. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu - Asiyetunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
3. Aibu ya maiti aijua mwosha - Siri ya mtungi aijuae kata
4. Mpenda chongo huona kengeza - kipenda roho hula nyama mbichi
5. Jungu kuu halikosi ukoko-koti la babu halikosi chawa

**Kwa kila neno ondoa herufi moja upate neno jipya**

1. Nazi___________
2. Budi _____________
3. Tibua _____________
4. Andama ____________
5. Daima________________

**Majibu:**

1. Nzi
2. Udi
3. Tibu
4. Ndama
5. Dama